**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 10 Agosti, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MUSTAFA H. MKULO):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 385

**Kilimo cha Tangawizi – Same**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa zaidi ya asilimia 7 (70%) ya wananchi wa Same Mashariki – Milimani wamejitokeza kulima zao la Tangawizi ambalo limeonyesha kustawi sana na kuwaongezea kipato; na kwa kuwa zao hilo linahitaji maji mengi sana kama vile maji ya Ndiva na Mabwawa:-

Je, Serikali kwa kuwajali wananchi wanaopenda na kuthamini kilimo nchini, itafanya jitihada gani kutoa elimu na misaada ya ujenzi wa Ndiva kwa wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA KLIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tangawizi hutumika kama kiungo katika kuongeza ladha, harufu na kuchangamsha katika vinywaji (kama soda, juisi, vilevi na kadhalika na vyakula mbalimbali (kama mikate, biskuti, keki, nyama za kusaga, achari na kadhalika).

Aidha, hutumika pia katika viwanda vinavyotengeneza madawa ya tiba mbalimbali (kama dawa za meno, kikohozi, tumbo na muwasho wa ngozi na kadhalika) pia hutumika katika vipodozi kama poda na kadhalika. Zao la Tangawizi lilianza kulimwa katika maeneo ya Same Mashariki – Mlimani, hususani katika kata ya Mamba tangu mwaka 1990, baada ya kuletwa na mkulima toka Wilayani Lushoto.

Serikali na baadhi ya wahisani wanaendelea kufanya jitihada za kuboresha kilimo cha umwagiliaji ambacho kinaboresha zao la Tangawizi katika maeneo ya Same Mashariki – Milimani kama ifuatavyo:-

(i) Shirika lisilo la Kiserikali la Uboreshaji wa Kilimo cha Umwagiliaji na Hifadhi ya Mazingira (*Traditional Irrigation and Environment Development Organisataion (TIP*) kuanzia mwaka 1995 limejenga na kukarabati jumla ya Ndiva 15 na mifereji 5 katika Kata ya Mamba. Shirika hili bado linaendelea na shughuli za uboreshaji wa kilimo cha umwagiliaji katika Kata ya Mamba.

(ii) Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*Participatory Agricultural Development and Empowerment Project (PADEP*) uliozinduliwa tarehe 20/3/2006 Wilayani Same, unaendelea na utekelezaji wa programu yake ya miaka mitatu ambapo utajumuisha kuboresha miundombinu ya umwagiliaji (Ndiva na mifereji pamoja na hifadhi ya vyanzo vya maji).

Shughuli zitatekelezwa kwa awamu mbili ambapo vijiji saba (7) kati ya 30 vitafaidika na mpango huo. Awamu ya kwanza itajumuisha vijiji 5, na awamu ya pili (2007) vijiji 2. *(Makofi)*

(iii) Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya. Halmashauri ya Wilaya ya Same, katika mwaka wa 2006/2007 iliomba Shilingi Milioni 18 ili kuwawezesha wakulima kuibua miradi mbalimbali kati ya Maendeleo na kuiboresha chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Program (ASDP*). Fedha hizi zilipatikana Januari, 2007 kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika vijiji 12.

Sera ya Serikali ni kutumia asilimia (75%) ya fedha zote za Bajeti ya Maendeleo ya kilimo zinazopelekwa kwenye Wilaya, zitumike kwa umwagiliaji. Hivyo tunashauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same uunge mkono jitihada za wananchi wa Same Mashariki – Milimani za kukuza zao la Tangawizi kwa kuliingiza kwenye Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya.

Aidha, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda ya Kilimanjaro, itasaidiana na Halmashauri ya Wilaya ya Same kuandaa miradi ya uvunaji maji (ndiva) na kuipendekeza kupewa fedha za *ASDP* kupitia *DADPS*.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata jibu kutoka kwa Naibu Waziri lakini kwanza ninamshukuru kwamba anazunguzia msisitizo wa jitihada ya Serikali ya kuboresha kilimo cha tangawizi katika kata moja tu, kata ya Mamba. Hili suala la kilimo cha tangawizi Jimboni kwangu siyo kwenye kata moja tu kama alivyoongea Mheshimiwa Naibu Waziri lakini sasa ni kata 12 zote za Same Mashariki – Milimani zinalima tangawizi na kwa kuwa hili zao sasa limezagaa mpaka limeteremka kwenye kata za tambarare na linastawi sana na wananchi wamejikita kwenye zao hili.

Je, Serikali haini kwamba ilikuwa imejikita kwenye kata moja tu na sasa ni zaidi ya kata 12 ambazo zinalima zao hili kwa hivyo tunahitaji nguvu ya ziada kupeleka pesa za kutengeneza ndiva?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa sasa hivi tuna tatizo moja la kwamba nchi jirani zote zinaingia kinyume cha taratibu kwenye kata zangu kule Same Mashariki - Milimani na kununua tangawizi kwa wananchi moja kwa moja na hili halmashauri inafahamu.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuisaidia halmashauri kunitafutia masoko ya nje ya uhakika kuliko ambavyo sasa hivi, nchi mbalimbali zinaingia na malori na kuchukuka tangawizi kutoka kwa wananchi wangu kwa bei ya kutupa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anne K. Malecela, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kujikita kwenye kata moja, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Anne Kilango, kwamba tunapoanza shughuli yoyote

kulingana na fedha zilizopo au hata tunapoanza mpango ili uweze kuendelea lazima tuanzie na mahali fulani. Lakini nakubaliana naye mimi mwenyewe nimetembelea katika jimbo hilo, katika wilaya hiyo nimeona jinsi tangawizi ambavyo inazidi kuongezeka siku hadi siku na kwa taarifa yake pia mimi nimeolea kule kwa hiyo napajua vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi mimi nilisema *PADEP* imeanza utaratibu katika vijiji 12 na tunaendelea kupanua jinsi fedha zinavyopatikana. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi kwamba tumejikita kwenye kata moja tu hapana, na wala siyo katika kata moja au katika jimbo moja tu lengo letu ni kupanua kilimo cha tangawizi katika sehemu nyingi za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ununuzi wa tangawizi mimi nadhani kama alivyosema mwenyewe ni jukumu la Halmashauri ya Wilaya na *local authorities* kuhakikisha kwamba ulaliaji wa wakulima hautokei na si kazi ya Wizara ya Kilimo peke yake.

Lakini kwa upande wa Serikali ningependa kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba ziko jitihada mbalimbali za Serikali katika kuboresha kilimo cha tangawizi na moja ni kwamba wenzetu wa Wizara ya Biashara, Masoko na Viwanda inaandaa mpango ambao utahusika na kuuza ya nje yaani *intergrated export program* huu mpango lengo lake ni kukuza mazao haya hususan mazao ya viungo kama tangawizi.

Lakini pia nimkumbushe kwamba Wizara hiyo hiyo inaandaa sera ya masoko ya mazao ya kilimo na sera hiyo itakapokuwa tayari Wizara ya Kilimo nayo itaingia na mchakato wa kuanzisha bodi ya mazao mchanganyiko ambayo pia itahusisha na mazao haya.

Na. 386

**Kiwanda cha Sukari Kilombero**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kiwanda cha Sukari cha Kilombero hununua miwa kutoka kwa wakulima wakubwa na kuacha miwa ya wakulima wadogo ikiozea mashambani na kwa kuwa, wakulima wadogo wanategemea sana kilimo hicho kwa maisha yao ya kila siku:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, wakulima wadogo wadogo wa zao la miwa wa Kata ya Kidatu, Mkata, Sanje, Mang'ula, Kiwawasawa na Kiberege wanafaidika na uwepo wa Kiwanda cha Sukari cha Kilombero?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Ubinafsishaji wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero, Mwekezaji alikarabati mitambo ya kusindika miwa na kuendeleza mashambo yote ya kampuni. Aidha, mwekezaji alihamasisha wakulima katika maeneo yanayozunguka kiwanda walime miwa wakiwa na uhakika kwamba itapata soko kiwandani. Kutokana na hatua hizo zilizochukuliwa na mwekezaji, uzalishaji wa sukari katika Kiwanda cha Kilombero umeongezeka kutoka tani 61,688 katika mwaka 2000/2001 hadi tani 136,941 katika mwaka wa 2005/2006. Uzalishaji huo ni sawa na asilimia 52 ya uzalishaji wa sukari kwa viwanda vyote nchini uliofika tani 263,317 katika mwaka wa 2005/2006. Kwa mwaka wa 2006/2007, kampuni inatarajia kuzalisha tani 103,000 za sukari. Miwa ya wakulima binafsi inatarajiwa kuchangia asilimia 49 ya sukari itakayozalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

Katika kuhakikisha kwamba wakulima wadogo wadogo wa miwa wanafaidika na kuwepo kwa Kiwanda cha Sukari cha Kilombero, Serikali kwa kupitia Bodi ya Sukari inahakikisha kuwa wakulima wote wa miwa wanasajiliwa na Bodi ya Sukari ili waweze kuuza miwa yao kiwandani. Bodi ya Sukari tayari imekamilisha zoezi la kuorodhesha wakulima wa miwa wa Kilombero kutoka Kata za Kidatu, Mkata, Sanje, Mang'ula, Kisawasawa na Kiberege, ambapo zaidi ya mashamba 14,000 yameorodheshwa. Aidha, Bodi ya Sukari inaandaa utaratibu wa kuwasajili wakulima hao, ikiwa ni pamoja na kutambua ukubwa na mashamba yao na wastani wa miwa inayotarajiwa kuzalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa kuuziana miwa kati ya kiwanda na wakulima unasimamiwa na Kamati ya pamoja inayojumuisha wajumbe wa kiwanda na wale wa chama cha wakulima wa nje ya kiwanda. Utaratibu wa kuvuna miwa ni sehemu ya mkataba na haubagui wakulima wakubwa na wadogo. Hata hivyo, katika msimu wa 2004/2005, baadhi ya mashamba ya wanavijiji hayakuvunwa kwa sababu ya mvua kubwa iliyonyesha kabla ya mwisho wa msimu na kuathiri uvunaji wa miwa. Tatizo hili lilikuwa nje ya uwezo wa kiwanda.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilitaka kujua tu kwa kuwa amekiri kwamba kumekuwa na nyongeza kubwa sana ya uzalishaji kwa asilimia 52 kwa miaka aliyoitaja.

Je, nilikuwa nataka kujua kwa kiwanda cha *TPC* kule Moshi, kwa nini kule bado kuna matatizo hasa ukizingatia kwamba Kilombero kumekuwa na uzalishaji mzuri zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba *TPC* tofauti na viwanda vingine haina *out growers*, haina wakulima wadogo wadogo. *TPC* ina matatizo kati ya uongozi na wafanyakazi wake wa viwandani ndio tatizo walilonalo kule lakini wakulima wenyewe kama wakulima hawana matatizo hayo. Hata hivyo tunaendelea kutumia vyombo mbalimbali kama mashirikisho ya vyama vya wafanyakazi kujaribu kutatua migogoro ya ndani iliyopo katika *TPC* na tuna hakika kabisa kwamba baada ya muda kutakuwa na suluhisho kwa sababu taarifa nilizonazo ni kwamba hali ile sasa iliyokuwepo inayotishia hata kuuwa kiwanda imeanza kupungua.

Na. 387

**Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii**

**MHE. FELISTA A. BURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sera ya Hifadhi ya Jamii iliundwa mwaka 2003 na kwa kuwa, kuchelewa kwa Sera hiyo kumesababisha kutokuwepo kwa udhibiti wa masuala ya Hifadhi hiyo na mfumo mmoja wa utoaji huduma katika Nchi yetu.

Je, ni lini Serikali italea Muswada wa Sheria Bungeni ili kuwezesha Sera hiyo kutekelezeka.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Felista Bura, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003, ni kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya kuhakikisha wafanyakazi wote nchini wanakingwa na majanga yanayotokana na kupungua au kupoteza uwezo wa kufanya kazi. Mifumo ya Hifadhi ya Jamii iliyopo sasa inatekeleza kwa sehemu kubwa lengo la Sera hiyo. Hata hivyo Sera imetamka wazi, kuhusu uundaji wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii ili kuboresha utoaji wa huduma za Hifadhi ya Jamii ikiwa ni pamoja na kwa na Mfumo mmoja wa utoaji huduma hiyo katika nchi yetu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, waraka wa mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria ya Kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii, umeshaandaliwa na kuwasilishwa *Cabinet Secretariat* na kujadiliwa ngazi ya *IMTC*. Hivi sasa unasubiri kujadiliwa ngazi ya Baraza la Mawaziri na hatimaye maekelezo yatokanayo na Baraza yaweze kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kuwasilishwa Muswada huo Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa Muswada utakaowasilishwa Bungeni utaimarisha mfumo wa Utawala bora, kwa kuhakikisha kuwepo kwa Taasisi endelevu za Hifadhi ya Jamii, kuundwa chombo cha usimamizi na kupanua wigo wa huduma za Hifadhi ya Jamii, na hivyo kuwezesha Sera ya mwaka 2003 kutekelezeka kama ilivyokusudiwa.

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pamoja na majibu hayo nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa sheria hii ya kuratibu mashirika ya hifadhi ya jamii au mifuko ya hifadhi ya jamii imechelewa kutoka na kufanya mifuko hii ilipe mafao kwa wafanyakazi kufuatana na sheria iliyounda mifuko hiyo.

Je, Serikali haioni kwamba kucheleweshwa kwa sheria hii kumewagawa wafanyakazi kwamba wapo ambao wanalipwa mafao mengi na wapo ambao wanalipwa mafao machache?

Je, Serikali haioni kwamba imewagawa wafanyakazi kufuatana na muundo huo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Felista Bura, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli inaweza kuonekana kwamba sheria hii ambayo inakusudiwa kuongoza sekta ya hifadhi ya jamii kuchelewa lakini sasa kama nilivyosema tumefika mahali pazuri, matayarisho ya waraka yameshapita kwenye *secretariat* ya Baraza la Mawaziri pia imeshazungumzwa kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu na sasa inasubiri kupita kwenye hatua ya Baraza la Mawaziri na kama itampendeza Mheshimiwa Rais basi Muswada huo utaletwa Bungeni na kutungiwa sheria. Mpaka sasa hivi tunayo mifuko na kila mfuko unaendeshwa kisekta kwa hiyo inaweza kudhaniwa kwamba kwa kufanya hivyo ni kugawa wafanyakazi lakini sisi tunaamini kwa sababu sasa kuna sheria ambayo mojawapo ya lengo lake ni kuunganisha mifuko hii ingawaje bado inaelekea kwamba uamuzi utakuwa kila mfuko ubaki kuendelea kwenye Wizara ya sekta yake utatua tatizo hilo ambalo kimsingi si sahihi.

Na. 388

**Shule za Sekondari Kila Kata**

**MHE. MGANA I. MZINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri ya kushirikiana na wananchi katika mpango mzima wa ujenzi wa shule za sekondari kila Kata ili kuhakikisha vijana wetu wengi wanaomaliza darasa la saba wanajiunga na shule za sekondari:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kutosha kwenye shule za sekondari za Chemchem, Gumanga, Nkinto,Mwanga, Kinyangiri, Ilinda na Iguguno?

(b) Je, Serikali haioni kwamba ujenzi wa madarasa ni lazima uambatane na ujenzi wa nyumba za walimu, hosteli, za wanafunzi katika kipindi hiki ambacho wanafunzi wanaofaulu wanapangiwa shule yoyote Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007 Shule za Sekondari za Wilaya ya Iramba zilipangiwa walimu 206 kati ya hao walimu 149 waliripoti na walimu 57 hawakuripoti. Aidha, shule zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge ziipangiwa walimu kama ifuatavyo:- Chemchem walipangwa 5, walioripoti 3, Nkinto walipangwa 9, walioripoti 7, Mwanga waliopangwa 10, walioripoti 6, Kinyangiri waliopangwa 10, walioripoti 7, Ilunda walipangwa 6, walioripoti 6, Iguguno waliopangwa 3, walioripoti 3 na Guwanga waliopangwa 5, walioripoti 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea na jitihada za kuajiri walimu wa Stashahada na Shahada na kuwapanga katika Mikoa kadri watakavyopatikana. Mkoa utawapanga walimu hao katika shule za sekondari kwa kuzingatia shule zenye uhaba mkubwa wa walimu. Tunaomba wananchi kuendelea kuboresha mazingira hasa ujenzi wa nyumba za walimu ili walimu wapate mahali bora pa kuishi na kuandaa mapokezi mazuri kwa walimu wapya wanaopangwa katika maeneo yao.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa ujenzi wa madarassa katika shule ni lazima uambatane na ujenzi wa nyumba za walimu. Kwa mujibu wa Waraka wa Elimu Na. 12 wa mwaka 2004, ujenzi wa madarasa unapaswa kwenda sambamba na ujenzi wa nyumba za walimu kwa kiwango cha madarasa mawili kwa nyumba moja ya mwalimu. Katika mwaka 2007/2008 Wizara imeweka kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za walimu kwa kuchangia nguvu za wananchi katika ujenzi wa nyumba 1500 kama Mheshimiwa Waziri wa Elimu alivyozungumza kwenye Bunge.

Aidha wanafunzi wachache kati ya waliofaulu kwa alama za juu katika mitihani wa darasa la saba hupata nafasi ya kuendelea na masomo katika shule za sekondari za kitaifa ambazo zina mabweni.

Wanafunzi wengi hupangwa katika sekondari za Kata zilizopo kwenye maeneo yao ambazo kimsingi ni za kutwa. Maeneo ambayo makazi ya wananchi yametawanyika kiasi cha wengi kuwa mbali na ilipo shule ya Kata, wanashauriwa kujenga hosteli ili

wanafunzi hao wakae katika mazingira ya shule. Serikali itachangia ujenzi wa hosteli kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MHE. MGANA I. MZINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa niulize swali la nyongeza na vile vile ninampongeza Waziri kwa majibu mazuri. Kwa kuwa nchi nzima wameona umuhimu wa elimu ya sekondari na kwa kuwa wanakuwa tayari kuchangia lakini Serikali inachelewa kupeleka fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Je, hili litasahishwa ili madarasa, nyumba za walimu na hosteli zijengwe mapema?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu la nyongeza la Mheshimiwa Msindai kama ifuatavyo. Ni kweli kabisa wananchi sasa wamejitolea sana katika ujenzi wa Shule za Sekondari hasa matokea ya mwaka uliopita wa fedha ambapo wananchi wameweza kujenga shule 1,084, lakini kama tulivyoshuhudi katika bajeti ambayo Waheshimiwa Wabunge mmetupitishia ya Wizara ya Elimu na vipaumbele ambavyo tumeviweka ni katika suala la kujenga madara 800 na kujenga nyumba za walimu 1,500.

Fedha hizi zikipatikana Serikali haitaziweka itazipeleka moja kwa moja kwa wananchi ili waweze kushiriki vema katika ujenzi wa madarasa, si kazi ya Serikali kuziweka zile fedha, faida kubwa ni fedha zifike kwa wananchi ili waweze kuzitumia kwa kujenga madarasa kwa sababu mwamko huo Serikali imeuona na ndio maana imejitolea au umejitosa mwaka huu kuhakikisha kwamba fedha hizo zinapelekwa kila zinapopatikana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba wako walimu wengi ambao hawakwenda kuripoti katika shule walizopangiwa za sekondari Wilayani Iramba.

Je, Serikali inatambua kwamba walimu wanashindwa kwenda kuripoti na kufundisha katika shule hizo kutokana na mazingira magumu yaliyoko huko?

Je, Serikali haioni sasa kuna sababu ya kutoa pesa ya mazingira magumu ili iwe kichocheo kwa walimu hawa kukubali kwenda kufundisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK JOHN MWANANZILA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Walimu wengi hawakuripoti katika Wilaya ya Iramba lakini si Iramba peke yake sehemu mbalimbali nchini hasa Mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Rukwa, Ruvuma, Mtwara na hata Lindi Walimu wengi tuna taarifa kwamba hawakwenda kuripoti.

Wizara imeshalitambua hilo na imeshaagiza kabisa katika msimu ujao Walimu watakaomaliza katika vyuo vyetu mahali watakapopangiwa wasipokwenda kuripoti basi hawatapata mishahara yao. Kwa hiyo, tunashauri kabisa kwamba wale Walimu wapya watakaokuwa wanamaliza kila mmoja mahali atakapopangiwa asibadilishe kituo kwa sababu haitawezekana tena kupata mshahara wake kwa urahisi.

Sasa kuhusu suala la Walimu kupata posho ya mazingira magumu. Suala hili limefanyiwa kazi ikiwa ni katika Tume iliyoundwa na Rais ya kuboresha mazingira ya kazi na posho ya wafanyakazi wote. Hili suala limejadiliwa na kina na ninaomba Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi na Walimu waliopo nchini wawe na subira ili Serikali iweze kuona suala hili litatekelezwa namna gani.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara hiyohiyo na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Lucy T. Manyenga kwa niaba yake Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni atauliza.

Na. 389

**Fedha za Mpango wa MMES.**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. MHE. LUCY T. MAYENGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Halmashauri zilisimamia vizuri za Mpango wa MMEM; na kwa kuwa kitendo cha fedha za MMES kuendelea kusimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kumesababisha malalamiko mengi kutoka kwa wananchi hasa kutokana na utendaji wa baadhi ya Walimu Wakuu na Walezi wanaopewa fedha hizi.

(a)Je, ni sababu zipi zinafanya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi isiache hela za MMES zisimamiwe na TAMISEMI ambayo ina watendaji wengi na waliopata uzoefu kutokana na Mpango wa MMEM?

(b)Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka kwa shule za sekondari za wananchi nazo kuwa chini ya Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK JOHN MWANANZILA):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2007/2008, Serikali imepanga kusaidia ujenzi wa madarasa 800 katika shule ambazo zimekwishaanzishwa. Kwa kuwa shule hizo sasa zinazo Akaunti za Benki fedha za MMES zitatumiwa moja kwa moja kwenye shule zitakazopendekezwa na Mikoa. Aidha, Serikali inaangalia uwezekano wa kutumia utaratibu mpya wa kujenga nyumba za Walimu na madarasa kwa kutumia taasisi au vikosi vya Jeshi kama vile JKT, JWTZ, *NSSF* na kadhalika. Fedha za MMES kusimamiwa na TAMISEMI ni suala ambalo bado linafanyiwa kazi hasa tukizingatia masharti ya Benki ya Dunia.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Shule za Sekondari za Wananchi hujengwa na wananchi kupitia Halmashauri zao. Serikali Kuu ina jukumu la kuziendesha kwa maana ya kuzipatia walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kufuatilia utekelezaji wa mitaala katika shule hizo. Hata hivyo Serikali ipo katika mchakato wa kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa kwa kuhamisha baadhi ya majukumu ambayo yatatekelezwa vizuri na Halmashauri. Kwa hiyo suala la Shule za Sekondari za Wananchi kuwa chini ya Halmashauri kiundeshaji ni miongoni mwa majukumu yatakayotazamwa katika mchakato wa *D by D.*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa katika mchakato mzima wa shule hizi za Sekondari kupitia mpango wa MMES umejitokeza kuwa na malalamiko ya baadhi ya Walimu Wakuu wa shule hizi kushindwa kuwashirikisha wananchi kikamilifu katika suala zima la uwazi wa matumizi ya fedha. Je, Serikali haioni kwamba ni vema suala hili likaeleweshwa vizuri kati ya wananchi na hao Walimu Wakuu wa shule ili raslimali hizi ziweze kutumika kama ambavyo Serikali imetazamia?

Pili, kwa kuwa Serikali sasa imeamua kwa dhati kufanya mpango huu wa D by D yaani *Decentralisation by Devolution.* Je, Mheshimiwa Waziri haoni kusema kwamba Serikali inaangalia tena utaratibu mpya wakati Serikali hiyo hiyo imeshaazimia kuanzia Bajeti hii kutekeleza mpango wa *D by D* itakuwa ni kupinga na dhana nzima ya Serikali kwa suala la kuwawezesha wananchi kuweza kuhimili shughuli hizi kwa pamoja?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri naomba majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK JOHN MWANANZILA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni kama ifuatavyo;

Ni kweli yapo malalamiko kwamba Walimu Wakuu wa shule za sekondari kwa muda mrefu wamekuwa hawashirikishi wananchi katika maeneo yale katika fedha zile za MMES zinazopelekwa kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wizara yangu imeelekeza kwamba fedha hizi hawatazipata bila maelezo yale kufika kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya pamoja na Kata yaani pamoja na Diwani kuzifahamu na ndiyo maana tunawashauri Waheshimiwa Wabunge na ninarudia suala hili tena kwa mara ya pili kwamba Waheshimiwa Wabunge itakapofika fedha zimepelekwa katika Mikoa yenu nendeni mkahakikishe kwamba fedha hizi zinagawiwa sawasawa katika Wilaya zenu na katika Kata zenu ili msimamie kwa karibu usije ukakosa katika shule yako unayopanga wewe ipate fedha.

Hakikisha unakuwepo pale, msipokwenda kama mlivyokwenda mwaka jana wengi walianza malalamiko kwamba fedha zimegawiwaje wakati ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge tuliwaeleza kwamba muende mkasimamie. Nendeni mkasimamie ugawaji wa fedha hizi ili muweze kupata kwa usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu suala la *D by D.* Mpango wa Wizara ya Elimu tayari tumeshateua Waratibu wa Elimu ya Sekondari katika kila Wilaya hivi kila Mbunge akienda katika Wilaya yake amtafute Mratibu wa Elimu ya Sekondari ambaye tayari yuko katika kila Wilaya. Huu ni mwanzo tu wa mpango wa *D by D* katika Wizara yetu, tutaendelea mpaka tuhakikishe kwamba suala hili tunalitengeneza kadri Serikali ilivyoagiza. (*Makofi*)

**MHE. JACKSON MUVANGILA MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Uzoefu unaonyesha kwamba katika ujenzi wa shule hizi za Sekondari na mafanikio haya ujenzi wa maabara umeonekana ni mgumu na wa gharama kubwa sana. Kwa hiyo, shule karibu robo tatu zilizojengwa na tunazozijua na tunazozitaja hapa hazina Maabara. Maabara zinahitaji utaalamu wa hali ya juu sana katika kujenga.

Je, Wizara haioni umuhimu wa maabara kujengwa na Wizara yenyewe na kwa sababu ya gharama zilivyo kubwa kuchagua shule chache katika nchi badala ya kudhani kwamba kila shule itakuwa na maabara?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK JOHN MWANANZILA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Jackson Makwetta, ambaye awali alikuwa Waziri wa Elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa maabara katika shule zetu za sekondari, lakini kama mnavyoelewa tulipokuwa tunapitisha Bajeti ya Wizara hii tuliweka vipaumbele katika Wizara yetu, pamoja na Serikali kuwa na vipaumbele vyake na Wizara ya Elimu ikapata fedha nyingi lakini na Wizara yenyewe ilikuwa na vipaumbele vyake ni pamoja na kujenga madarasa ili wanafunzi waweze kupata mahali pa kusomea lakini tupate pia na nyumba za Walimu. Lakini suala la maabara na lenyewe tumeliwekea maanani kwa mwaka huu tunajenga maabara karibu 84

nzima, tunajua haitoshi lakini fedha zinapopatikana tutahakikisha kwamba na maabara zinajengwa kwa kadri ya mahitaji ya shule zetu.

Lakini pia ninashauri Waheshimiwa Wabunge pamoja na kwamba maabara hazitasambazwa kwa urahisi katika shule zote Waheshimiwa Wabunge tunaomba pia mtusaidie kununua vivunge vya sayansi ambavyo vina vifaa vya msingi kwa ajili ya kufundishia sayansi katika shule zetu. Wanaweza kutumia vile vivunge katika kujifunza *principles* nyingi za sayansi katika shule zao. Tunaomba tushirikiane katika kuhakikisha kwamba tunafanya hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Miundombinu, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki.

Na. 390

**Ujenzi wa Barabara ya Arusha – Babati – Dodoma – Iringa**

**MHE. MARIAM S. MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Dodoma wanafarijika sana wanaposikia maelezo ya Serikali jinsi inavyoshughulikia ujenzi wa barabara ya Arusha, Babati na hasa Babati, Dodoma, Iringa na kwa kuwa, upembuzi yakinifu ulishaanza:-

(a) Je, Kazi ya upembuzi yakinifu imefikia wapi na lini itakamilika?

(b) Je, baada ya upembuzi yakinifu kukamilika, ni lini kazi ya ujenzi itaanza rasmi?

(c) Je, fedha za ujenzi zitatoka wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mbunge Viti Maalum, lenye a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Arusha – Babati – Dodoma hadi Iringa yameanza na yapo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Arusha (Minjingu) – Babati (61 km), Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na maandalizi ya nyaraka za zabuni vimekamilika.

(ii) Dodoma – Babati (261 km), Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika na hivi sasa Mhandisi Mshauri anaendelea na usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni. Kazi zote zitakamilika katika mwaka wa fedha 2007/2008.

(iii) Dodoma – Iringa (267 km), Mkataba wa Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni ya ujenzi unatarajiwa kutiwa saini mwezi huu Agosti 2007. Kazi ya usanifi wa kina kwa barabara ya Arusha – Babati – Dodoma hadi Iringa, inagharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Nchi za Nordic pamoja na mchango wa Serikali ya Tanzania.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika kazi za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zitaanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wafadhili mbalimbali wakiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Japan *Bank for International Cooperation*, ili kupata fedha za ujenzi wa barabara hiyo.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anajumuisha yaani wakati wa hotuba yake vilevile alitoa maelezo ambayo nadhani hayaachani sana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Swali langu la nyongeza ni kwamba inaonekana mpaka sasa bado utaratibu wa kutafuta fedha unaendelea lakini niombe sasa kuuliza kuhusu suala la kutengeneza kwa kiwango cha changarawe. Mpaka sasa Barabara ile hasa kutoka Kondoa mpaka Dodoma – Iringa haijatengenezwa vizuri kwa kiwango cha changarawe. Ni lini Serikali itaanza utengenezaji wa kiwango cha changarawe kwa Barabara ile?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam S. Mfaki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba fedha ambazo zinawekwa kwa ajili ya ukarabati mdogomdogo siyo kiasi kikubwa sana na kwa kweli tulitegemea kwamba kazi hizi baada ya kumalizika tutaweza kupata mfadhili na kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza muda si mrefu.

Kwa hivi sasa Serikali inachofanya ni kuweka fedha ambazo zinaendelea kufanya Barabara hii iweze kupitika na tukitegemea kwamba tutakamilisha haya maandalizi na

vilevile tutaweza kupata fedha za ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha lami kwa haraka iwezekanavyo.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, maana yake leo Wabunge Wanawake ndiyo wanaouliza maswali toka mwanzo mpaka sasa.

Na. 391

**Ubovu wa Barabara ya Kwenda Isaka**

**MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, magari yote yanayotoka Dar es Salaam kwenda Isaka (*Dry Port*) yakifika Nzega hayaendi Tinde/Isaka yanapitia Nzega – itobo – Mwangoye – Ilagaja – Isaka, na kwa kuwa, sehemu ya mto Sipiyu ni korofi sana hali hiyo inayoifanya kuwa, sehemu ya mto Sipiyu ni korofi sana. *(Makofi)*

Je, Serikali ina mpangogani wa kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe ili ipitikie kipindi chote hasa masika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mbunge wa Bekene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nzega – Itobo – Mwangoye – Ilagaja – Isaka imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya barabara kutoka Nzega hadi Itobo yenye urefu wa kilometa 20 ni ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Tabora. Aidha, sehemu ya barabara kutoka Itobo – Mwangoye – Ilagaja hadi Isaka yenye urefu wa jumla ya Kilometa 43, pamoja na sehemu ya mto Sipiyu iko chini ya Halmashauri ya Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya barabara iliyopo chini ya Wizara yangu inahudumiwa inavyopaswa na kuifanyia matengenezo pamoja na kuweka changarawe kila mwaka na inapitika vizuri wakati wote.

Aidha, naishauri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutenga fedha kadri Bajeti itakavyoruhusu ili kukarabati sehemu korofi kati ya Itobo na Isaka ili barabara yote iweze kupitika kwa wakati wote.

**MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa *council* zetu tunajua kwamba zina fedha kidogo na kwa kuwa sehemu hii ambayo nimeitaja kutoka Itobo kwenda Mwangoye kutelemka mpaka Isaka ndiyo sehemu yenye mpunga mwingi sana ambao unasafirishwa Isaka *Dry Port* kwenda Burundi na mwingine kuja Mwanza na mwingine kuletwa Dar es Salaam na Tabora.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka kuisaidia *council* angalau kutengeneza ile sehemu korofi kama nilivyosema ya Mto Sipiyu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyofuatilia masuala ya Barabara kwenye Jimbo lake.

Lakini kuhusu suala la Serikali kuisadia Halmashauri ni kweli kwamba Serikali imeona umuhimu wa kusaidia Halmashauri zetu na ndiyo maana fedha za Barabara kwa ajili ya Halmashauri zimeongezwa kwa ujumla wake kutoka bilioni 25 mwaka jana mpaka bilioni 65 mwaka huu na nina hakika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega vilevile imeongezewa.

Kwa umuhimu wa Barabara hiyo kama alivyoelezea nina hakika ataweza kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Nzega iweze kurekebisha maeneo hayo korofi.

**NAIBU SPIKA:** Kufuatana na muda tunaendelea na swali la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.nalo linaulizwa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, lakini atauliza Mheshimiwa Lucy F. Owenya, kwa niaba yake.

Na. 392

**Malimbiko ya Hoja za Fedha**

**MHE. LUCY F. OWENYE (K.n.y. MHE. DR. WILBROD P. SLAA)** aluliza:-

Kwa kuwa, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2006 imeonyesha kuwa kuna malimbikizo ya hoja za thamani ya shilingi 12,890,826,865/= na $.2,021,525.20:-

(a) Je, Serikali inaweza kuliarifu Bunge kuwa, fedha hizo zilikusudiwa kwa malengo gani kwa mchanganuo na kwa nini majibu sahihi ya hoja hizo hayakuweza kupatikana kwa muda wote huo na sasa Serikali inatoa kauli gani kuhusu fedha nyingi za wananchi kutopata maelezo sahihi?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo hasa ikitiliwa maanani kwamba, askari wa ngazi za chini wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu ya mishahara duni, kutokuwa na makazi bora na kutokuwa na vifaa bora vya kufanyia kazi?

(c) Je, Serikali iko tayari kuwachukulia hatua wale wote ambao kwa uzembe kwa makusudi walishindwa kutunza fedha za umma?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Hoja anazozungumzia Mheshimiwa Mbunge kwa kiasi kikubwa zimetokana na pesa zinazotolewa na Mashirika ya Misaada ya Kimataifa yaani *UNHCR, DANIDA, WFP* moja kwa moja kwenda kwenye miradi iliyolengwa (*direct project funding*) na hazipitii Wizarani kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika hayo ya Kimataifa hutoa huduma kwa wakimbizi au maeneo yanayohifadhi wakimbizi kwa njia ya Vifaa, chakula na huduma za kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakaguzi walihoji kwa nini Wizara haikuingiza thamani ya huduma na vifaa hivyo kwenye Vitabu vya Serikali katika miaka husika. Thamaniya vifaa na huduma zilizohojiwa ni jumla ya Shilingi 12,890,826,865.00 na USD 2,021,525.20.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu haikuweza kuingiza vifaa na huduma kwenye vitabu kutokana na huduma na vifaa hivyo kutolewa kwa ajili ya wakimbizi na siyo kwa ajili ya Watanzania. Kwa sasa, suala hili linashughulikiwa na Wizara yangu

kwa kushirikiana na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (Hazina) pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuuu wa Hesabu za Serikali baada ya kupata Kamati ya Bungeya Hesabu za Serikali wakati wa kujadili Hesabu za Wizara zilizoisha tarehe 30 Juni, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kiasi cha Shilingi 155,930,000/= ni maduhuli ambayo hayakukusanywa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Hii ilitokana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutokuwa na nguvu za Kisheria baada ya Sheria Na. 3 ya mwaka 1985 iliyonda Jeshi hilo kufutwa kwa mujibu wa Kifungu cha 35 (b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002. Aidha, Wizara yangu imepeleka mapendekezo Hazina ili kuangalia utaratibu wa kufutwa malimbikizo ya maduhuli ya muda mrefu.

Ni matumaini yangu kuwa baada ya Jeshi hili sasa kutambulika Kisheria maduhuli yataendelea kukusanywa ipasavyo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimeelekeza katika sehemu (a) ya jibu langu, asilimia kubwa ya hoja hizi ni fedha, huduma na vifaa kutoka kwa Wafadhili vinavyopelekwa moja kwa moja kwa ajili ya wakimbizi na maeneo yaliyoathiriwa na uwepo wa wakimbizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uduni wa maslahi na maisha ya Askari kwa ujumla wa Serikali inatambua haja ya kuboresha hali ya watumisi wake wakiwemo Askari.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali siku zote huwachukulia hatua wale wote wanaozembea kazi zao pale inapodhihirika hivyo kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za ajira zao.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina swali dogo la nyongeza.

Pamoja na yeye kusema kwamba fedha hizi ni za kigeni na hazipitii kwenye vitabu vyao lakini sioni ni kwa nini wasiweze kutunza mahesabu ya fedha hizi. Ninapenda kujua kwamba Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba ubadhilifu huu hautokei tena ili ziweze kutumika kwa Askari wale wa ngazi za chini kuboresha maisha yao kama makazi na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy F. Owenya kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi suala hili ambalo lipo mbele yetu si ubadhilifu wa fedha lakini ni kwamba pesa zilikuwa zimeletwa na mashirika ya nje na zimepelekwa moja kwa moja kwa wakimbizi na maeneo ambayo yameathirika na uwepo wa wakimbizi.

Suala la kuboresha maslahi ya maisha ya Askari ni suala tofauti na Serikali imekiri kwamba inatambua kuna haja ya kuboresha hali ya watumishi hao na Serikali inalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Parmukh S. Hoogan.

Na. 393

**Kutokomeza kwa Ugonjwa wa Ndui Nchini**

**MHE. PARMUKH S. HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, karne iliyopita Shirika la Afya Duniani (*WHO*) likishirikana na mataifa yote ulimwenguni lilifanikiwa sana kupambana na kutokomeza kabisa ugonjwa hatari wa Ndui; na kwa kuwa, ugonjwa huo haupo tena hivi sasa:-

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge ni hatua gani zilichukuliwa hadi kutokomeza ugonjwa huo ulimwenguni?

(b) Je, ni magonjwa gani yanaweza kutokomezwa kabisa ikiwa hatua kama hizo zitachukuliwa na ni hatua gani zimeshafanikiwa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika karne iliyopita Shirika la Afya Dunia *(WHO)* kwa kushirikiana na mataifa mbalimbali duniani ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanikiwa kupambana na hatimaye kutokomeza kabisa ugonjwa wa hatari wa ndui.

Hatua zilizochukuliwa kupambana na hatimaye kuutokomeza kabisa ugonjwa huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa elimu ya afya kwa umma kuhusu ugonjwa huo; chanzo chake, dalili zake, jinsi unavyoenea na jinsi ya kujikinga.

(ii) Kuendesha kampeni maalum ya chanjo ya ugonjwa huo kwa umma.

(iii) Kuhakikisha kuwa wagonjwa wote wanapatiwa tiba sahihi.

(iv)Kuimarisha ufuatiliaji na kuhakikisha kwamba wale ambao hawakufika kwenye vituo vya kutolea huduma wanafuatwa majumbani kwao ili kupatiwa chanjo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi magonjwa yote yanayopunguzwa makali au kuzuiwa kwa chanjo yanaweza kutokomezwa endapo hatua madhubuti zitachukuliwa. Kufanikiwa kwa mikakati hiyo kutachangiwa kwa kiasi kikubwa iwapo wananchi watapata uelewa wa kutosha wa ugonjwa wenyewe na kujiona wao ni sehemu ya mafanikio na hivyo kushiriki kikamilifu katika mpambano mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ugonjwa mwingine unaoweza kutokomezwa kabisa iwapo hatua tajwa hapo awali zitachukuliwa ni ugonjwa wa kupooza yaani *polio,* hivi sasa ni nchi chache zinazosumbuliwa sana na ugonjwa huo zikiwemo Nigeria, Angola, Zambia, Corte D'Voire kwa upande wa Afrika lakini vilevile Pakistan na India.

Taarifa zetu hapa nchini za ufuatiliaji wa magonjwa zinaonesha kuwa tangu mwaka 1995 mpaka sasa hakuna vimelea vya ugonjwa vilivyopatikana kwenye sampuli zote zilizochunguzwa kutoka kwa wagonjwa waliohisiwa. Mgonjwa wa mwisho hapa nchini alipatikana mwaka 1996.

Hata hivyo, kutokana na uvukaji mwingi wa watu katika mipaka ya nchi yetu yaani *cross border movements,* ufuatiliaji (*surveillance*) utaendelea hadi hapo shirika la Afya Dunia litakaporipoti kuwa nchi zote jirani zimetokomeza ugonjwa huo.

**MHE. PARMUKH S. HOOGAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, surua nayo ni maradhi hatari na imeshaua watoto wengi nchini kwetu.

Je, Serikali haiwezi kuchukua hatua kama hiyo kwa maradhi hayo ili kuweza kuyatokomeza kama ilivyokuwa kwa ndui.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Majibu tafadhali maana wewe ni daktari kwa hiyo yote unayaweza tu. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA AFYA NAUSTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimjibu Mheshimiwa Parmukh S. Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni mjini Mgharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli surua inaua watoto wengi hapa nchini lakini ukifuatilia takwimu zetu idadi ya watoto wanaopata surua inapungua mwaka hadi mwaka na ni mwaka jana tu tulipopata surua katika Jiji la Dar es Salaam ambayo tuliidhibiti kikamilifu katika muda wa miezi miwili.

Lakini nchini kote idadi ya watoto imepungua ni kwa sababu ya ushiriki wa wananchi na chanjo ambayo tunaiendesha.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali mwisho kwa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Juma S. Killimbah.

Na. 394.

**Riba inayotozwa na BOT**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MHE. LAZARO S. NYALANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* inatoza kiwango cha juu sana cha riba (*interest rates*) hali inayosababisha gharama za kukopa fedha kuwa kubwa kuliko nchi yoyote mwanachama wa *SADC* na Afrika Mashariki:-

(a) Je, nini chanzo cha utata huo?

(b) Je, *BOT* inalitazamaje tatizo hilo na athari zake kiuchumi?

(c) Je, kwa nini *BOT* inaruhusu matumizi ya Dola za Kimarekani katika Transaction za ndani ya nchi?

**MHE. NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa Benki Kuu ya Tanzania kwa sasa haitoi mikopo kwa Serikali wala mabenki ya biashara au watu binafsi na kwa hiyo haitozi riba ya mikopo. Shughuli za utoaji riba kwa kawaida hufanywa na taasisi za kifedha zinazotoa mikopo mathalani mabenki ya biashara na taasisi za *microfinance* ambazo zina wajibu wa kukopesha fedha kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yanayosababisha riba za mikopo kuwa juu sana hapa nchini ni pamoja na miundombinu hafifu ambayo huongeza gharama za

uendeshaji shughuli za kibenki, ardhi kutotumika kama dhamana ya mikopo, ucheleweshaji wa kesi za mabenki na wateja wake, utoaji wa *court injunctions,* wateja kuchelewa kupata hati miliki za arhi yaani *title deeds* na benki za biashara kutokuweza kuuza dhamana za mikopo kwa kipindi kifupi ili kurejeshewa fedha zao.

Vile vile kuna udhaifu katika kurejesha mikopo kwa baadhi ya wakopaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo sikubaliani na hoja ya Mheshimiwa Nyalandu kwamba gharama za kukopa fedha Tanzania ni kubwa kuliko nchi yoyote mwanachama wa *SADC* au Afrika ya Mashariki. Kati ya mwaka 2004 na 2007 riba kwenye mikopo iliyotolewa na Mabenki ya kibiashara Tanzania ilikuwa kati ya asillimia 14 na 15 wakati Zambia ni kati ya asilimia 28 hadi 30. Malawi asilimia 33 hadi 36. Hali kadhalika viwango vya riba katika nchi ya Botswana ilikuwa asilimia 15, Madascar asilimia 16.1 – 17, Msumbiji asilimia 17.3 na jirani zetu Kenya asilimia 16.5 mpaka 14.4. Viwango hivi vilishabihiana sana na viwango ambavyo vinatozwa hapa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikishirikiana na Benki Kuu itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kibiashara ili kuziwezesha Benki zetu kutoza riba nafuu. Hii itawezekana tu baada ya matatizo niliyoyataja hapo juu kupungua au kumalizika kabisa chini ya mpango wa maboresho wa sekta ya fedha unaoendelea hivi sasa yaani *Second Generation for Financial Sector Reform.*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 sehemu ya 3 yaani *Part III* kipengele cha 26 kinatamka wazi kwa shilingi ya Tanzania itakubalika na kutumika kama fedha halali kwa malipo yaani *Legal tender* ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Tafsiri ya kipengele hiki kisheria si kuwa kinakataza matumizi ya fedha za kigeni kama Dola za Kimarekani na nyinginezo katika malipo au kunukuu bei zinazohitajika kulipwa ndani ya nchi. Kimsingi kipengele hiki kinaaminisha kuwa shilingi ya Tanzania ndiyo fedha pekee ambayo haiwezi kukataliwa na mtu yoyote kwa malipo yoyote halali ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Serikali inatambua kuwa bado kuna wafanyabiashara nchini ambao kwa sababu mbalimbali wanaamini zaidi malipo ya fedha za kigeni kuliko shilingi yetu ya Tanzania ingawa hali hii kwa sasa imeanza kupungua.

Ndiyo maana Serikali kwa kuzingatia hali hii na kwa kutambua michango na maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala hili imeagiza Benki Kuu kulifanyia kazi na kutoa mapendekezo ambayo yatazingatia kulinda mafanikio yaliyokwishapatikana kwa kuondoa *exchange controls* na wakati huo huo kuimarisha malipo ya kutumia shilingi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Dolarisation* limeulizwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana katika kikao hiki. Kama alivyotamka Mheshimiwa Waziri Mkuu jana humu Bungeni Serikali itatoa tamko maalum kuhusu *dolarisation* humu Bungeni. Namshauri Mheshimiwa Mbunge Lazaro Nyalandu asubiri tamko la Serikali.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Benki Kuu ndiyo mhimili na ndio msimamizi mkuu wa Taasisi hizi za kifedha ambazo zinakopesha wananchi na zinakopesha wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza vitu mbalimbali hapa nchini. Na kwa kuwa Taasisi hizi za kifedha zimekuwa na riba kubwa sana na hadi kufikia juzi Mheshimiwa Rais akawa amesema zipunguze riba.

Sasa je, Benki Kuu kupitia Wizara wanasemaje kuhusiana na suala la hizi Taasisi ambazo bado zinaendelea kutoza riba kubwa na kufanya watu na hasa wawekezaji kushindwa kuwekeza?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye suala la msingi Serikali inatambua kwamba hata asilimia 14 mpaka 15 bado ziko juu.

Waziri wa Fedha alishazungumza na Benki Kuu na Mabenki yote 21 ambayo yako hapa nchini kuzungumzia suala la mikopo, suala la riba, Mabenki yana chombo chao kinaitwa *Tanzania Banker's Association* wameunda Kamati, Kamati hii inatazama suala zima la riba, suala zima la mikopo hadi vijijini na vile vile jinsi gani wananchi wengi wanaweza wakapata mikopo. Wakati wowote Benki Kuu itamletea Mheshimiwa Waziri wa Fedha ripoti ya mazungumzo yao. Ni matumaini ya Serikali kwamba katika muda mfupi riba zinaweza zikapungua na si kupungua riba tu kwamba hata wananchi wa vijijini wanaweza wakapata mikopo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge dakika 5 ni zile zilizotumika wakati wa kuwasilisha nyaraka. Kwa hiyo, muda umekwisha na maswali yamekwisha.

Waheshimiwa Wabunge ninawatambulisha wageni lakini utaratibu wetu ni ule kwamba wageni wanatakiwa watolewe taarifa siku kabla ya kikao hiki. Maana mkileta hapa mmeandika kwa mwandiko wenu wa aina mbalimbali mnaweza kumpa matatizo Spika. Kwa hiyo, nategemea kwamba unapeleka ofisini yanakuja katika *typewritten document*. Sasa wageni tulionao leo kwanza nina wageni lazima nianze na wageni wa Waziri anayetoa hotuba sasa.

Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Fedha ana wageni wafuatao. Kwanza kuna ndugu Gray Mgonja, Katibu Mkuu wa Hazina, kuna Bwana Ramadhani Khija, Naibu Katibu Mkuu Hazina, kuna Ndugu Andrew Nyumayo, Naibu Katibu Mkuu Hazina, kuna Bwana Daudi Balali, Gavana wa Benki Kuu, kuna Bwana Lilla Mkila, Naibu Gavana Benki Kuu, Bwana Harith Kitilya, Kamishna Mkuu wa *TRA,* kuna Bwana Ludovick Utuoh, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, kuna Bi Mwanaidi Mtanda, Mhasibu Mkuu wa Serikali, hongera mama kwa kuwa Mhasibu Mkuu.

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Andrew Chenge. Naye ni Mheshimiwa Brigadia Adam Mwakanjuki, Waziri wa

Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar akiwa na wanawe. Karibu sana Mheshimiwa Waziri. Tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Stephen Wassira naye ni Balozi Ali Mchumo, Mkurugenzi Mkuu wa *Commodity Fund Organisation* karibu. Yeye alishakuwa Mbunge zamani hapa na Waziri wa Viwanda. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Joel Bendera, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo nao ni kikundi cha Kwaya kutoka *St. Andrew Church Korogwe* wakiongozwa na Padri Singano. Naomba wasimame waliko huko, Kikundi cha Kwaya kiko wapi. Karibuni sana.

Halafu nina wageni wa Mheshimiwa Zungu wao ni viongozi wa CCM kutoka Mchikichini Ilala, naomba wote wasimame. Halafu nina mgeni wa Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Bibi Oliver Kimaro, mke wake. Karibu sana. Halafu nina mgeni wa Mheshimiwa James Lembeli, Bibi Hawa Lembeli, mke wake pia karibu sana mama.

Nina wageni wa Mheshimiwa William Shellukindo ambao ni Makamishna watatu na Sekretariet ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano. Naomba wote wasimame, wako wengi. Karibuni sana. Humu ndani mwetu bado tunategemea matokeo ya Tume hiyo mara nyingine tunagombana kwa sababu hatujapata taarifa hiyo.

Kuna wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Bodi ya *NMB* Ndugu Meshack Ngatunga, naomba asimame alipo. Karibu sana ameongozana na Bi. Shyrose Bhanji, Meneja Uhusiano wa Benki hiyo, naomba asimame. Halafu tuna wanafunzi wa Shule ya Sekondari Jamhuri Dodoma walipo na walimu wao wasimame. Halafu kuna wanafunzi 40 kutoka *ACT Vocation Training Centre Dodoma* na walimu wao. Karibuni sana.

Halafu tuna wanafunzi 24 kutoka Shule ya Sekondari Msalato Dodoma, naona ni kundi lingine karibu sana ni shule ya wasichana kazaneni kusoma kwa bidii. Halafu nina wageni wa Mheshimiwa Daniel Nswanzugwanko Naibu Waziri ambayo ni mke wake Bibi Midlaster na watoto wao. Yuko wapi? Karibu sana. *(Makofi)*

Halafu tunaendelea na maswali matangazo ya kazi. Mwenyekiti Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anawatangazia wajumbe wake kwamba leo tarehe 10 saa 5.00 asubuhi katika ukumbi Na. 231 kutakuwa na kikao.

Mheshimiwa Msindai, Mwenyekiti wa Kamati za Hesabu za Serikali za Mitaa anatangazia wajumbe wake kwamba leo tarehe 10 saa 5.00 asubuhi kutakuwa na kikao Na. 231 ghorofa ya 2. Nadhani wataungana na ile Kamati nyingine. Halafu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi anaomba wajumbe wake wakutane leo saa 8.00 mchana katika chumba 428. Halafu Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii anawatangazia wajumbe wake leo tena wao ni saa 4.30 asubuhi watakuwa na kikao chumba 219.

Kuna tangazo la Bunge kwamba kesho tarehe 11 Waheshimiwa Wabunge kutakuwa na ufunguzi wa Tawi la *NMB* na sherehe zitafanyika pale Uwanja wa *Nyerere Square* saa 5.00 asubuhi kesho Wabunge wote mnakaribishwa.

Katibu Mkuu wa *TAPAC* anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa kuna kikao cha wanachama wote wa *TAPAC* tarehe 10 katika Ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya kuahirisha Bunge saa 7.00 Mchana leo.

Lakini Mwenyekiti wa *TAPAC* pia anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho tarehe 11 kutakuwa na semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Semina hiyo ambayo inahusu UKIMWI na Haki za Binadamu itaanza saa 3.00 asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa na imeandaliwa na *TAPAC* kwa kushirikiana na *UNDP* na Tume ya Kudhibiti UKIMWI *TACAIDS.*

Halafu napenda kuwatangazia pia Mheshimiwa Shellukindo wale ndugu mafundi wa kulenga shabaha tunaomba tuwatangazie kwamba kesho kutwa tarehe 12 itafanyika JKT Makutupora, wanaopenda kushiriki wajiorodheshe hapa langoni tunapopokelea *Order paper* kabla ya saa 7.00 mchana wa leo. Wale wataalamu wa shabaha kesho kutwa lakini mjiandikishe leo.

Kesho tarehe 11 Agosti, 2007 Timu yetu ya *Bunge Sports Club* wanasafiri kwenda Mpwapwa kucheza michezo ya kirafiki na *Veterans* wa Mpwapwa katika michezo ya *netball* na *football* na kuondoka itakuwa saa 5.00 asubuhi. Halafu tarehe 12 Agosti, 2007 Bunge *Sports Club* watacheza na Ma-*veterans* wachezaji wa zamani wa *Taifa Star* wale waliocheza fainali za Kombe la Taifa Huru la Afrika mwaka 1980 Nigeria, hapa hapa.

Wakati natangaza kuhusu Balozi Ali Mchumo amefuatana na mke wake Mheshimiwa Fatma Said Ali Mbunge mwenzetu tunamfahamu sana. Karibuni sana na wageni wengine wote mnakaribishwa. Halafu kuna matangazo mengine Kamati ya Uongozi kwa maana ya Wenyeviti wote *Steering Committee* kutakuwa na kikao kesho saa 5.00 asubuhi kwenye ukumbi wa Spika. Halafu pia mnakumbuka kwenye *Order Paper* yetu tulikuwa tunaona matangazo ya uchaguzi wa wale watakaotuwakilisha kwenye Vyuo Vikuu cha Kilimo, Sokoine nafasi 1, Chuo Kikuu cha Dodoma nafasi 1, Chuo Kikuu cha Mzumbe nafasi 1, nafasi 1 ya Chuo Kikuu cha Mzumbe ni nafasi ya Mbunge mwanamke. Chuo Kikuu cha Sayansi na Afya Muhimbili nafasi 2 zinazozingatia jinsia, Chuo Kikuu cha Ardhi nafasi 2 zinazozingatia jinsia.

Sasa naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa tarehe 17 mara baada ya kipindi cha maswali utafanyika uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda kuwakilisha Bunge kwenye Baraza la Vyuo Vikuu. Waheshimiwa wanaopenda kugombea mojawapo ya nafasi za Baraza la Vyuo Vikuu waweze kujaza karatasi za uteuzi na maelezo ya mgombea na kuirudisha Ofisini kwa Katibu wa Bunge siku ya Jumatatu tarehe 13 Agosti kabla ya saa 7.00 mchana. Ukichelewa hapo haitapokelewa. Mahitaji ya Wabunge ni kama nilivyoeleza. Fomu za maombi hayo ziambatanishwe kwenye waraka nilioandaa na zitapatikana ofisini kwa Katibu wa Bunge kuanzia sasa.

Kwa hiyo, wale wanaotaka kugombea nafasi hizo wakachukue fomu kuanzia leo lakini zinarudishwa Jumatatu saa 7.00 mchana.

Waheshimiwa Wabunge tumekuwa na matangazo mengi naomba tuendelee. Tangazo lingine la *Order Paper* Waheshimiwa Wabunge mmegawiwa *Order paper* nyingine kwa ajili ya shughuli za leo. Jana jioni tulipokuwa tunaahirisha mimi nilitangaza kwamba siku 35 za Bajeti zinaisha leo na ndivyo ilivyo. Zinaisha leo kwa namna gani kwa hotuba ya Waziri wa Fedha na Muswada wa *Appropriation*.

Muswada wa *Appropriation* maana yake yote tuliyozungumza siku 35 leo tunayafungasha na ule Muswada wa *Appropriation.* Muswada ule wa *Appropriation* hatuujadili ni kwamba ni yale tuliyojadili na kuamua kila Wizara tumeamua sasa Waziri wa Fedha atautoa ule Muswada kama vile kufanya maunganisho. Kwa hiyo ule hatuujadili, kwa hiyo atasoma leo hotuba yake Waziri wa Fedha kama kawaida tutajadili kama kawaida halafu tutaupitia Muswada wa *Appropriation.* Kama muda utapatikana basi tunaingia shughuli nyingine basi.

Ule Muswada wa fedha kama utakuweko muda atasoma Muswada tutaendelea nao Jumatatu Muswada wa Fedha. Naomba marekebisho haya tuyazingatie jana pale kulikuwa na mkanganyiko *Order paper* iliyoletwa ilituchanganya kidogo.

Kwa hiyo, naomba tuzingatie hivyo. Waziri atasoma hotuba yake kama kawaida mwishoni baada ya kupitia Kamati ile ya Matumizi atasoma Muswada wa *Appropriation* hapo ndiyo tumemaliza siku 35 Muswada wa Fedha hauko katika zile siku 35. Kwa hiyo kama atakuwa na muda atausoma majadiliano tunaendelea nayo Jumatatu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2007/2008 Wizara ya Fedha

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi iliyowasilishwa hapa Bungeni leo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likae kama Kamati ili likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato, Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako pamoja kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Kamati za Bunge, kwa umakini wenu katika kuendesha majadiliano ya bajeti ya mwaka 2007/2008, tangu yalipoanza tarehe 18 Juni, 2007 hadi sasa. Aidha, ninashukuru sana kwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati zote za Kudumu za Bunge katika kuchambua mapendekezo ya bajeti za Wizara, Idara na Mikoa. Natoa shukrani za pekee kwa Kamati ya Fedha na Uchumi chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Abdalah Omari Kigoda, Mbunge wa Jimbo la Handeni kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyoyatoa kwa Wizara yangu. Napenda kuwahakikishia

Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali inathamini sana michango, na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yanayoonekana katika ukuaji wa uchumi, ongezeko la mapato ya Serikali, ongezeko la uwekezaji, udhibiti wa matumizi ya Serikali na kadhalika ni vielelezo vya matunda ya ushirikiano mzuri kati ya Serikali na Wabunge kupitia Kamati za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008 Wizara ya Fedha, pamoja na mambo mengine, itaendelea kuzingatia ushauri uliotolewa na Bunge wakati wa kujadili Bajeti Kuu ya Serikali katika maeneo yafuatayo:-

Kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo visivyo vya kodi;

Kuboresha mifuko ya dhamana kwa ajili ya kuwezesha wananchi kupata mikopo;

Kuharakisha upatikanaji wa mikopo ya nyumba na ya kukodi rasilimali;

Kupunguza mlolongo wa taratibu ndefu za kuondoa mizigo bandarini ili kukabiliana na uwezekano wa kupoteza biashara ya kikanda (*transit traffic*); na

Kuboresha huduma ya Pensheni kwa Wastaafu na wasimamizi wa Mirathi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara iliendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje kwa kutekeleza yafuatayo:-

Kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji ili kuwezesha sekta binafsi kukua;

Kuharakisha mageuzi katika sekta ya fedha, hususani sekta ndogo ya benki ili kupanua wigo wa mitaji na hivyo kuongeza wigo wa kodi;

Kuimarisha uhusiano na wahisani pamoja na mashirika ya fedha ya kimataifa ili kuendelea kupata misaada na mikopo yenye masharti nafuu; na

Kusimamia kwa karibu mageuzi makubwa yanayoendelea ndani ya Mamlaka ya Mapato *(TRA)* chini ya Mpango wake wa pili wa maboresho wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2006/2007, Wizara ililenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi bilioni 2,327.647 (trilioni 2). Makusanyo halisi ya kodi kutoka *TRA* mpaka mwisho wa mwaka wa fedha 2006/2007 yalifikia shilingi bilioni 2,529 (trilioni 2.5) ukilinganisha na malengo ya Shilingi bilioni 2,269.579 (trilioni 2.3). Hivyo makusanyo ya kodi toka *TRA* yalivuka malengo kwa asilimia 11.4.

Aidha, makusanyo yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2006/2007 yamefikia shilingi bilioni 28.137. Matokeo mazuri ya ukusanyaji wa mapato pamoja na mambo mengine, yalitokana na utekelezaji makini wa hatua za mapato zilizoidhinishwa na Bunge katika Bajeti ya Taifa ya 2006/07 na kuongezeka kwa wananchi wanaolipa kodi kwa hiari. Napenda nichukue nafasi hii kwanza kuwapongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ufanisi wao katika ukusanyaji mapato na kuwapongeza walipa kodi wote ambao wanatimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa hiari kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato imeendelea kuboresha taratibu za ukusanyaji wa mapato, ikiongozwa na Mpango Mkakati wa Pili (*Second Corporate Plan).* Malengo Makuu ya Mpango Mkakati huu, ambao utekelezaji wake ulianza mwaka 2003 na utakamilika Juni 2008, ni kujenga uwezo wa Mamlaka ili kukusanya mapato yote yanayostahili, na pia kuboresha huduma kwa walipakodi. Pamoja na kukua kwa uchumi, utekelezaji wa mpango huo umetoa mchango mkubwa katika ongezeko la ukusanyaji wa mapato. *TRA* imekuwa ikivuka malengo ya ukusanyaji mapato kwa wastani wa asilimia 5 tangu kuanza kutekeleza Mpango Mkakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu yaliyojitokeza katika kipindi hiki ni pamoja na haya yafuatayo:-

Ukusanyaji wa mapato umeongezeka kwa asilimia 123, kutoka shilingi trilioni 1.11 mwaka 2002/03 hadi shilingi trilioni 2.5 mwaka 2006/07. Katika mwezi wa Juni 2007, TRA ilikusanya shilingi bilioni 289, na hivyo kuvunja rekodi yake ya kukusanya shilingi bilioni 259 mwezi Machi, 2007.Katika mwaka 2006/07, Idara ya Walipakodi Wakubwa (*Large Taxpayers Department*) imepata Hati ya Ubora wa Huduma inayotolewa na Shirika la Viwango Ulimwenguni *(ISO Certification)* kwa kutambua ubora wa huduma zake. Idara nyingine za TRA ziko katika hatua tofauti kuelekea kupata hati kama hiyo.

Mamlaka imeongeza matumizi ya teknolojia, ikiwemo kupokea ritani na kadhia za walipakodi, kukadiria kodi, kupokea malipo, na kulipa marejesho ya kodi iliyolipwa zaidi kwa njia ya elektroniki (*e-filing and electronic payment systems).*

Taratibu za kiforodha zimerahisishwa kwa wafanyabiashara wenye viwango vinavyokubalika vya uwajibikaji *(tax compliance*) kwa lengo la kupunguza muda wa mizigo kukaa katika vituo vya forodha, hasa bandarini. Elimu kwa umma imeendelea kutolewa kwa njia mbalimbali, ikiwemo chapisho linalolenga kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wafanyabiasha wadogo.

Wizara yangu inategemea kukusanya jumla ya shilingi trilioni 3.319 katika mwaka 2007/2008 kati ya shilingi trilioni 3.517 ambazo zinatarajiwa kukusanywa na Serikali kwa ujumla. Kati ya kiasi hiki, *TRA* inatarajiwa kukusanya shilingi trilioni 3.237. Ili kukusanya kiasi hicho, *TRA* itaimarisha utendaji wake kwa kuchukua hatua zifuatazo.

Kupanua wigo wa kodi kwa kuongeza idadi ya walipa kodi kwa angalau asilimia 30 katika kipindi cha mwaka huu wa fedha kwa kushirikisha taasisi ya *BRELA* na Serikali za Mitaa katika zoezi la kuandikisha walipa kodi wapya.

Kuimarisha usimamizi wa kodi, ikiwa ni pamoja na kuongeza kwa angalau asilimia 10 uchunguzi na ukaguzi wa kodi. Hii ni pamoja na kuongeza kasi katika ukaguzi kwa makampuni ya uchimbaji madini; makampuni ya mafuta ya petroli, sekta ya utalii na ujenzi; kuimarishaji doria sehemu za mipakani na majini; kuongeza matumizi ya teknolojia ya mtandao wa mawasiliano (*Wide Area Network);* kuimarisha taaluma ya watumishi kuhusu maeneo mapya ya "*lease and morgage financing"* na kuanzisha Kamati za Ushauri za Kodi (*District Tax Advisory Commitees*) katika Wilaya zote nchini.

Kukamilisha maandalizi ya Mpango Mkakati (*Corporate Plan)* wa Tatu utakaojumuisha kipindi cha 2008/2009 hadi 2012/13. Wizara itasimamia ipasavyo zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa misaada na mikopo toka nje Wizara ilipanga kupata shilingi bilioni 804.554 za misaada na mikopo nafuu ya kibajeti kwa mwaka 2006/2007, kutoka kwa nchi wahisani na mashirika mbalimbali ya fedha ya kimataifa. Hadi tarehe 30 Juni 2007, jumla ya shilingi bilioni 745.685 zilipatikana ambayo ni asilimia 93 ya lengo. Kiasi hiki kimefikiwa kutokana na wahisani wengi kutoa sehemu kubwa ya misaada ya bajeti katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha kulingana na makubaliano baina yao na Serikali chini ya utaratibu wa *"General Budget Support*". Jitihada zitaendelezwa kuwashawishi wahisani na mashirika ya fedha ya kimataifa kutoa misaada yao katika maeneo yanayochochea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mara ya kwanza ilifanya Mkutano na Wenyeviti na Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umma ili kukumbushana kuhusu dhana ya uendeshaji na uwajibikaji katika Mashirika na Taasisi za Serikali. Hatua hii imetokana na kumomonyoka kwa maadili, utawala bora na uwajibikaji katika baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha usimamizi wa Asasi hizi za umma, ofisi ya Msajili wa Hazina ipo katika hatua za kuajiri wataalam watakoandaa utaratibu utakaowezesha kuingiza kumbukumbu zote za Mashirika na Taasisi za Serikali katika Kompyuta (*data base)* ili kurahisisha usimamizi wa utendaji wa asasi hizi hasa usimamizi na uidhinishaji wa mishahara ya Taasisi, makato ya kisheria n.k. Kazi hii itafanywa kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Utumishi na Idara ya Bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu imeendelea kutekeleza sheria mpya ya Benki Kuu ya mwaka 2006, pamoja na ile ya Benki na asasi za Fedha *(Banking and Financial Institutions Act)* ya mwaka 2006. Muundo wa Uongozi wa Benki Kuu umekamilika baada ya Mheshimiwa Rais kuwateua Profesa. Beno Ndullu, Bwana Juma Reli na Bwana Lila Mkila kuwa Manaibu Gavana.

Vile vile, Serikali imeamua kuwa jukumu la usimamizi wa masuala ya kifedha katika Sekta ndogo ya Hifadhi ya Jamii litatekelezwa na Benki Kuu. Katika mwaka 2007/2008, Serikali itakamilisha Muswada wa Sheria wa kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi (*Regulator)* katika shughuli za hifadhi ya jamii hapa nchini. Lengo la Sheria hii ni kutoa miongozo na kuweka vigezo katika uamuzi wa uwekezaji katika nyanja mbalimbali zinazofanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kuboresha na kuimarisha shughuli za uwekezaji na kulinda maslahi ya wanachama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Benki Kuu ililenga kusimamia utekelezaji wa Sera ya Fedha (*Monitory Policy)* na kuweka uwiano wa ujazi wa fedha unaoendana na nia ya kudhibiti mfumuko wa bei kulingana na viwango katika nchi tunazofanya nazo biashara kubwa. Aidha, sera ya fedha ililenga kuhakikisha kunakuwa na mitaji ya kutosha katika sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu iliendelea kuimarisha usimamizi wa Sekta ndogo ya benki nchini kwa lengo la kulinda amana za wananchi. Kufikia Mei 2007, amana katika mabenki zilifikia Shilingi (trilioni 4,320.9) ikiwa ni ongezeko la asilimia 24.4 ukilinganisha na hali ilivyokuwa mwezi Mei, 2006. Mikopo kwa sekta binafsi nayo iliongezeka kwa asilimia 39.3 ikilinganishwa na lengo la asilimia 35 kwa mwaka ulioishia Juni, 2007. Uchambuzi uliofanywa na Benki Kuu unaonyesha kuwa ukopaji na uaminifu katika urejeshaji mikopo umeongezeka kutokana na kuimarika kwa mazingira ya biashara nchini. Aidha, kuanzishwa kwa Mifuko ya Dhamana za Mikopo (*Credit Guarantee Schemes)* kumechangia sana upatikanaji wa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wale wa kati. Vile vile makubaliano kati ya Benki za Biashara na mashirika ya kifedha kuanzisha mikopo ya jumla (*wholesale banking*) kwa *SACCOS* yamewezesha wanachama wengi zaidi kukopeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na wadau husika, itaendelea kutekeleza kwa kasi zaidi mabadiliko ya sekta ya fedha kwa lengo la kuwawezesha wajasiriamali wadogo, wa kati, na wakubwa kupata mikopo na mitaji kwa gharama nafuu; na pia kusogeza huduma za benki karibu zaidi na wananchi hususani wale wanaoishi vijijini. Aidha, Serikali itaendelea kuzifanyia marekebisho Benki ya Rasilimali Tanzania, Benki ya Posta na Twiga Bancorp Limited kwa lengo la kuziwezesha kutoa mchango unaotegemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza azma yake ya kuiimarisha Benki ya Rasilimali Tanzania kwa kuiongezea mtaji kwa awamu hadi itakapofikia Shilingi bilioni 50. Hadi sasa, Serikali imekwishaiongezea *TIB* mtaji wa Shilingi bilioni 12.7 na hivyo kufikia Shilingi bilioni 20.0.

*TIB* pia imeweza kupata mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 5.0 kutoka *Nordic/Southern African Development Community (NORSAD)* na mazungumzo yanaendelea kati yake na Mifuko ya Hifadhi za Jamii ya *PPF, NSSF,* na *PSPF* ili kupata mikopo itakayoiwezesha benki hiyo kutoa mikopo ya muda mrefu kwa sekta ya uzalishaji. *TIB* itaimarisha usimamizi wa mifuko maalum, ikiwa ni pamoja na Mfuko wa

Fedha za Kuhuisha Mikopo (*Refinancing)* na ule wa Utaratibu Maalum wa ukopeshaji kwa ajili ya uzalishaji wa maua (*structured financing*) yenye thamani ya Shilingi bilioni 42.0.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la *TIB* katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, ni kuongeza rasilimali zake kwa kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha vya ndani na nje. Aidha, mfumo wa uongozi utarekebishwa, ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa teknohama, ushirikiano na vyombo vya fedha vya kimataifa kwa lengo la kupata mikopo zaidi kwa miradi ya kimaendeleo ili kukuza uchumi. Lengo ni kuhakikisha mtaji unakua hadi Shilingi bilioni 73.7 ifikapo mwaka 2010 na mikopo kufikia Shilingi bilioni 155.3 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa shughuli za benki ya NMB ni wa kuridhisha. Mapato ya Benki hiyo iliyo na mtaji wa Shilingi bilioni 91.15 yameongezeka kutoka Shilingi bilioni 74.91 mwaka 2005 hadi Shilingi bilioni 100.75 mwaka 2006. Amana za wateja nazo ziliongezeka kutoka Shilingi bilioni 617.0 hadi Shilingi bilioni 688.0, wakati mikopo midogo midogo iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 81.87 hadi Shilingi bilioni 137.46. Aidha, jumla ya mikopo 12,163 ya uwezeshaji wananchi yenye thamani ya Shilingi bilioni 12.1 ilitolewa kwa wale waliotimiza masharti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, *NMB* imelenga kukusanya amana za wateja zenye thamani ya Shilingi bilioni 846.0, ili kuwezesha kutoa mikopo midogo midogo yenye thamani ya Shilingi bilioni 210.0 na mikopo ya Uwezeshaji ya Shilingi bilioni 17.0. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC),* itakamilisha mchakato wa kuwauzia wananchi hisa kupitia soko la Hisa la Dar es Salaam asilimia 21 kati ya asilimia 49 ya hisa za Benki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Juni 30 2007, Benki ya Posta ilikuwa na matawi 24 na Ofisi 115 katika Shirika la Posta Tanzania na hivyo kuifanya iwe ndiyo benki inayoongoza kwa kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi hasa vijijini kuliko zote hapa nchini. Huduma za Benki ya Posta zimeanza kuimarika na hivyo kuvutia wateja wengi zaidi. Amana za wateja zimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 58.179 mwaka 2005 hadi Shilingi bilioni 63.075 mwaka 2006, na hivyo kuiwezesha kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 22.876 kwa mwaka 2006 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 14.5 mwaka 2005. *TPB,* pia iliwekeza katika vitega uchumi mbalimbali vyenye thamani ya Shilingi bilioni 60.243 katika mwaka 2006, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 52.9076 mwaka 2005, wakati fedha za kigeni zilizotumwa nje na kupokelewa katika huduma ya *"Western Union"* ziliongezeka kutoka Shilingi bilioni 77.549 hadi Shilingi bilioni 94.041 katika kipindi hicho. Shughuli hizi katika mwaka 2006 ziliingizia *TPB* faida ya Shilingi milioni 964.0 ikilinganishwa na Shilingi milioni 609 iliyopatikana mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007, Benki ya Posta itaendelea kuboresha huduma kwa wateja wake ili kuhamasisha uwekaji wa amana hadi kufikia Shilingi bilioni 72.536; kuongeza mikopo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kwa wajasiriamali wadogo wadogo hadi kufikia Shilingi bilioni 29.739, na kupanua huduma ya kutuma na kupokea fedha kufikia wateja 250,000 kutoka 238,495. Aidha, benki

imelenga kuongeza vituo vya kuwahudumia wateja wake na kuimarisha matumizi ya mtandao wa Teknolojia ya Habari *(IT)* ili kupunguza msongamano ndani ya matawi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Twiga Bancorp Limited* imeendelea kutoa huduma kama Taasisi ya Fedha (*Licenced Financial Institution*) kwa kupokea na kutunza amana za wateja, na kutoa mikopo ya kibiashara kwa wateja wadogo wadogo, wa kati na wakubwa. Amana za wateja ziliongezeka kutoka Shilingi bilioni 22.983 mwaka 2005, hadi Shilingi bilioni 23.629 katika mwaka 2006. Mikopo nayo iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 8.937 hadi Shilingi bilioni 9.698 katika kipindi hicho. Hadi kufikia Desemba, 2006, Twiga Bancorp ilikuwa imewekeza jumla ya Shilingi bilioni 11.224 kwenye dhamana za Serikali na amana katika Benki nyingine ikilinganishwa na Shilingi bilioni 10.653 mwaka 2005. Shughuli hizi kwa ujumla ziliingiza faida kabla ya kodi ya Shilingi bilioni 1.472 katika mwaka 2006, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 1.182 mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007, Taasisi hii imedhamiria kuendelea kuimarisha shughuli zake kwa kujiunga na mpango wa kufanikisha malipo (*Tanzania Interbank Settlement System* (*TISS);* kutoa huduma za kuchukua fedha kwa Mashine *(ATM's);* na kufungua matawi zaidi. Aidha, kufuatia kuendelea kuimarika kwa mtaji wake, *Twiga Bancorp Limited,* inatarajia kuiomba Benki Kuu kuipatia leseni kamili ya benki. Jitihada hizi zinatarajiwa kuiingizia Taasisi hii amana za wateja kiasi cha Shilingi bilioni 32.04 ikiwa ni ongezeko la asilimia 38 kwa mwaka 2007; mikopo kwa wateja inatarajiwa kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 15.721 sawa na ongezeko la asilimia 62; na kuwekeza kiasi cha Shilingi bilioni 13.057. Juhudi hizi zinalenga kuipatia taasisi hii faida ya Shilingi bilioni 1.450 katika mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Bima imeendelea kukua ambapo idadi ya makampuni, madalali na wakala wa bima iliongezeka katika mwaka 2006. Pato kutokana na ada ya bima *(premium income)* limeongezeka kwa asilimia 15.3 kutoka shilingi bilioni 100.1 mwaka 2005 hadi Shilingi bilioni 115.4 mwaka 2006. Vitegauchumi vya bima navyo viliongezeka kwa asilimia 30.2 kutoka shilingi bilioni 95.6 mwaka 2005 hadi Shilingi bilioni 133.0 mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyotajwa, sekta ya bima imeendelea kukabiliwa na matatizo ya uelewa mdogo wa wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na bima za maisha, bima za afya, na bima za mali zao. Aidha, bado kuna ukosefu wa wataalamu wazalendo katika fani ya bima na "*risk management*". Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha *Connectcut* cha Marekani, inakamilisha maandalizi ya kuanzisha Chuo cha *"Risk Management*" katika majengo ya kilichokuwa Chuo cha Bima Mikocheni jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuendeleza huduma za bima nchini, changamoto kubwa ni kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu na faida za kujiwekea bima kama kinga ya afya zetu na mali zetu. Utafiti unaonyesha kuwa bado kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa umma kuanzia na viongozi wa Serikali; Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla kuhusu umuhimu wa bima kwa maendeleo ya kila

mtu na katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii. Changamoto hii siyo ya Serikali pekee bali ni yetu sote. Napenda kuchukua fursa hii kuwaomba Wabunge wenzangu kushirikiana na Serikali katika kuwahamasisha wananchi wa mijini na vijijini kujenga utamaduni wa kuwa na bima za maisha na mali zao, kama vile bima ya mazao, bima ya mifugo, bima ya nyumba, bima ya afya na kadhalika. Wizara inapitia upya Sheria ya Bima na Kanuni zake ili kuainisha maeneo yenye matatizo na kupendekeza marakebisho ili kuboresha zaidi shughuli za bima hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kulirekebisha Shirika la Bima la Taifa *(NIC)* bado unaendelea chini ya *PSRC*. Baada ya kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi wa kurejea uthamini wa majengo ya *NIC*, uthamini uliofanyika ulionyesha thamani ya majengo hayo ni shilingi milioni 41,155 badala ya shilingi milioni 26,631 zilizokuwa zimekadiriwa katika tathmini ya awali. Wazabuni walioshinda katika mchakato wa awali wamepatiwa uthamini huu mpya wakitakiwa kurekebisha maombi (*bids*) yao ya awali pamoja na kuainisha namna ya kuwashirikisha wafanyakazi, na wamekataa kuendelea katika mchakato huu. Hivi sasa serikali inatathmini hatua iliyofikiwa katika mchakato wa kubinafsisha *NIC* kabla ya kuamua mkakati mpya

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchakato huu, *NIC* imeendelea kutoa huduma za bima. Biashara iliyoendelea ni kuandikisha wateja wapya wa bima, na kuendelea kulipa madai ya bima halali zilizoiva. Hata hivyo, zoezi la kulipa madai ya zamani ya bima zilizoiva lilishindikana ama kutokana na baadhi ya wadai kuwa na vielelezo visivyotosheleza, au kuwa na vielelezo visivyokuwa halali. Hadi Desemba, 2006, makusanyo ya ada ya bima *(premiums)* yalifikia shilingi bilioni 17.7, mapato mengineyo Shilingi bilioni, 19.525 wakati malipo ya madai hadi Desemba, 2006, yalifikia shilingi bilioni 9.4, kati ya madai ya shilingi bilioni 26.7 yaliyothibitishwa. Katika mwaka 2007/08, Shirika la Bima litaendelea kufanya shughuli za bima na matarajio ya Shirika ni kupata jumla ya shilingi milioni 21,508, kutokana na shughuli za bima za kawaida shilingi milioni 12,068.0, shilingi milioni 9,440.0 bima za maisha na shilingi milioni 4,451 kutokana na mapato mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana *(CMSA)* yameendelea kusimamia na kuboresha mazingira ya kukuza soko la hisa nchini ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri kuhusu uwekezaji wa pamoja, na uuzaji wa hisa katika Soko. Katika mwaka 2006/07, Mamlaka ilisimamia uandikishaji na uuzwaji wa hisa za Kampuni ya Saruji Wazo (Twiga) na Kampuni ya *Jubilee Holding Limited* ya Kenya katika Soko la Hisa la Dar es Salaam *(DSE)*. Aidha, Serikali iliendelea kuorodhesha katika soko hatifungani za miaka 2, 5, 7 na 10 hadi kufikia thamani ya Shilingi bilioni 708.4. Benki ya Wananchi wa Dar es Salaam *(DCB)* iliruhusiwa kuongeza mtaji wake kwa kutoa hisa za upendeleo *(rights issue)* kwa wahisa wake badala ya kuziuza kwa ushindani katika soko huria ili Benki hiyo ijiandikishe rasmi katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Aidha, Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania *(UTT)* uliruhusiwa kuanzisha mpango wa pili unaoitwa "Wekeza Maisha" *(Invest Life Unit Trust Scheme).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha zaidi usimamizi wa masoko ya hisa nchini, Mamlaka imepitia upya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994 na sheria nyingine husika kwa lengo la kuondoa upungufu unaojitokeza, kurahisisha uratibu na usimamizi wa shughuli za mifuko ya dhamana, na kuzuia michezo ya upatu *(pyramid schemes).* Aidha, Soko la Hisa la Dar es Salaam limeanzisha mfumo wa ununuzi wa hisa kwa njia ya teknolojia ya Kompyuta *(Automated Trading System- ATS).* Mfumo huu unawawawezesha wafanyabiashara na madalali kufanya biashara zao wakiwa mahali popote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08, Mamlaka itaendelea kuboresha mfumo wa sheria ili huduma zitolewazo zifikie viwango vya Kimataifa. Mamlaka pia itaanzisha Soko la Wajasiriamali wadogo na Kampuni za Kati ili kuyawezesha makampuni hayo kupata mtaji wa masharti nafuu bila kuzingatia kuwa na uzoefu wa faida. Aidha, Mamlaka imeazimia kuorodhesha hisa za makampuni zaidi katika soko la hisa pamoja na kuongeza dhamana mpya sokoni zitakazouzwa kwa wananchi ndani na nje ya *DSE*. Mamlaka itaendelea kutoa elimu kwa umma na kuendelea kufanya tafiti za kuboresha zaidi sera ya ukuzaji wa masoko ya hisa na dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Hisa la Dar es Salaam *(DSE)* lililoanzishwa mwaka 1998, limeshaorodhesha kampuni 10. Kati ya hizo, tatu zinatoka Kenya na saba zinatoka Tanzania. Thamani ya Kampuni hizo inafikia shilingi bilioni 3,115.38 (trilioni 3.115). Aidha, Soko limeorodhesha hatifungani tano za makampuni na kumi na mbili za Serikali Kuu zikiwa na thamani ya shilingi bilioni 898.181. Katika mwaka 2007/08, Wizara inatarajia kuorodhesha kampuni za *NMB Bank Limited*, *CRDB Bank Ltd*., *DSM Community Bank, NICO Ltd.,* na *Tanzanite One*. Vilivile, *DSE* inatarajiwa kuendelea kuandikisha hatifungani za Serikali Kuu, Halmashauri/Manispaa na Makampuni, kuanzisha Soko la Kukuza Wajasiriamali pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu umuhimu wa Soko la Hisa na manufaa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania *(UTT)* tangu uanze kutoa huduma zake mwaka 2003, umekuwa na mafanikio makubwa kutokana na matokeo mazuri ya Mfuko wake wa kwanza wa Umoja (*Umoja Fund).* Thamani ya kipande imepanda kutoka shilingi 109.8 mwaka 2005 hadi Shilingi 119.2 Juni, 2007. Kutokana na mafanikio hayo, *UTT* kwa kushirikiana na Kampuni ya Bima ya *Alliance* imeanzisha mfuko mwingine wa Uwekezaji unaoitwa “Wekeza Maisha” *(Invest Life).*

Mwekezaji katika mfuko huu atanufaika kwa kupata faida za uwekezaji pamoja na Bima ya Maisha, ajali na gharama za mazishi, na ni uwekezaji kwa kipindi cha miaka 10. Mpango huu umeweka viwango mbalimbali vya kuchangia kulingana na uwezo wa walengwa. Kiwango cha chini ni shilingi 8,340 kwa mwezi kwa miaka 10 na kiwango cha juu ni shilingi milioni 1.0 kwa mkupuo mmoja. Aidha, Mfuko utaendelea kutoa elimu kwa umma na kutafiti kuhusu mifuko mingine ili kuwahamasisha wananchi kujijengea utamaduni wa kuwekeza akiba kwa manufaa ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ya Tanzania (*Gaming Board of Tanzania)* imeendelea kusimamia vizuri shughuli za michezo ya kubahatisha. Hadi Juni, 2007, Bodi iliweza kukusanya kodi ya jumla ya shilingi bilioni 2.59 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 1.46 kwa mwaka 2006. Katika mwaka 2007/08, Wizara imekwishawasilisha Bungeni kupitia muswada wa Sheria ya Fedha *(Finance Act 2007/08)* mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha *(The Gaming Act)* Sura Na. 41 ili kuziba mianya ya ukwepaji wa kodi. Marekebisho haya yanalenga kuihakikishia Bodi ukusanyaji wa mapato ya Shilingi bilioni 3.0 kama kodi ya michezo ya kubahatisha *(Gaming Tax).* Aidha, Bodi pia itaanzisha leseni mpya kwa uendeshaji wa biashara ya "*Slot machines"* inayoendeshwa mikoani au wilayani ambako hakuna "*Casino*" pamoja na kuhakikisha kuwa vifaa vyote vya michezo katika "*Casino* na *Slot machines*" vinapimwa na kukaguliwa kwa mujibu wa Sheria. Hatua hizi zinalenga kuipatia Bodi mapato ya ziada ya Shilingi bilioni 2.0 kwa mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu *(Anti Money Loundering)* ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo mwezi Novemba 2006, na imeanza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2007. Aidha, chini ya Sheria hii kimeanzishwa chombo cha Kiserikali cha uchunguzi kitakachopokea na kuzichambua taarifa mbalimbali kutoka Mabenki na Taasisi za Fedha ndani na nje ya nchi, zenye mwelekeo wa mashaka *(suspicious transactions)* kuhusiana na biashara ya fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya ugaidi *(terrorism financing),* na kuziwasilisha katika vyombo husika kwa hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2007/08, nilielezea kwa ufupi kuhusu Mpango wa "*Millennium Challenge Corporation (MCC)".* Ningependa sasa niitumie nafasi hii kutoa ufafanuzi kuhusu hatua tuliyofikia. Kati ya tarehe 23 – 26, Julai 2007, ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Katibu Mkuu wa Hazina, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi Zanzibar ulikuwa na mazungumzo na Shirika la *MCC* ambapo mambo mengi ya msingi yalijadiliwa kwa kina na muafaka wa awali kufikiwa kuhusu miradi mbalimbali yenye uwezekano wa kupata fedha kupitia shirika hili. Aidha, Bodi ya *MCC* inatazamiwa kukutana Septemba, 2007 kupitisha makubaliano yaliyofikiwa kati ya ujumbe wa Serikali ya Tanzania na *MCC.* Baada ya hapo, "*Compact*" hiyo itawasilishwa katika Bunge la Marekani, na tutakuwa na uhakika kuhusu fedha zitakazopatikana baada ya Bunge hilo kuridhia mapendekezo ya *MCC.* Serikali itapata fursa ya kulifahamisha Bunge lako Tukufu fedha zitakazopatikana kwa ajili ya kutekeleza miradi itakayokuwa imekubalika. Miradi iliyojadiliwa ni pamoja na:- Barabara ya Tunduma – Sumbawanga; Barabara ya Tunduru – Namtumbo; Barabara ya Tanga – Horohoro; Mradi wa kutengeneza barabara sita za Pemba; Mradi wa kiwanja cha ndege cha Mafia; Mradi wa kuongeza maji kwa Jiji la Dar es Salaam; Mradi wa kuimarisha upatikanaji wa maji mjini Morogoro; Mradi wa kuimarisha baadhi ya Taasisi zilizoundwa mahususi ili kusimamia vyanzo vya maji; Mradi wa kupeleka umeme Zanzibar *(Underground Cable)*; Mradi wa umeme wa nguvu ya maji wa Malagarasi *(Malagarasi Minihydro)*; na Mradi wa kuimarisha miundombinu ya umeme katika miji ya Mbeya, Iringa, Dodoma, Morogoro, Tanga na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuratibu kwa karibu utekelezaji wa Mpango huu, Serikali kwa kushirikiana na *MCC* inatarajia kuanzisha chombo cha usimamizi wa Mpango kitakachojulikana kama "*Millennium Challenge Account* Tanzania" (*MCA* - Tanzania). Chombo hiki kitakuwa chini ya Wizara ya Fedha na kitasimamia utekelezaji wa Mpango kwa muda wa miaka mitano, muda ambao utekelezaji wa miradi yote unatarajiwa kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuishukuru rasmi Serikali ya Marekani kwa kuijumuisha Tanzania kwenye Mpango huu. Baada ya taratibu za upatikanaji wa fedha zitakapokamilika baadaye mwaka huu, nitaomba Bunge lako Tukufu kupitisha fedha hizo kama mapato ya ziada kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ili ziweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara ya Fedha kwa kutumia vitengo vyake vya Ukaguzi wa Miradi *(Technical Audit Unit)* na Ufuatiliaji wa Matumizi *(Expenditure Tracking Unit)* ilifanya ukaguzi wa majaribio kwa miradi 197 inayotekelezwa na Serikali katika ngazi ya Halmashauri, Mikoa na ya Taifa, na kutoa maelekezo kwa watekelezaji jinsi ya kuboresha utekelezaji wa miradi hiyo. Lengo la ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti na Ukaguzi wa miradi ni kuhakikisha kuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge zinawafikia walengwa na zinatumika kwa kazi zilizoidhinishwa na viwango vya ubora uliokusudiwa. Ukaguzi uliofanyika umebaini kuwepo kwa matatizo mbalimbali ya kiutekelezaji ikiwa ni pamoja na: kutokamilika kwa baadhi ya miradi katika muda uliopangwa, kuongezeka kwa gharama, usimamizi hafifu, na kiwango duni cha ubora wa kazi iliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08, Awamu ya Kwanza ya Ukaguzi wa Miradi ambayo inatekelezwa kupitia mafungu ya Miundombinu, Maji, Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, na Ofisi ya Waziri Mkuu –Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Tanga Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Pwani na Dar es Salaam imeanza kukaguliwa kuanzia tarehe 23 Julai, 2007. Kazi hii imeanza mapema ili kufikia mwisho wa mwaka wa fedha tuweze kukagua maeneo yote ambayo tumepanga kuyakagua. Aidha, kazi ya uanzishaji kanzi data *(Data Bank)* ya miradi yote inaendelea Wizarani. Zoezi hili litatusaidia kufahamu kila wakati kila mradi unaotekelezwa umefikia wapi, na kiasi cha fedha kilichotumika katika mradi husika. Katika kuboresha utekelezaji wa zoezi hilo muhimu, Wizara ya Fedha itashirikiana na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Aidha, Wabunge katika maeneo yao yanapokaguliwa wanaombwa kutoa ushirikiano kwa Wakaguzi wa Miradi na ufuatialiaji wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, ili kuhakikisha fedha zinazotolewa zinafanya kazi iliyokusudiwa. Ni imani yangu kwamba utekelezaji wa zoezi hili utaleta nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali na hivyo kuleta maisha bora kwa Wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza zoezi hili kwa ufanisi, Wizara ya Fedha itaviimarisha vitengo hivi kwa kuvipa vitendea kazi vya kutosha kama magari, rasilimali watu; kuongeza rasilimali fedha na uimarishaji wa kanzi data *(Data Bank)* ya miradi yote na kuboresha miundombinu ya utoaji wa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2006/07, Wizara iliendelea kusimamia kikamilifu mwenendo wa madeni ya Serikali ya ndani na ya nje, kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, na Mkakati wa kusimamia Deni la Taifa. Jitihada hizi zimefanya deni letu lipungue kiasi, hususan baada ya Serikali kufutiwa madeni na wadai wetu. Katika mwaka 2007/08, Wizara itaimarisha uchambuzi wa misaada ili kuhakikisha kuwa fedha zinazotokana na mikopo zinawekezwa katika miradi yenye tija na ile iliyopewa kipaumbele kitaifa kama vile miundombinu, umeme, elimu na afya. Aidha, katika mwaka huu wa fedha, Wizara itaendelea kukopa kwa kutumia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada na inatarajia kuuboresha Mkakati wa Kusimamia Deni la Taifa ili uendane na mabadiliko yaliyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/07, Tume ya Pamoja ya Fedha iliwasilisha Serikalini Mapendekezo ya Vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Suala hili litajadiliwa katika kikao cha Kamati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi inayoshughulikia masuala ya Muungano. Tume pia imewasilisha Serikalini, Taarifa za Uchambuzi wa Takwimu za Madeni baina ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na ya Uchambuzi wa Wizara/Idara na Asasi za Muungano na Gharama zake kwa kipindi cha mwaka 1993/94 hadi 2003/04. Aidha, Tume imeendesha warsha kuhusu mahusiano ya kifedha kwa nchi zenye kuunda Muungano kwa Wadau wake zikiwemo Wizara za Fedha za pande zote mbili na kuwaelimisha wananchi kuhusu majukumu yake kupitia Vyombo vya Habari na Maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/08, Tume ya Pamoja ya Fedha imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:- kuandaa Mpango Mkakati *(Strategic Plan)* wa Tume; kufanya utafiti katika maeneo ya kuimarisha uhusiano wa kifedha na kibajeti kati ya SMT na SMZ, mapato ya Muungano na kuhusu misaada na mikopo baina ya SMT na SMZ; kuendelea kujaza nafasi za kazi zilizo wazi kwa mujibu wa Muundo wa Tume; na kuendelea kuelimisha wananchi na wadau wa masuala ya Muungano kuhusu majukumu ya Tume ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha Sura ya 140.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa kuna usimamizi wa kutosha na ufanisi katika matumizi ya Umma, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo yanayohusu matumizi ya mtandao wa Usimamizi wa Fedha za Umma. Watumishi walionufaika na mafunzo hayo ni kutoka Wizara na Idara zote za Serikali, Mikoa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mafunzo haya yamelenga kuongeza ujuzi katika matumizi ya mtandao *(IFMS)*. Katika mwaka 2007/08, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na TAMISEMI itakamilisha kazi ya kusambaza mtandao wa *IFMS* katika Halmashauri 37 zilizosalia. Kazi ya kuimarisha usalama wa mtandao wa *IFMS*, pamoja

na ile ya kuunganisha Hazina Ndogo na Makao Makuu ilioanza Julai, 2006, sasa imekamilika. Kazi inayoendelea ni kufanya majaribio ili kuhakikisha kuwa unafanya kazi kabla haujaanza kutumika. Kukamilika kwa kazi hii kutazifanya sasa Ofisi za Hazina Ndogo na Ofisi za *RAS* kuwasiliana na Makao Makuu ya Wizara ya Fedha moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Serikali na udhibiti wa fedha na rasilimali za Serikali, Serikali imeanzisha Kada ya Wakaguzi wa Ndani. Wakaguzi Wakuu wa Ndani 48 wameteuliwa kwa ajili ya Mafungu yote ya Wizara na Idara zinazojitegemea. Aidha, Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani wapatao 1,069 wamepewa mafunzo ya kuwaimarisha kiutendaji, kazi iliyobaki ni kukamilisha Ikama za Idara ya Ukaguzi wa Ndani katika Wizara, Idara na Mikoa, kazi hii itafanyika hatua kwa hatua. Mafunzo kwa Kada za Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani yataendelea kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)* ilikamilisha maandalizi ya mifumo na mikakati mbalimbali ya kuziwezesha taasisi za umma kufanya ununuzi kwa ufanisi na hivyo kuiwezesha serikali kupata vifaa na huduma bora. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kujenga uwezo wa watendaji wa Serikali Kuu na Serikali za mitaa wa kufanya ununuzi kwa tija na ufanisi. Katika mkakati huo mafunzo kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004, na Kanuni zake yalitolewa kwa watendaji wa vitengo vya ununuzi na wajumbe wa bodi za zabuni wapatao 1,050.

(ii) Kuanza utekelezaji kwa majaribio, mfumo wa kudhibiti na kukagua shughuli za ununuzi kwa taasisi za umma zikiwemo Serikali za Mitaa. Taasisi tano zilishiriki katika majaribio hayo zikiwemo *TANESCO*, *TANROADS*, Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo Hifadhi na Chakula na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mafunzo yaliendeshwa kwa wataalamu wa Ununuzi 348 na Wakaguzi wa Ndani wa Hesabu wapatao 174 kutoka taasisi za umma juu ya utaratibu huu ambao utaanza kutumika mwaka huu wa fedha. Chini ya utaratibu huu, taasisi zitakuwa zinawasilisha taarifa zao za ununuzi kwa Mamlaka na shughuli za ununuzi zitafanyiwa ukaguzi *(procurement audit)*.

(iii) Kukamilisha mfumo wa ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za ununuzi unaotumia TEKNOHAMA ambao kwa sasa upo katika majaribio na utaanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2007/2008.

(iv) Kuwaelimisha wazabuni kuhusu haki zao na taratibu za zabuni ikiwa ni pamoja na kuandaa miongozo ya kuwasaidia wazabuni kuandaa zabuni zenye kukidhi vigezo vinavyotumika katika kuitisha zabuni.

(v) Kukamilisha na kutoa nyaraka na miongozo mbalimbali ya kufanya shughuli za ununuzi na kuzisambaza kwa watendaji na pia kuziweka kwenye tovuti ya Mamlaka na;

(vi) Kuendesha mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge ili waelewe taratibu za ununuzi wa umma na majukumu ya Mamlaka kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Bodi ya Rufani za Kodi ilisikiliza na kutolea maamuzi rufani 58. Bodi vilevile ilitoa elimu juu ya sheria za kodi pamoja na utaratibu mzima wa kukata rufaa katika mikoa ya Mbeya, Iringa na Tanga. Elimu hii ni muhimu kwa walipakodi katika mfumo mzima wa utekelezaji wa dhana ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka 2007/2008, Bodi ya Rufani za Kodi itaendelea kupokea na kutoa maamuzi ya rufani za kodi mapema iwezekanavyo. Ili kuhakikisha chombo hiki kinafahamika zaidi, zoezi la kutoa elimu litaendelea katika mikoa na wilaya ambazo elimu hiyo bado haijatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Rufani za Kodi liliundwa kwa Sheria ya Rufaa za Kodi Sura Na. 408 ili kusikiliza rufaa zinazohusu maamuzi ya migogoro ya kodi inayotolewa na Bodi ya Rufani za Kodi. Kwa mwaka 2006/2007, Baraza lilipokea rufaa 67, kati ya hizo rufaa 54 zilisikilizwa na kutolewa maamuzi. Rufaa zilizosalia zinaendelea kusikilizwa na zitatolewa maamuzi mapema iwezekanavyo. Aidha, Baraza lilitoa elimu kwa wadau katika mikoa ya Mwanza, Morogoro na Kigoma kuhusu Sheria, Kanuni na taratibu za kukata rufani kwenye Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08, Baraza litaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kusikiliza na kutoa maamuzi ya migogoro ya kodi kwa haraka zaidi ili kuondoa kero kwa wadau pamoja na kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria, kanuni na taratibu za rufani za Kodi. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha vyombo hivi ili kuhakikisha haki inatendeka kwa wakati pale inapotokea migogoro ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa Fedha 2006/07, Wizara ilikamilisha uthamini wa mali za Serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 51.178 katika Wizara na Idara za Serikali 20. Jumla ya bohari 430 za Serikali zilihakikiwa, magari 136, mitambo 67 na pikipiki 7 zilifutwa na kuuzwa kwa njia ya mnada wa hadhara katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Lindi, ambapo jumla ya shilingi milioni 520.4 zilipatikana kutokana na zoezi hilo. Aidha, Serikali ililipa fidia na kifuta machozi vyenye thamani ya Shilingi milioni 119.7 kwa wadai mbalimbali 29 kwa amri za Mahakama. Serikali ilifidiwa jumla ya Shilingi milioni 18.9 kutoka kwa watu waliosababisha hasara kwa ajali na upotevu wa mali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa Fedha 2007/08, Wizara itahakiki bohari za Serikali 500 na itakamilisha uingizaji kwenye mtandao daftari la mali za Serikali *(Assets Register)* lenye kuonyesha idadi na thamani yake. Wizara pia itaendelea na zoezi la uthamini wa mali za Serikali katika Wizara nane na Idara zinazojitegemea kumi na moja. Aidha, Wizara itaendelea na zoezi la ufutaji na uondoshaji wa vifaa chakavu yakiwemo magari, mitambo, madawa, na vifaa vingine katika Wizara na Idara za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/07, Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu *(NBAA)* kwa kushirikiana na wadau wengine iliendesha mafunzo kwa Wahasibu na Walimu wa Vyuo vya Uhasibu kuhusu mabadiliko ya taratibu za kuandika na kukagua hesabu za mashirika na makampuni kwa kuzingatia miongozo ya kimataifa. Aidha, *NBAA* imeanzisha mchakato wa kuunda vyombo viwili vya kitaaluma ambavyo vitakuwa na majukumu tofauti. Chombo kimoja kitakuwa na majukumu ya kuhudumia na kusimamia wanachama wa *NBAA* ambao ni wahasibu na wakaguzi wa ndani.

Katika nchi nyingine majukumu ya aina hiyo hufanywa na chombo kinachojulikana kama Taasisi ya Wahasibu *(Institute of Certified Public Accountants).* Chombo kingine kitakuwa na majukumu ya kusimamia sera, miongozo na kanuni za uendeshaji wa shughuli zote za uhasibu na ukaguzi *(Accountancy Regulatory Board).* Mchakato huo utakapokamilika Muswada wa Sheria wa kubainisha utaratibu huo na vyombo husika utaandaliwa na kufikishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali *(National Audit Office -NAO)* ni chombo muhimu katika udhibiti wa matumizi ya Serikali. Katika mwaka 2006/2007, Ofisi hii iliweza kutekeleza mambo yafuatayo:- kukagua hesabu za Wizara 51, Mikoa 21, Halmashauri 124 na Ofisi 10 za Ubalozi wa Tanzania nje ya nchi.
Kwa mara ya pili mfululizo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeweza kutoa ripoti ya ukaguzi kwa wakati; kujenga uwezo wa kiutendaji wa ofisi kwa kutoa mafunzo kwa watumishi 105 wanaoendelea na mafunzo hapa nchini na kununua magari mapya 14 ili kuwawezesha watumishi kusafiri kwenda maeneo ya kazi; kuendesha mikutano ya wadau mbalimbali kujadili ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2004/05.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2007/2008 ni kutekeleza yafuatayo: - kukagua mafungu 51 ya Wizara na Idara za Serikali, hesabu 21 za mikoa ya Tanzania Bara, hesabu za Halmashauri za Miji na Wilaya 132 na Balozi zote 30. Katika kuimairisha shughuli za Ukaguzi, Ofisi inatarajia kufanya *'Surprise cash Audit'* angalau mara 4 kila mwaka katika ofisi zote inazozikagua. Kuimarisha ukaguzi wa ufanisi katika utendaji *(Performance Audit)* na thamani ya fedha ili kuchangia katika kuimarisha mfumo wa uwajibikaji ndani ya Serikali; kuanza kujenga uwezo kwa wafanyakazi katika kaguzi za kiuchunguzi *(Forensic Audit & Investigative Audit),* kufanya kaguzi kwa kutumia mifumo ya kompyuta na kuimarisha ukaguzi na utoaji wa taarifa kwa ujumla; kuendelea kulipia mafunzo ya watumishi walio katika vyuo mbalimbali na kukamilisha utekelezaji wa muundo mpya wa Ofisi ili kukidhi mabadiliko yaliyokusudiwa katika sheria mpya ya usimamizi wa fedha ya mwaka 2001; kuendelea kufanya matengenezo kwa vitendea kazi na kuongeza vipya ikiwa ni pamoja na magari mapya 4 yanatarajiwa kununuliwa. Ofisi inatarajia kuendelea na mchakato wa kupata ofisi zake, na itaendelea kujenga ofisi za mikoa ya Mbeya na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara iliajiri watumishi wapya wapatao 1,364 ikiwa ni Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani. Kati ya hao

164 wamebakizwa Wizarani na 1200 wamepelekwa katika Wizara zingine na Halmashauri mbali mbali. Aidha, jumla ya wafanyakazi 225 walipatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi kwa kufuata mpango wa mafunzo. Aidha, jumla ya wanafunzi 1,214 walidhaminiwa kupata mafunzo katika fani za Uhasibu, Teknolojia ya Habari *(IT)* na Ununuzi katika Vyuo vya *Tanzania Institute of Accountancy (TIA), Institute of Accountancy Arusha (IAA)* na Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM).* Wanafunzi 65 kati ya hao wanachukua Stashahada ya Uzamili na 1,149 Stashahada ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, vyuo vya *TIA*, *IFM* na *IAA* vilitoa wahitimu 5,552 katika fani za Uhasibu, Ugavi na Ununuzi, Wachambuzi wa Mifumo ya Kompyuta, na Watalaamu wa Benki na masuala ya Fedha. Wengi wao walidhaminiwa na Wizara yangu. Aidha, kwa mwaka 2007/2008, ili kukidhi mahitaji ya watalaamu katika sekta hii, Vyuo hivi vinatarajia kuongeza wanafunzi kutoka jumla ya wanafunzi 5,552 hadi 8,707 katika fani za Uhasibu, Ugavi na Ununuzi, Uchambuzi wa Mifumo ya Kompyuta, na masuala ya benki. Wachache kati ya Wanafunzi hao watasomea ngazi ya Cheti, wengi wao ngazi ya Stashahada ya Juu *(Advanced Diploma)* na wengine wachache Shahada ya Uzamili *(Masters Degree)* katika fani hizo.

Katika jitihada za kupunguza kero ya wafanyakazi kuhusu ucheleweshaji wa mishahara, Wizara yangu imeingia mkataba na *NMB* kuwalipa Watumishi wa Serikali mishahara yao kila tarehe 23 ya kila mwezi. Wizara pia imeingia mkataba na Kampuni ya *EMS* inayosafirisha vifurushi kwa ajili ya kusafirisha *"payroll*" kwa nchi nzima hadi Makao Makuu ya Hazina ndogo katika kila Mkoa ili "*payroll*" hizo kuwafikia wahusika mapema kwa ajili ya kufanya malipo mapema. Hundi pamoja na orodha ya walipwaji huwasili *NMB* kabla ya tarehe 20 ya kila mwezi. Makubaliano haya yameleta ufanisi wa malipo na kuondoa kero kwa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya pensheni kwa wastaafu na mirathi bado ni kero na changamoto kubwa kwa Wizara ya Fedha. Wizara yangu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wastaafu. Katika mwaka 2007/08, Wizara yangu itakamilisha mchakato wa kuwahamishia baadhi ya wastaafu wanaolipwa na Hazina kwenda kwenye Mifuko ya Pensheni ya *PPF, PSPF, GEPF, LAPF*, na *NSSF* ili waweze kupata huduma bora zinazotolewa na Mifuko hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006/2007, lengo la Wizara yangu lilikuwa kuwarejesha katika daftari wastaafu 3,849 waliokuwa wamelipwa malipo ya uzeeni kwa mkupuo. Hata hivyo, wastaafu 2,178 ndiyo walifanikiwa kurejeshwa. Wastaafu waliobaki 1,671 wengi wao hawana kumbukumbu za kuwezesha upatikanaji wa majalada yao na wengine wamegundulika kuwa hawastahili. Hadi kufikia mwezi Juni, 2007 jumla ya wastaafu 19,983 wamerejeshwa kwenye daftari la wastaafu tangu zoezi hili lilipoanza mwaka 2004. Lengo ni kuwarejesha wastaafu wanaokadiriwa kufikia 26,536 kwenye daftari la pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya mafao ya Wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki yalianza rasmi tarehe 22 Septemba, 2005. Hadi kufikia tarehe 30

Juni, 2007, Wizara yangu ilikuwa imewalipa wastaafu wapatao 36,455 jumla ya Shilingi bilioni 116.4. Kati ya hizo, shilingi bilioni 31.463 zimelipwa kama mirathi kupitia Mahakama mbalimbali nchini. Zoezi hili linafanywa kwa makini ili kuhakikisha haki inatendeka na malipo yanafanywa kwa wale wanaostahili. Kabla ya malipo, Wizara inafanya uchunguzi kubaini maombi yapi ni halali na yapi siyo halali ili wale wanaostahili walipwe na wale wadanganyifu wasilipwe na ikiwezekana wafikishwe kwenye vyombo vya sheria. Hadi sasa madai 182 yamebainika kuwa ni maombi yenye udanganyifu. Wizara bado inaendelea kupokea nyaraka za uthibitisho wa wadai ya malipo kutoka katika mashirika yaliyokuwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma *(PSPF)* katika mwaka 2006/2007, uliendelea kutekeleza majukumu yake ya kusajili wanachama, kuhifadhi kumbukumbu sahihi za wanachama, kukusanya michango na kuwekeza na kulipa mafao kwa wanachama waliostaafu na wengine wanaostahili kwa mujibu wa sheria. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2007, Mfuko ulikuwa umekusanya jumla ya Shilingi bilioni 118.43 ikiwa ni michango ya waajiri na wanachama wa Mfuko na shilingi bilioni 44.56 kutoka katika vitega uchumi mbalimbali. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya shilingi bilioni 67.27 zimetumika kulipa mafao. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, mfuko unatarajia kukusanya shilingi bilioni 147.65 ikiwa ni michango ya waajiri na wanachama, shilingi bilioni 54.40 kutoka katika vitega uchumi na kutumia kiasi cha shilingi bilioni 122.12 kulipa mafao kwa wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa *PSPF* ulianza kupokea michango kutoka kwa wanachama kuanzia tarehe 1 Julai, 1999. Hata hivyo, Mfuko unawajibika kulipa mafao ya wastaafu kwa kipindi chote cha ajira ya mstaafu kikiwemo kipindi ambacho mstaafu alipokuwa hachangii. Tathmini ya kitaalam *(actuarial valuation)* iliyofanyika imedhihirisha kuwa mafao ya utumishi wa nyuma kabla ya tarehe 1 Julai, 1999 yanakadiriwa kuwa shilingi billioni 933, na kwa sasa Serikali inatafakari hatua za kuchukua kuhusiana na upungufu huo.

Tatizo la kumbukumbu za watumishi wa Serikali wanapostaafu, japokuwa linaendelea kupungua, bado linaathiri shughuli za Mfuko. Mfuko utaendelea kukusanya na kuhakiki kumbukumbu za watumishi wakati wa zoezi la usajili linaloendelea pamoja na utoaji wa semina kwa wadau wote nchini kote. Sanjari na kuboresha kumbukumbu za watumishi, Mfuko umeanza kutoa mikopo ya nyumba kwa wanachama wake ambapo kwa sasa umeanza na wanachama ambao wamebakiza si zaidi ya miaka mitano kustaafu. Aidha, Mfuko unatarajia kuanza kujenga nyumba za bei nafuu kwa lengo la kuwakopesha wanachama wake hasa walimu walio vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha huduma za Mfuko wa *PSPF,* Mpango wa Pili wa miaka mitano (2007/08 – 2011/12) unaotoa mwongozo, mikakati na malengo ya utekelezaji wa majukumu ya Mfuko umeandaliwa, ambapo kipaumbele kimewekwa katika kuboresha huduma kwa wastaafu na wanachama wa mfuko kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/07, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini *(GEPF)* uliendelea kutekeleza majukumu ya kuboresha huduma kwa wanachama, kukusanya michango kutoka kwa wanachama, kuwekeza fedha za wanachama katika vitega uchumi vilivyo salama na kulipa mafao kwa wastaafu. Katika kipindi hicho Mfuko uliweza kuboresha huduma zake kwa wanachama na kuweza kulipa mafao kwa wanachama kwa muda usiozidi siku kumi na nne. Hadi kufikia mwezi Juni, 2007, jumla ya shilingi milioni 28,624.12 zilikusanywa kutoka kwenye michango ya wanachama, mapato ya vitegauchumi na vitegauchumi vilivyokomaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2007/08, Mfuko unategemea kukusanya jumla ya shilingi milioni 33,759.41 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ikijumuisha michango ya wanachama na kutoka kwenye vitegauchumi. Mapato yanayotokana na vitegauchumi yanatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 29.64 kutoka shilingi milioni 3,058.63 mwezi Juni, 2007 hadi shilingi milioni 3,965.26 mwezi Juni, 2008. Vilevile Mfuko unategemea kuwa na Tovuti yake ili kurahisisha mawasiliano na wanachama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma *(PPF)* ulikusanya shilingi bilioni 63.83 kama michango toka kwa wanachama katika mwaka 2006 ikiwa ni ongezeko la asilimia 21 ya kiasi cha shilingi bilioni 52.85 kilichokusanywa mwaka 2005. Mapato kutokana na uwekezaji yalikuwa shilingi bilioni 24.2 kwa mwaka 2006, kutokana na vitega uchumi vya muda maalumu, kodi ya pango, na hisa kutoka kampuni mbalimbali. Thamani ya mfuko imekua kwa asilimia 21.2 hadi kufikia shilingi bilioni 320 katika mwaka 2006 ikilinganishwa na thamani ya shilingi bilioni 264.45 mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2007, thamani ya Mfuko inategemewa kukua kutoka shilingi bilioni 320 ya mwaka 2006 hadi kufikia shilingi billioni 362 mwaka 2008, kutokana na kufikiwa kwa malengo ya kukusanya michango ya wanachama ya shilingi bilioni 60, na uwekezaji shilingi bilioni 31.0 ifikapo Desemba, 2007. Mfuko unategemea kulipa mafao ya jumla ya shilingi bilioni 22.8 ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Aidha, Mfuko unategemea kuandikisha wanachama wapya 20,000 kutoka Sekta Binafsi pamoja na kuanza ujenzi wa awamu ya pili ya nyumba za bei nafuu za Kiseke jijini Mwanza zipatazo 300 baada ya awamu ya kwanza ya nyumba 280 kukamilika mwezi Mei, 2006. Mfuko pia unatarajia kushiriki katika ujenzi wa mabweni kwa ajili ya Chuo Kikuu kipya cha Dodoma. Mradi huu unajumuisha jumla ya nyumba 1,140 ambazo zitauzwa kwa wananchi wa kawaida na huku kipaumbele kikielekezwa kwa wanachama wa Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu ambayo nimekwisha yaeleza na kufikia malengo yaliyokusudiwa katika Mwaka wa Fedha 2007/2008, Wizara yangu inaomba Bunge lako liidhinishe jumla ya shilingi 286,640,256,000 kwa Fungu 50, shilingi 609,147,867,000 kwa Fungu 22, shilingi 102,396,578,000 kwa Fungu 23 na shilingi 12,362,932,000 kwa Fungu 45 kama ifuatavyo:

Fungu 50: Wizara ya Fedha - (a) Matumizi ya Kawaida Shilingi 252,932,256,000. Kati ya fedha hizo Matumizi ya Kawaida ya Idara na Taasisi chini ya Wizara, shilingi 143,121,884,000; na Matumizi Maalumu, shilingi 109,810,372,000. (b) Miradi ya Maendeleo Shilingi 33,708,000,000. Kati ya hizo, Fedha za Ndani - shilingi 4,062,000,000, Fedha za Nje - shilingi 29,646,000,000.

Fungu 22: Deni la Taifa, shilingi 609,147,867,000. Fungu 23: Mhasibu Mkuu wa Serikali: (a) Matumizi ya Kawaida shilingi 96,234,578,000. (b) Miradi ya Maendeleo, shilingi 6,162,000,000: (i) Fedha za Ndani - shilingi 367,000,000 (ii) Fedha za Nje - shilingi milioni 5,795,000,000.

Fungu 45: - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi: (a) Matumizi ya Kawaida - shilingi 10,062,932,000; (b) Miradi ya Maendeleo - Shilingi 2,300,000,000: (i) Fedha za Nje - shilingi 2,300,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 7 Juni, 2007, Kamati yangu ilikutana na Waziri wa Fedha ambapo ilipata fursa ya kupitia, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Taarifa ya Shabaha na Malengo ya Wizara hiyo kama ilivyo kwenye Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2007/2008.

Kamati inachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Naibu Mawaziri wa Fedha, Makatibu Wakuu wa Wizara pamoja na Wakurugenzi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kwa kumpa pole nyingi sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa msiba mkubwa uliowapata wa kufiwa na baba yao mzazi. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha ni kiungo mhimili kutokana na majukumu yake ya kubuni na kusimamia Sera za Uchumi mpana, ukusanyaji wa mapato ya ndani na ya nje na kusimamia utaratibu, udhibiti wa mfumo wa taarifa za kihasibu Serikalini za mapato na matumizi. Aidha, Wizara ina jukumu la kusimamia Vitegauchumi vya Serikali katika Makampuni, Asasi, Taasisi na Mashirika ya Umma na

kusimamaia na kuhakiki mali za Serikali na udhibiti wa deni la Taifa. Kimsingi kazi kubwa ya Wizara ni kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za Mapato na Matumizi.Wizara imepata mafanikio katika ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya Serikali. Aidha, nchi yetu imeendelea kuwa na mahusiano mazuri na Wahisani pamoja na kusimamia vizuri matumizi ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2006/2007 mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ulikuwa wa kuridhisha, ambapo mambo yafuatayo yalitekelezwa:- Kusimamia na kuendeleza Uchumi katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Wizara imeweza kusimamia kwa mafanikio makubwa utekelezaji wa Mpango wa Matumizi wa Miaka Mitatu *(MTEF)* 2006/2007; Kuboresha Ukusanyaji wa Mapato; kupitia Kamati Maalum ya Mageuzi ya Mfumo wa Kodi *(Task Force on Tax Reform)*; kuratibu misaada ya kiufundi kupitia *TRA*; kuimarisha uhusiano endelevu kati ya Tanzania na Wahisani, kupitia Mkakati wa pamoja wa kusimamia misaada Tanzania (MPAMITA) *(Joint Assistance Strategy for Tanzania*); kuimarisha uhusiano wa Wahisani hivyo kuendelea kupata misaada na mikopo kwa wakati; kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kubuni mbinu za kusimamia vizuri zaidi bajeti ya Serikali kupitia:- Utoaji wa mafunzo kwa wafanyakazi pamoja na kuajiri watumishi wapya; na kujenga uwezo na ujuzi katika fani ya ununuzi wa mali za Umma, pamoja na utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliridhika na hatua zinazochukuliwa na Wizara za kuendelea kuboresha utendaji wa taratibu za usimamizi wa fedha kwa kufanya yafuatayo:-kuwasilisha kwa wakati unaotakiwa kisheria Taarifa za Hesabu za Mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Mapitio ya Matumizi *(Public Expenditure Review)* katika kutayarisha Mwongozo wa Bajeti ya Mwaka 2007/2008 na Matayarisho ya Taarifa ya Mwaka ya Misaada ya Kibajeti *(General Budget Support – GBS)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nyanja za Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma, Wizara iliendelea kutekeleza mambo yafuatayo:- kutathmini utendaji wa Mashirika/Taasisi za Umma ili kuimarisha utendaji kwa kutoa miongozo mbalimbali; kusimamia hisa za Serikali katika makampuni na mashirika ya umma na kuishauri Serikali kuhusu uwekezaji wa hisa ili kuhakikisha upatikanaji wa gawio kwa Serikali. Kati ya mashirika 147 ya kibiashara, Serikali inazo hisa asilimia 100. Hisa asilimia 50 zipo katika mashirika 11. Hisa chini ya asilimia 50 zipo katika mashirika 26. Katika kuleta ufanisi, mashirika 329 yamebinafsishwa na mali 638 zisizo za kibiashara *(Non-core Assets).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ukaguzi wa Miradi Kamati ilifahamishwa kuwa Wizara ilitumia vitengo vyake vya Ukaguzi wa Miradi *(Technical Audit Unit)* na ufuatiliaji wa Matumizi *(Expenditure Tracking)* kufanya ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Serikali ambapo kati ya miradi 197 ya kimkoa na ya kitaifa nchini ilikaguliwa. Katika ukaguzi huo ilibainika mambo yafuatayo:- Baadhi ya miradi kutokamilika katika muda uliopangwa; kuongezeka kwa gharama; usimamizi hafifu na

kiwango duni cha ubora wa kazi iliyofanyika. Hali hii ikiendelea ni ushahidi tosha wa kutopata thamani ya fedha za Serikali zinazotumika katika maeneo husika. Kamati yangu imebaini kuwa Wizara imeendelea kuboresha usimamizi wa Fedha kwa kufanya mambo yafuatayo:- kuanzishwa kwa mfumo wa malipo *(Integrated Financial Management System – IFMS)* kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali; kuendelea kutoa mafunzo ya uhasibu kwa Watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa; kutayarisha hesabu katika viwango vinavyokubalika kimataifa *(International Financial Reporting Standards - IFRS).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imebaini kuwa takriban asilimia 70 ya bajeti ya fedha za Kawaida *(Recurrent Budget)* na asilimia 100 ya bajeti ya Maendeleo *(Development Budget)* zinakwenda kwenye manunuzi. Hivyo, ni jukumu la Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa wanaboresha Ununuzi wa Umma kwa kuendelea kutoa mafunzo ya ununzi kwa watendaji wa Mashirika ya Umma, Taasisi na Asasi kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi ya Mwaka 2004. Aidha, Rufani za Zabuni zisikilizwe na kutolewa mamuzi mapema. Kuhusu majaribio ya utaratibu wa kudhibiti na kukagua shughuli za ununuzi wa taasisi za Umma ulioanzishwa katika taasisi tano zikiwemo *TANESCO,* Wakala wa Barabara Tanzania, Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii uendelezwe katika Taasisi zote za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2006/2007, Mapato ya Ndani na Nje, Kamati imeridhika na hali ya Mapato ambayo yameongezeka hadi kufikia shilingi 260 bilioni kwa mwezi. Hali hii inatia moyo hasa ikizingatiwa kuwa tumeweza kukabiliana na majanga mbalimbali yaliyoikumba Taifa yakiwemo ukame, uhaba wa chakula, uhaba wa umeme, bei kubwa ya mafuta duniani na ungonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa *(RVF).*

Kamati inaipongeza Wizara na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kwa kufanya kazi kwa bidii na kubuni mbinu mbalimbali kwa lengo la kupanua wigo wa mapato na kupunguza mianya ya ukwepaji kodi. Jitihada hizo zimeiwezesha Serikali kuvuka malengo katika makusanyo ya mapato yatokanayo na kodi na yale yasiyo ya kodi kwa asilimia 8.7 zaidi ya matarajio kwa kipindi hicho. Kuhusu fedha za nje ambazo ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Wahisani mbalimbali, Wizara ya Fedha imeendelea kuratibu na kuhamasisha. Hadi kufikia Machi, 2007, misaada na mikopo ilifikia shilingi bilioni 745.685 ambayo ni sawa na asilimia 93 ya matarajio ya mwaka mzima. Kamati inazipongeza nchi Wahisani kwa misaada yao. Hata hivyo, Serikali inatakiwa kufanya juhudi za makusudi ili kupunguza pengo la Bajeti ambayo ni tegemezi kwa asilimia 39. Mapato ya Serikali bado hayawiani na matumizi hali inayosababisha kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ili kuziba pengo la Bajeti. Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi ya kukusanya mapato yetu ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yatafanikiwa endapo Serikali itatilia mkazo utekelezaji wa mambo yafuatayo:- kuimarisha uchumi kwa kuweka mazingira bora ya uwekezaji na biashara ili kuwezesha sekta binafsi kukua na hivyo kupanua wigo wa kodi; kuimarisha mpango wa MKURABITA na mipango mingine ya kuongeza biashara zilizosajiliwa na ajira, ambako kutasaidia kusajiliwa walipa kodi wapya; kuendelea

kutekeleza Mpango wa Pili wa Maboresho *(Second Corporate Plan)* wa Mamlaka ya Mapato Tanzania unaolenga kuimarisha usimamizi wa kodi ili kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo: Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzingatia ushauri tulioutoa wakati wa kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Serikali iliyotolewa hapa Bungeni. Aidha, Kamati inaendelea kushauri Serikali kuimarisha utaratibu wa matumizi ya fedha hasa ikizingatiwa kuwa moja ya kigezo kinachoonyesha uhai wa Taifa ni kuwa na akiba kubwa ya *Foreign Reserves.* Ni vyema mkakati sahihi wa kupunguza matumizi fedha za bajeti *(Budgetary Expenditure Cards)* uzingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa takriban asilimia 70 ya bajeti ya Serikali imepelekwa kwenye Serikali za Mitaa kwa utaratibu wa *(D by D)* kwa kuhamishia baadhi ya majukumu pamoja na rasilimali fedha, rasilimali watu na vitendea kazi kutoka Wizara tano za Serikali Kuu kwenda kwenye Halmashauri. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imebainisha kuwepo kwa matatizo ya matumizi ya fedha katika Halmashauri hasa ikizingatiwa kuwa mpaka hivi sasa hakuna Kanuni *(Regulations)* madhubuti zinazosimamia matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa. Aidha, Wizara kwa kutumia vitengo vyake vya ukaguzi wa miradi *(Technical Audit Unit)* na ufuatiliaji wa matumizi *(Expenditure Tracking)* iendelee na ukaguzi wa miradi hususan inayotekelezwa na Halmashauri za Wilaya.

Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwekea mkazo eneo la udhibiti wa fedha za Serikali ili kupata thamani ya fedha inayotumika *(Value for Money).* Hivi sasa udhibiti umeegemea zaidi katika eneo la fedha *(Cash basis).* Aidha, usimamizi na udhibiti wa fedha za Umma uende sanjari na kuimarisha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kuongeza Wakaguzi pamoja na mafunzo. Kutokana na mabadiliko yanayotokea katika sekta ya Umma, majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi yamebadilika pia. Serikali iendelee kuimarisha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ili iweze kumudu majukumu yake mapya kwa kuipatia vitendea kazi vya kisasa na kuajiri wataalamu wa fani mbalimbali, na kuwapatia mafunzo yakiwemo ya *Computer based auditing na performance auditing.*

Jitihada za Serikali za kuendelea kudhibiti mfumko wa bei ziendelezwe. Kamati yangu bado inaamini kuwa mfumko wa bei ambao unasimamiwa na Wizara ya Fedha, mara zote unawaathiri zaidi wale walio na vipato vya chini na ndio walio wengi. Kwa vile kodi zimehuishwa katika sekta ya Mafuta na Utalii, Maliasili, ukusanyaji wa mapato kutoka maeneo haya ufanywe kwa umakini mkubwa ili tufanikiwe katika kuongeza mapato yetu ya nchi. Kamati yangu inaipongeza Serikali kupitia Mawaziri wa Fedha na Mipango kukubaliana na ushauri wa Kamati wa jinsi gani mchakato na utaratibu wa kurekebisha Shirika la Bima la Tanzania ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutafakari faida na hasara zinazopatikana kutokana na kuchelewesha urekebishaji wa Shirika hili, wadau wote tulikubaliana kuwa hasara ni kubwa kuliko faida kwa Taifa na kuendelea kuchelewa kubinafsisha shirika hili ipo hatari ya kuliingiza Shirika hili katika ufilisi. Kwa vile katika makubaliano hayo

tumezingatia maslahi ya watu wote hususan ya wafanyakazi kwa maana ya kuwalipa mafao yao, ni matumaini ya Kamati kuwa mchakato huo utafanywa kwa kasi mpya ili tulinusuru *NIC* na kuweza kuchangia kwa kiwango kikubwa uchumi wa Taifa letu. Katika nchi nyingine, Bima huchangia kiwango kikubwa katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imebaini kwamba wakati Bunge linaridhia sheria ya kuruhusu ushindani wa mashirika binafsi ya bima na sheria iliyoanzisha Shirika la Bima la Taifa *(NIC)* haikuweka kipengele katika Sheria hizo cha kuyataka mashirika ya umma kama vile Benki Kuu, *TANESCO, PPF, ATC* na kadhalika kuendelea kukata bima zao katika Shirika hili, katika kipindi cha mpito kama ilivyofanywa na nchi nyingine wakati wa utekelezaji wa zoezi kama hili. Hali hiyo ilichangia kudhoofisha uwezo wa Shirika hili la umma na wakati huo kusaidia kuimarisha kibiashara mashirika ya binafsi yaliyokuwa yanashindana na *NIC.* Kamati inaishauri Serikali kuyaagiza mashirika haya ambayo yanatumia fedha za Umma kufanya hivyo badala ya kukata bima kwa mashirika ya watu binafsi kwa lengo la kuimarisha hali ya kibiashara na tamani ya *NIC*.Kamati inapendekeza utaratibu utakaotumika kubinafsisha Shirika hili ufanane na ule wa *NMB* ambapo asilimia 59 ya hisa ziliuzwa kwa sekta binafsi na asilimia 41 kumilikiwa na Serikali kwa niaba ya wananchi na hatimaye ziuzwe kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu naomba nitoe maelezo mafupi kuhusu kikao cha Kamati yangu kilichofanyika tarehe 8/8/2007 kuhusu mchakato wa ubinafsishaji wa *NIC*.

Jana tarehe 09/08/2007 Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mbunge ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati yangu, alizungumzia katika mchango wake, masuala na muafaka uliofikiwa katika Kikao cha pamoja cha Kamati yangu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, *PSRC, NIC* na Jumuiya za Wafanyakazi ambapo ni kinyume na Kanuni za Bunge 88(7), Toleo la 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imekuwa ikijadili suala la Ubinafsishaji wa *NIC* kwa muda mrefu, na ikafikia hatua ya kuitisha kikao hiki ili kukubaliana kwa pamoja, hatua za utekelezaji wa siku za mbele *(The Way Forward).* Tulizingatia mambo mengi pamoja na mchango wa Sekta ya Bima kwa pato la Taifa, bima za wanyonge (Wafanyakazi, Polisi, Walimu, Wauguzi, na kadhalika), thamani ya mali za *NIC*, na ukomo wa muda wa kufanya kazi wa *PSRC* ambao ni Disemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisahihishe kwamba muafaka uliofikiwa ni wa kuzingatia ushauri wa Kamati yetu kwa Serikali na Wadau wengine kwa kuzingatia mabadiliiko ya Kiuchumi, kama vile tathmini za mali na majengo, na pia hali halisi ya kuboreka kwa hali ya kifedha ya Shirika hili kwa hivi sasa. Kamati imetoa mapendekezo ya kutekelezwa na Wadau wote ili kuharakisha na kufanikisha zoezi la ubinafsishaji wa *NIC.* Wahusika wanakwenda kuyafanyia kazi na watarejea kwetu na maendeleo ya kazi hiyo *(progress report).* Hivyo basi, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mjumbe wa Kamati yangu, amezungumzia mapema na bila makubaliano mambo ambayo yatawasilishwa

Bungeni kwa taarifa rasmi ya Kamati ya Fedha na Uchumi baada ya kufanyiwa kazi. Ni vyema ikazingatiwa kuwa maelezo aliyoyatoa mjumbe si kutokana na kazi iliyotokana na kazi ya Upinzani, bali ni kutokana na kazi iliyofanywa na Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyozungumzia msemaji wa Kamati yangu jana wakati akiwasilisha Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, kuhusiana na suala la ubinafsishaji wa *TRC* na *NIC,* kusisitiza kwamba Kamati imetoa maagizo na ushauri wa kutekelezwa ili kuharakisha au kukwamua matatizo yoyote ambayo yanakwamisha au yanayochelewesha utekelezaji wa baadhi ya mambo ambayo yanatekelezeka, kama vile suala la kupunguza Wafanyakazi na kuirekebisha *NIC*, Kamati yangu imependekeza na kushauri kwamba *NIC* ichukue hatua za kuongeza uwezo wa fedha ili kuweza kuiongezea thamani *NIC* ya kibiashara na ya rasilimali pamoja na kupunguza madeni ili ubinafsishaji au urekebishaji wa Shirika hili uliweke katika hali nzuri, kwa mfumo utakaoamuliwa na wahusika waliokabidhiwa dhamana hii, kwa kuzingatia ushauri wa Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kamati yangu inatarajia Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, *PSRC, NIC* na Jumuiya ya Wafanyakazi watarejea kwenye Kamati na hatua zitakazofikiwa, na Kamati itarejea kwenye Bunge hili na matokeo ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake, inaomba fedha kama ifuatavyo:- Fungu 50 – Wizara ya Fedha, jumla ya shilingi 291,842,256,000; Fung 22 - Deni la Taifa, shilingi 609,147,867,000; Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali, jumla shilingi 106,760,578,000; na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jumla shilingi 12,362,932,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii tena nimshukuru Waziri wa Fedha, Manaibu Mawaziri wa Fedha wote, Watendaji wote kutoka Idara, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara ya Fedha jinsi walivyoisaidia Kamati kazi zake kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 87(4) ya Kanuni za Bunge napenda nichukue fursa hii niwapongeze Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango na maoni yao pamoja na kufanya kazi kwa tija na ufanisi. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Adam K. Malima, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Charles M.

Kajege, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru na kumpongeza, Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S.L. Foka na Makatibu wa Kamati, Ndugu Anselm Mrema na Hellen Mbeba, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga Mkono Hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHESHIMIWA FATMA ABDULHABIB FEREJI (K.n.y. KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI NA MSEMAJI MKUU WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 43(5)(b)(c) na 81(1), Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema na Upendo, kwa kutujalia kukaribia kumaliza shughuli zetu za Bunge hili la bajeti, katika hali ya usalama, amani na katika kutujenga katika umoja ambao ndio ngao kuu ya kushinda katika vita vyetu vikuu vya kujenga Demokrasia ya kweli, ambayo ndio nyenzo muhimu katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijami nchini mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Spika, Mheshimiwa Samweli J. Sitta, Mbunge na wewe Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Makinda pamoja na Wenyeviti wanaokusaidia kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge letu katika misingi ya kidemokrasia na kuhakikisha hadhi na uhuru wa Bunge unaheshimika na kulindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitakishukuru chama changu cha CUF kwa kuniteua kuwa mgombea kwa tiketi ya chama hicho na ushirikiano kilichoutoa kuhakikisha ninashinda. Aidha, sitaweza kuwasahau wananchi wa Jimbo la Mjimkongwe kwa maana nitaendelea kutetea haki zao na Watanzania wote kwa

ujumla kwa sababu Haki na Usawa ndio misingi yetu. Nia yetu ni kumsaidia Mtanzania aondokane na umasikini wa kila aina na nitasimamia hilo daima.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba kutoa pole kwa ndugu, rafiki, jamaa na familia za marehemu, Hayati Mheshimiwa Amina Chifupa pamoja na mzee wetu Chifu Abdallah Said Fundikira. Mola awape subra marehemu wote waliotangulia mbele ya haki. Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amin*!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishikuru familia yangu, watoto wangu na kwa aina ya kipekee namshukuru mume wangu Bwana Breik kwa kunipa moyo wakati wote wa kazi zangu. Bila ya ushirikiano wao, kunipa moyo na kunivumilia nisingefanikiwa kiasi hik. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke kuwa madhumuni ya Kambi ya Upinzani ni kujenga na sio kubomoa. Hivyo kwa yale yote yenye manufaa kwa Taifa, Kambi ya Upinzani inawahakikishia watanzania kuwa itaendelea kutoa ushirikiano wa hali ya juu na Serikali, lakini kama mambo yanakwenda tofauti na matarajio ya wananchi, Kambi ya Upinzani hata kwa sekunde haitasita kuikumbusha Serikali juu ya kasoro hizo kwani sote mdau wetu ni mmoja na ni Mtanzania. Hivyo, katika hotuba yangu leo naomba nigusie mambo machache tu nikianza na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Kambi ya Upinzani ilionyesha ni kwa njia gani Serikali ingeweza kuimarisha Mamlaka ya Manunuzi kwa kujitegemea na kwa jinsi gani Serikali ingeweza kuboresha manununuzi ya umma kwa kufuata kifungu cha sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa bado Wizara, Idara na asasi nyingi za Serikali zinafanya manunuzi bila kufuata masharti yaliyomo ndani ya sheria hii. Taarifa kutoka kwenye kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika mwaka 2005/2006, Sura ya Saba, inathibitisha kuwa katika manunuzi ya umma kwa kutumia mfumo wa sasa kuna upotevu mkubwa wa fedha. Kwa mwaka huo wa fedha kiasi cha sh. 67.2 billioni kilipotea bila ya maelezo yanayojitosheleza kutokana na kutokufuatwa kwa sheria ya manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo unotumika sasa kwa manunuzi ya umma una mlolongo mrefu na unaongeza gharama za utangazaji kwenye magazeti, gharama za utengenezaji wa majarida, fedha pamoja na rasilimali watu. Kwa mfano, kila zabuni kisheria inatakiwa itangazwe katika magazeti matatu ya kila siku kwa bei ya shilingi 500,000 kwa kila gazeti moja maana yake ni shilingi 1,500.000 kwa zabuni moja. Wakati kama tungelitumia mtandao pesa hizi zingetumika kwa zabuni nyingi na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoripotiwa na Tume ya Takwimu ya Taifa Juni, 2006 kuwa Serikali ya Tanzania inaripotiwa kutumia asilimia 70 ya fedha za matumizi ya kawaida *(Reccurent Expenditure)* katika manunuzi ya bidhaa na huduma, kwa kutumia takwimu za mwaka 2005/6 fedha za matumizi ya kawaida zilikuwa bilioni

2,018 na hivyo Serikali ya Tanzania ilitumia karibu ya shilingi bilioni 1,410 kwa ajili ya manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kipindi kirefu sasa inatambua kuwepo kwa rushwa iliyokithiri Tanzania na imekuwa ikijitahidi kupunguza. Inakadiriwa kuwa kwa ngazi ya Taifa karibu asilimia 20 ya manunuzi ya Serikali katika miradi hupotea kutokana na rushwa, hasa kupitia hongo na njia za kughushi. Kwa kuwa ununuzi wa vifaa vya umma unatumia kwa asilimia 70 ya bajeti yote ya matumizi ya kawaida, basi ni dhahiri kuwa serikali hupata hasara ya shilingi bilioni 300 kwa mwaka, kiasi ambacho kwa jumla kinatosha kabisa kwa bajeti ya Wizara ya Afya na Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango hiki kinazidi kile cha Serikali ilichoongeza katika kodi ya mafuta ambayo inazidi kumwongezea umasikini mtu wa kawaida, hivyo ni wazi kuwa hasara hii kiuchumi haivumiliki. Kwa hiyo, hoja ya kutaka mfumo wa sasa kufanyiwa marekebisho ya haraka iko dhahiri kama kweli Serikali inakusudia kutumia vizuri rasilimali za walipa kodi, kupambana na rushuwa na kuongeza ufanisi katika manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tunarudia tena ushauri wetu tulioutoa toka mwaka 2003 wa kutumia manunuzi ya mtandao *(E-Procurement),* ambao kutokana na nchi nyingi zinazotumia hivi sasa zimeweza kupunguza gharama za manunuzi kwa wastani wa asilimia 15. Kutokana na kiwango hicho cha manunuzi, basi Serikali ingeliweza kuokoa takriban shilingi bilioni 211 kwa mwaka ambazo zingeweza kutumika katika masuala mengine ya maendeleo.

Mfumo wa sasa wa manunuzi una matatizo mengi, kwa mfano, ripoti ya Benki ya Dunia yaani *(Review of World Bank Financed Projects)* iliyofanya uchambuzi juu ya matatizo yaliyomo katika mfumo wa sasa wa manunuzi nchini mwetu, waligundua udhaifu ufuatao:-mipango dhaifu ya uagizaji wa vifaa unaopelekea ufungwaji wa vifaa *(packaging)* usiowiana na thamani halisi ya kifedha ya vifaa husika; uchache wa matangazo unaokwaza upatikanaji wa *potential bidders* na hiyo kupunguza ushindani kati yao na thamani halisi ya kifedha; kutumika zaidi kwa njia ya ununuzi, kunakopunguza sehemu ya gharama za miradi zinazofikiwa kupitia njia zinazokubalika za utoaji wa zabuni; upungufu katika utayarishaji wa uhifadhi mzuri wa kumbukumbu za mchakato wa zabuni unaorudisha nyuma msukumo na ukaguzi mzuri wa miradi; taarifa za tathmini zisizowiana kiubora, zinapelekea maombi yasiyo ya wazi na vigezo vya tunzo; kutokuwepo uhalisia wa kukamilishwa kwa utekelezaji ndani ya kipindi kilichoombwa, hali inayopelekea kuongezwa tena kwa gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa manunuzi wa sasa unalidwa na Sheria Na. 21 ya mwaka 2001 *(Procurement Act).* Katika sheria hii na ile ya marekebisho ya mwaka 2004 ilitoa uwezo wa kuanzishwa kwa taasisi kubwa mbili ambazo ni *Public Procurement Regulatory Authority (PPRA)* pamoja na *Procuring Entities.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inayo asasi ya manunuzi *(procuring entity)* maarufu na inayostahili kuwa na uwezo wa kuratibu manunuzi yote ya umma. Asasi hii

inajulikana kama *Central Tender Board*. Lakini pamoja na hilo tunazo pia mamlaka za manunuzi za *Ministerial/Independent Tender boards* kwa kila Wizara, Mkoa, Wilaya, na halamashauri *(The Local Government Authority Tender Boards)* ambayo ipo Tanzania pekee ukilinganisha na nchi nyingine Afrika ya Mashariki. Lakini pamoja na hizo pia tunazo za mashirika ya Umma *(Parastatal Tender Boards).*

Kwa kifupi tunaweza kusema kuwa Tanzania ina mlundikano wa taasisi za manunuzi na kila moja kama ikitangaza zabuni moja kwa mwezi, gharama zake zinatosheleza kujenga shule moja kwa mwezi. Mbaya zaidi inasababisha kuwepo kwa wafanyakazi ambao wanafanya kazi zinazofanana katika kila ngazi hivyo kusababisha upungufu wa wataalamu wa manunuzi na upotevu wa fedha na rasilimali kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Serikali ya mwaka jana kuwa Watanzania wengi ambao wanafanya biashara bado hawajakuwa wazoefu katika mtandao, hivyo kwa kufanya *e-procurement* tutawanyiwa wazalendo nafasi za kupata zabuni, imepitwa na wakati kwa sababu suala la *e-procurement* haliepukiki duniani hasa ukizingatia mlipuko wa *e-commerce/government* katika nchi zinazoendelea. Aidha, mfanyabiashara ambaye hajaweza kuingia katika matumizi ya mtandao, huyo hana hata sifa ya kuingia kwenye zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida za *e-procurement* hazitaishia kuokoa fedha za serikali zinazopotea bali pia utaimarisha utaratibu mzima wa manunuzi kwa kupunguza rushwa, upendeleo na kuongeza ufanisi. Kambi ya Upinzani inapendekeza kanuni zinazotokana na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2001 iliyorekebishwa 2004 ieleze utaratibu wa kutumia *e-procurement* katika manunuzi yetu.

Aidha, Mamlaka ya Manunuzi itumie utaratibu huu kwa ajili ya kujitegemea kwa kukusanya mapato ya wale watakaotumia utaratibu huu na wale watakaonunua zabuni. Utaratibu huu pia utaipatia mapato Serikali na hivyo kupanua wigo wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla ya yote naomba nitoe pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na watumishi wake wote. Pamoja na ukweli kikatiba kuwa ofisi hii inapaswa kuwa inayojitegeme, historia imeonyesha kwamba ni Wizara ya Fedha ndiyo inaiombea fedha ofisi hii *(Vote* Na.45). Hazina pia ndiyo inayochagua maafisa wahasibu wanaokaguliwa na ofisi hii. Aidha, hazina ndio inayochagua Mkaguzi wa nje wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa mujibu wa *Public Finance Act* inayotawala ofisi hii, ni dhahiri kuwa Wizara ya fedha inawajibika kwa uimarishaji na ufanisi wa ofisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua unyeti wa ofisi hii ndio maana Kambi ya Upinzani inaendelea kutoa maoni yake juu ya ofisi hii. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 143, Ofisi hii ina majukumu yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha kwamba fedha zozote zinazokusudiwa kutolewa kutoka katika mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali matumizi yake yanaidhinishwa na kwamba zitatolewa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 136 ya Katiba.

(b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Bunge na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumizi hayo yamefanywa na kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo. Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya mwaka 2005/2006 iliyotolewa tarehe 31 Machi 2007 katika kutekeleza jukumu namba (3) kikatiba, ilipokelewa vizuri na Serikali kwa kutambua umuhimu wa uwajibikaji wa Serikali ndani ya nchi. Kambi ya Upinzani kupitia nafasi hii tunapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuipokea taarifa iliyotolewa na ofisi hii na kuifanyia kazi. Tunachoomba ni kufuatilia kwa vitendo kwa kuchukua hatua madhubuti kwa watakaobainika na kukiuka taratibu za matumizi ya Fedha za Serikali. Maana ni vizuri kukemea, lakini ni vizuri zaidi kuchukua hatua ili kutoa funzo kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha, nchi yetu imeshuhudia ongezeko la imani ya wafadhili, zaidi ya nchi 14 ambao wameipatia Serikali fedha takriban dola za kimarekani milioni 700 kama mchango wa jumla kwenye bajeti *(General Budget Support)*, ukilinganisha na Dola za Kimarekani milioni 200 zilizotolewa mwaka uliopita (2006/2007). Hatuna hakika kama Serikali imekwishajiongezea uwezo wa kutumia ongezeko hili kubwa katika kipindi kifupi. Ni vema Waziri akatuelezea namna walivyojitayarisha kiutendaji kutumia ongezeko hili la mapato. Maana si hoja kupata, hoja ni namna ya kutumia kipato hicho, unaweza ukanunua ndege nyingine inayotua viwanja viwili tu badala ya vitatu vilivyopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi hii ni muhimu katika kuendelea kujenga imani kwa walipa kodi wetu na ya wahisani kwa matumizi ya fedha zao wanazotoa. Kwa mfano, mchango wa mapato ya ndani ni trilioni 3.5, wafadhili kwa mwaka huu ni trilioni 2.5. Hizi ni fedha nyingi sana zinazohitaji ukaguzi madhubuti wa ofisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo katika kuimarisha uwezo wa ofisi hii, Kambi ya Upinzani inaunga mkono hatua ya kutunga sheria ya ukaguzi *(Audit Act)* kuwepo kwa sheria hii kutaimarisha maeneo yafuatayo:- Bajeti ya ofisi hii haitakuwa tena lazima kutegemea maoni ya Hazina kwani utaratibu unaotumika na nchi nyingi ambazo tayari zina sheria ya ukaguzi zikiwemo Kenya na Uganda. Bajeti zao hupitishwa na *Audit Commission* na kupelekwa moja kwa moja Bungeni.

Kwa mujibu wa taarifa tulizonazo ofisi hii katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 iliomba shilingi bilioni 18.2 ili kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi. Lakini cha kustaajabisha ni kwamba pamoja na unyeti wa ofisi hii Serikali imeamua kuidhinisha shilingi bilioni 10 tu kwa ajili ya ofisi hii na bajeti ndogo ya maendeleo ya kiasi cha

shilingi bilioni 2.3.Madhara ambayo yanaweza kutokana na kutengewa bajeti na mkaguliwa yaani Hazina, ni makubwa sana ambayo yanaweza kuwa ni hatua za kimakusudi za mkaguliwa kuzorotesha shughuli za ukaguzi. Kuwepo kwa bajeti ndogo ya maendeleo katika ofisi hii kunaathiri pia ukaguzi kwa kuzingatia ukweli kwamba wakaguzi lazima wawe na ofisi zao na sio kutegemea ofisi za wakaguliwa. Madhara ya jambo hili ni kwamba wakaguzi kukaa katika ofisi moja na wakaguliwa kwa muda mrefu kunasababisha watumishi kujenga urafiki wa karibu na hivyo ni kuweka mwanya wa kufichiana siri na kuharibu kabisa dhamira na lengo la uaminifu katika utumishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii itampa uhuru Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali wa kuajiri watumishi anaowahitaji kufuatana na mahitaji yake bila ya kutegemea viwango vya ikama *(cealings)* kutoka Utumishi serikalini. Umuhimu wa ofisi hii hauwezi kulinganishwa na asasi zingine za Serikali. Sasa ni wakati muafaka Serikali ikaipatia ridhaa ofisi hii ili iweze kuajiri wafanyakazi wake kutokana na kiwango cha taaluma na uaminifu badala ya mfumo unaotumika sasa wa kutumia Utumishi. Naongelea hili kwa sababu Wizara ya Utumishi pia ni moja ya maeneo yanayohitaji kufanyiwa ukaguzi na ofisi hii. Hivyo yule mfanyakazi anaweza kuwa na woga wa kufichua uovu wa Wizara hii kwa kuhofia kibarua chake. Aidha, sheria hii itaimarisha uhuru wa mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(functional independence)* ili afanye kazi yake kama anavyopanga kitaalamu na kwa miujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wetu tunaotaka kukuzwa kwa uwajibikaji nchini tunategemea sana kuundwa kwa Sheria ya Ukaguzi. Pia wafadhili wanaosaidia nchii hii wametaka kuwepo kwa sheria hii kama kigezo *(Prio Action)* muhimu katika kutoa misaada. Kutokuwepo kwa sheria hii kunaweza kukasababisha upungufu wa fedha katika maeneo yafuatayo, kama tulivyoeleza awali *General Budget Support* imeongezeka kutoka shilingi milioni 200 hadi 700 katika mwaka huu. Na kuna uwezekano wa kuongezeka hadi kufikia bilioni 1 mwaka ujao kama alivyoeleza Mheshimiwa Balozi wa Uingereza katika semina na Wabunge tarehe 6, Juni, 2007. Kutokuwepo kwa sheria ya ukaguzi kutatupunguzia uwezekano wa kuongezeka kwa fedha kutoka katika chanzo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano ya awali yalionyesha kuwa muswada wa kuanzishwa sheria hiyo ungewasilishwa Bungeni mwezi wa Februari, 2007 baadaye Serikali ilomba iwasilishe mwezi Novemba, 2007.

Tunaisihi Serikali ifanye hivyo ili kukinga athari itakayopatikana kutokana na kutokuwepo kwa sheria hiyo. Tumesisitiza hili kwa sababu serikali yetu ina historia ya kutokufuata masharti tuliyokubaliana na wafadhali ambayo hutupelekea kukosa au kupungua misaada tuliyoahidiwa. Kwa mfano, mradi wa *Public Finacial Management Reform Program – PFMRP* ulipata kiasi kidogo cha fedha baada ya Serikali kushindwa kutengeneza mpango wa kutathmini mradi *(Strategic Review),* ambao unapaswa kukamilika Oktoba, 2007. Mradi wa Benki ya dunia wa MKUKUTA *(World Bank Poverty Reduction Support Credit –PRS*C) ambao ilikuwa ni kuimarisha ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambapo kigezo Na. 6 cha mradi huu kilikuwa ni kuwasilishwa Bungeni kwa mswaada wa Sheria ya *Audit*, kutokana na makubaliano na Benki ya Dunia, kama kigezo *(Prior Action)* hakikutimizwa kwa wakati uliokubaliwa,

kutakuwa na punguzo kwenye bajeti *General Budget Support* na pia kwenye mradi wa MKUKUTA – *PRSC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Serikali iliposhindwa kutimiza kigezo kimoja cha Sheria ya Barabara ya kuletwa kwa mswada kwa wakati wa makubaliano, ilisababisha Serikali kukosa katika Bajeti Dola za Kimarekani milioni 10 ambazo ni takriban *Tshs.13 billion.* Kama kigezo cha kuleta mswaada wa sheria wa Ukaguzi (*Audit Bill)* katika Bunge la Novemba, mradi wa MKUKUTA – *PSRP* wa Dola za Kimarekani 250 milioni, takriban *Tshs.* 300 *billion* zitapunguzwa kwa asilimia 5 hadi 7 ambazo ni Dola 12 mpaka 15 takriban *Tshs.* 20 *billion.*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuwepo kwa sheria ya ukaguzi ni kigezo muhimu katika kuendelea na mradi wa *National Audit Office Development Project (NAODP)* unaofadhiliwa na Sweden. Pamoja na hilo ofisi za ukaguzi hukaguliwa na kuwekewa daraja la ufanisi ambao hupangwa kwa madaraja matano (I-V). Ofisi yetu sasa hivi daraja lake ni la mwisho yaani 1, ukaguzi utakaofuata wa Shirikisho la Wakaguzi wa Afrika yaani *AFROSAI* litafanyika mwaka 2009 na ili ofisi iweze kusogea angalau daraja la tatu panahitajika kuwepo kwa sheria ya ukaguzi *(Audit Act).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano tuliyoonyesha inadhihirisha ni jinsi gani Serikali inavyojiwekea mazingira ya kushinikizwa na wafadhili, hatua ambazo Serikali ingeweza kuchukua bila ya kushinikizwa. Kwa mfano, jambo la Sheria ya Ukaguzi lina mantiki ya kuimarisha uwajibikaji wa Serikali kwa fedha za umma na ni zuri kwa Taifa letu. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kulazimishwa kufanya hivyo. Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali iliokoe Taifa hili kutokana na aibu ya kushinikizwa na wafadhili kutimiza wajibu wake ipasavyo na kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa sababu tulizotoa hapo ni dhahiri kwamba muswada wa Sheria ya Ukaguzi hauna budi kuletwa Bungeni ili kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kukidhi mategemeo ya walipakodi na wachangiaji wa bajeti yetu. Aidha, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwepo kwa Sheria ya Ukaguzi ili kuwezesha kuundwa kwa *(Audit Commission)* ambayo itakuwa na mamlaka ya kupitisha bajeti itakayozingatia matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo kulingana na mahitaji ya ofisi hiyo. Pia Mkaguzi wa Nje *(External Auditor)* atachaguliwa na *Audit Commission* na sio Wizara ya Fedha kama ilivyo sasa. Mtindo huu wa sasa umesababisha hesabu za ofisi hii kutokaguliwa kwa wakati unaotakiwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu umuhimu wa Benki Kuu ya Tanzania kwa taifa. Benki Kuu ni moja ya mhimili mkubwa wa uchumi wetu. Kwa sababu yenyewe ndiyo yenye mamlaka ya kuangalia, kudhibiti na kuratibu uchumi wa nchi kwa kuratibu na kudhibiti mfumuko wa bei pamoja na kulinda thamani ya fedha yetu. Faida inayopata Benki hii ambayo kwa kiwango kikubwa inatokana na biashara inayofanya na Serikali, ni kubwa sana. Kwani kwa mfano kutokana na ripoti ya mwaka 2004/05 ya Benki Kuu *(Bank of Tanzania Annual Report 2004/05)* inadhihirika kuwa ndani ya mwaka 2004 Benki hii iliweza kupata faida yaani *net profit* ya takriban *Tshs.* 127,487,492,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kustaajabisha na kutia mashaka ni kuwa ndani ya mwaka huo huo, gawio la Benki Kuu, kwa Serikali ilikuwa ni shilingi 4,778,847,459 tu. Hii inamaanisha ni asilimia 3.8 ya faida ndio Serikali ilipewa kama gawio. Pengine ni kutokana na uzoefu wetu mdogo ndio maana hatukufahamu undani wa hili, hivyo, Kambi ya Upinzani kwa kuzingatia umuhimu wa suala hilo tunaitaka Serikali itupatie ufafanuzi ufuatao:- Serikali itupe maelezo ya kina kwa nini gawio la Serikali ni dogo sana ukilinganisha na faida ya Benki? Je, hizo pesa nyingine zilikwenda wapi ilhali gharama nyingine *(operation costs)* zote zilikwishatolewa ili kupatikana faida hiyo? Na ni kwa kutumia vigezo vipi Serikali inaweza kupanga faida yake kutoka kwenye taasisi hii ambayo inapelekea kupatikana kwa faida kidogo na nyingine isieleweke inakokwenda? Je, Zanzibar nayo ilipata kiasi gani cha gawio?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala jengine ambalo Kambi ya Upinzani imeona ni bora kupata majibu muafaka ni kuhusiana na takwimu za ripoti ya benki hii na ripoti zinazowasilishwa na Wizara kwenye kitabu cha *financial statement and revenue estimates (volume 1).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia mwaka huo huo wa 2004/2005 Benki Kuu ya Tanzania katika ripoti yake imeonyesha ya kuwa gawio la Serikali katika mwaka huo ni takriban shillingi bilioni 5 wakati kwenye kitabu cha Wizara *Volume I* tulichokitaja hapo juu ndani ya mwaka huo huo unaonyesha kuwa gawio la Serikali kutoka katika Benki Kuu ni shilingi bilioni 7.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, imeona hapa kuna mushkeli na haina budi kupata maelezo ya kutosha. Kambi ya Upinzani inapenda kuelimishwa ni kwa nini kuna tofauti kubwa kiasi hichi? Si hayo tu, bali kitu kingine tulichotambua wakati tukisoma takwimu hizi ni ukweli kuwa kuna matatizo ya makadirio ya ajabu ndani ya kitabu cha Wizara ya Fedha cha *Volume I.* Kwa mfano, katika gawio la Serikali kutoka Benki Kuu mwaka wa fedha wa 2004/05 Wizara ilikadiria kupata shilingi bilioni 2.8 wakati ikafanikiwa kupata shillingi bilioni 4.8. Wakati katika mwaka 2005/2006 walikadiria kutokupata chochote yaani 0. Lakini mapato yakawa shillingi bilioni 6.2. Hili si jambo baya lakini ukweli ni kuwa linatupa wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kwa kutumia vigezo gani vinavyofanya Wizara hii kukadiria kidogo na kuweka katika vitabu lakini hatimaye matokea yanakua tafauti. Baya zaidi Serikali haijawahi kutupa taarifa ya mapato ya ziada na yanavyotumika ili Bunge likaidhinisha au huu ndio utaratibu wa Kiserikali. Sisi tusio na uzoefu na ujuzi tunaomba kuelimishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu ni chombo cha Muungano na kinatarajiwa kuwatendea haki wanahisa wake hata kama mmoja ni mdogo. Zanzibar inayo benki yake- Benki ya Watu wa Zanzibar *(Peoples Bank of Zanzibar-PBZ)* ambayo ilikuwa inamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100 kama ilivyokuwa *NMB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha wakati Serikali inata kuibinafsisha *NMB,* Benki Kuu ilichukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kuipatia uongozi na kuwapa kila aina ya biashara ili kukuza mtaji wao, hadi iliponona ndipo baadhi ya hisa za *NMB* zikauzwa. Jambo la kusikitisha ni namna Benki Kuu ilivyolishughulikia suala la ubinafsishwaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ).* Ilijaribu kuipatia uongozi wa kama ilivyofanya kwenye *NMB*. Lakini pamoja na hilo waliinyang'anya *PBZ* hata zile huduma walizokuwa wakizitoa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Na kazi hizo zinafanywa na *BoT* yenyewe hadi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kwa Zanzibar *BoT* inafanya kazi za Benki ya biashara, kwa makusudi ya kuiua *PBZ.* Hivi leo inabinafsishwa kwa ya bei chee. Kitendo hiki ni cha makusudi na suala hili lilielezwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi, lakini *BoT* haikuwa na nia nzuri kwa *PBZ* ndiyo maana ikafikishwa ilikofika. Je, Mheshimiwa Spika huku ndiyo kuimarisha Muungano wetu? Tunaomba maelezo ni kwa nini *BoT* iinyang'anye *PBZ* zile shughuli ambazo zikiipatia mapato?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge ya mwaka 1988, kifungu cha 10, nilimwandikia Waziri barua, KUB.B7/07/07 ya tarehe 17.7.07 na kuinakili kwako Mheshimiwa Spika na kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikiomba taarifa zifuatazo:

(a) Taarifa ya Ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka 2005/2006 pamoja na *Management Letter* inayohusu ukaguzi huo.

(b) Taarifa ya Ukaguzi uliofanywa na *Delloite & Touch,* 2004/2005, na ya 2005/2006 ambayo haikuwa kukamilika pamoja na *Manegment letter* kwa miaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze na kulieleza Bunge lako Tukufu ni kwa kutumia ibara ipi ya Katiba na kifungu gani cha sheria kilichompa malaka ya kuninyima taarifa hizo hadi leo hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kila Mkutano wa Bunge la Bajeti, Wabunge kwa ujumla wao, wamekuwa wakilalamika juu ya wafanyabiashara wanaolipa kodi Zanzibar na hatimaye kutakiwa kulipa tena hapa Tanzania Bara. Hili limekuwa donda ndugu na kila mwaka ufafanuzi hutolewa lakini inaelekea ni mkakati kwamba nyinyi mtasema sisi tutaendelea .

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna utaratibu wa kupitisha mizigo bila kukaguliwa kwa wafanyabiashara waaminifu. Hivi hawa wa Zanzibar ndiyo waonekane sio waaminifu tu? Usumbufu na unyanyasaji bado upo. Kambi ya Upinzani mwaka huu tunataka hili lipate ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha wabunge tumekuwa tukilalamika juu ya magari yanayotoka Zanzibar kuchukuliwa kama magari ya kigeni, na maelezo tunayopewa hapa kuwa hilo siyo kweli! Hapa mimi nina risiti za malipo ya *USD* 25 kila mwezi kwa gari Na. ZNZ 53463 inayomilikiwa na Bwana Abdulahamid Mohamed. Je, Zanzibar ni nchi

tofauti si Sehemu ya Jamhuri ya Muungano? Je, Zanzibar haimo katika Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki au na wao Zanzibar wazitoze kodi gari zilizosajiliwa Bara? Kambi ya Upinzani na hili inaomba limalizike.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya kukusanya kodi Zanzibar, Mamlaka ya Mapato Tanzania, katika shughuli zake huko, uwakala wa ukusanyaji mapato au huduma, kwa mfano wako *TICS* na *Clearing Agents* na kadhalika, ili kuondosha usumbufu kwa nini *TRA* Zanzibar hawawapi uwakala bodi ya mapato Zanzibar (Zanzibar *Revenue Board*) kukusanya mapato yote ya *TRA* Zanzibar ili kupunguza gharama za uendeshaji. Hasa ukizingatia kwamba makusanyo yote hubakia katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa nini chombo cha umma kinanyimwa uwakala wakati makampuni binafsi yanapewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo kwa waliokuwa watumishi wa Jumuia ya Afrika Mashariki, Kitengo cha *Income Tax,* gonjwa hili la mafao ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki sasa linaelekea kuwa sugu na kukosa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitengo cha *Income Tax* ni mojawapo ya vitengo vilivyokuwa vikitumikia Jumuiya ya Afrika Mashariki kabla ya kuvunjika kwake mwaka 1977. Jumuiya hii ilianza kumeguka mwaka 1973 na ndipo watumishi wa Idara hii walipohamishiwa katika Wizara ya Fedha. Kwa upande wa nchi yetu watumishi hawa walikuwa takriban 400 na wote walihamishiwa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni haki ya kila mtumishi kupata mafao yake kulingana na muda aliotumikia pale atakapostaafu. Madai ya wastaafu hawa ambao wametumikia Taifa kwa maadili na unyenyekevu katika idara ya *Income Tax* ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni ya muda mrefu sasa na yamekuwa yakipuuzwa pamoja na kwamba wahusika wamekuwa wakifuatilia na kufuata ushauri wanaopewa ili kuweza kupata haki zao lakini hadi leo wanapigwa dana dana pamoja na kwenda Mahakamani. Cha ajabu wastaafu kutoka Idara ya Forodha, walikwishalipwa ambao nao pia walihamishiwa Wizara ya Fedha. Wenzao wa Kenya na Uganda walikwishalipwa miaka mingi iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashidwa kuelewa ni kwa nini watumishi hawa hawakujumuishwa kulipwa mafao yao kama watumishi waliowahi kulitumikia Taifa kupitia Jumuiya hiyo. Kama hoja ni kuwa walikwishakoma kuwa watumishi wa Jumuiya hiyo kwa nini watumishi wa forodha walipwe? Na kwa nini wale *income tax* wa Uganda na Kenya walilipwa mafao hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Namba 2 ya mwaka 1987 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliweka wazi kuwa Tanzania kama nchi ililazimika kulipa mafao kwa raia wake. Sheria inaweka wazi haki ya watumishi hao lakini kutowalipa malipo yao watumishi hawa ni kuwanyima haki zao. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo ya kina katika masuala yafuatayo:- Ni kwa sababu gani ya msingi inayosababisha kutowalipa watumishi hao mafao yao? Au ni mazoea ya Serikali mpaka ipelekwe mahakamani hivyo Serikali inasubiri hilo? *(Makofi)*

Ni kwa nini katika kumbukumbu za Hazina inaonyesha kuwa watumishi hawa wamekwishalipwa kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki toka mwaka 1974 ilhali Hazina kwa kupitia kumbukumbu zao wameshindwa kulithibitisha malipo hayo kwa kutoa taarifa ya Benki iliyotumika kuwalipia, nyaraka za *payment voucher* pamoja na kushindwa kutoa majina ya wale waliolipwa na *payroll* namba zao?Katika barua za kuajiriwa za watumishi hawa wakati wakihamishiwa Wizara ya Fedha Septemba, 1973 ambazo zilitoka Ofisi ya Rais zilionyesha wazi kuwa mafao yao yataendelea kuunganishwa pamoja na watakayovuna katika utumishi wao Wizarani. Je, hilo pia mnaligeuka?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, kama ilivyowaahidi Watanzania kuwa itaendelea kutetea haki zao siku zote. Na kwa hawa watumishi 400 wa Serikali, Kambi ya Upinzani inataka kupata maelezo kwa nini wastaafu hawa wasilipwe haki zao. Pia tungependa kuelewa ni kwa sababu gani kumekuwa na taarifa za kupotosha huko Hazina na na kwa nini kama kuna uvunjwaji wa sheria wahusika hawajuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kila bajeti ya Wizara Waziri katika kushughulikia matatizo ya wastaafu huwaomba Wabunge kama kuna malalamiko basi apelekewe. Mwaka 2006, nilimpelekea Waziri malalamiko ya aliyekuwa mfanyakazi wa Afrika Mashariki, Shirika la Posta na simu, Bwana Abdullah Issa Khamis, ambaye mbali na kuandika barua na kuiwasilisha vielelezo na mimi mwenyewe nilikwenda Wizarani kufuatilia hilo hadi leo hakulipwa wala hakuelezwa chochote. Eti leo ndio baada ya kuona kuwa kuna bajeti ya Wizara ndiyo kapelekewa barua eti apeleke barua alioajiriwa baada ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni ushahidi tosha unaoonyesha wastaafu wanavyonyanyasika, ikiwa huyu ni nimemfuatilia mimi, leo ndiyo anapelekewa barua. Je, hao wengine wasiokuwa na watetezi? Tunahitaji maelezo ya kina na kujulishwa ni lini mstaafu huyu atapatiwa mafao yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha *(JFC)* kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 134, na Katiba ya Zanzibar Sehemu ya Pili ibara ya 114 (Fedha zote ambazo ni sehemu ya mchango wa Muungano na ambao Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zinawajibika kulipa zitakuwa ni gharama inayotoka Mfuki Mkuu wa Hazina. Serikali iliidhinisha kuanzishwa kwa akaunti ya fedha ya pamoja, ambayo inatakiwa kuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ambamo kutawekwa fedha zote hizo. Sheria ya Tume ya pamoja ya fedha sura 140 ndiyo iliyotoa mamlaka ya kuanzishwa kwa Tume hii tarehe 3 Juni, 2003. Mshauri *(consultant)* ambaye alikuwa anangalia masuala haya yote ya muungano amefanya uchambuzi wa kitaalamu na ripoti yake imekwishawasilishwa katika Serikali zote mbili mwezi Agosti, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka Agosti, 2006 mpaka hii leo tayari mwaka umekwishapita. Kambi ya Upinzani na Watanzania, kwa ujumla inajiuliza ni hadi lini tutaendelea kuheshimu matakwa ya Katiba hizi mbili ya kuwa na mfuko wa pamoja utakaobainisha waziwazi mapato na matumizi ya Jamhuri ya Muungano? Kambi ya

Upinzani na Watanzania walio wengi wana matumaini sana juu ya Tume hii ambayo inaweza kuwa chachu ya kupunguza kero nyingi za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutahadharisha kuwa utafiti uliofanywa na Kambi ya Upinzani ni wa kina na maswali ambayo yameulizwa yanahitaji uchambuzi wa kina. Hatuhitaji majibu yaliyojaa utashi wa kisiasa kwani tuliyoyaidhinisha hapa ni masuala ya kitaifa na si ya kiitikadi. Hii ni nchi yetu sote inayojengwa na wenye moyo na kuliwa na wenye meno.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwashukuru wote kwa kunisikiliza na Mungu Ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha pamoja na marekebisho ya data kidogo niliyoyafanya.

**NAIBU SPIKA:** Ambao watafuata ni Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Omar Sheha Musa, hawa hawajachangia kabisa. Halafu Dr. Chrisant Mzindakaya na Mheshimiwa John Lwanji. Nimesema kwa kuanzia kuna wengine akiwemo Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Fedha. Natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na Manaibu wake wawili. Lakini pia na watendaji wote wa Wizara kwa jinsi walivyoandaa bajeti yao. Lakini pia kwa jinsi wanavyotenda kazi zao katika kuendesha Wizara ambayo ni Wizara nyeti katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaangalia vyombo viwili ambavyo viko chini ya Wizara ya Fedha. Napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge ambao katika vikao vilivyopita vingi wametoa pongezi nyingi kwa *TRA* kwa jinsi ambavyo tumeweza kukusanya makusanyo ya nchi hii. Tumeshuhudia chombo cha *TRA* kikikusanya mapato ambayo yamekuwa yanaongezeka mwezi hadi mwezi na mwaka hadi mwaka. Kwa kweli tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko sababu nyingi ambazo zimesaidia chombo hiki kutenda kazi vizuri. Lakini niseme sababu moja, leo hii ukiangalia chombo hiki, ukiangalia wafanyakazi wake wa ngazi zote ni kwamba ni wafanyakazi tofauti na iliyokuwa Idara ya Kodi hapo zamani. Wafanyakazi wa sasa ukiongea nao ni wafanyakazi ambao wa elimu nzuri wamejiendeleza. Ni kawaida sasa hivi kuongea nao, anakuambia kijana kwamba mimi nina *MBA* anakuambia mimi nina *MSC Finance* na yule ambaye hana elimu hii atakuambia kwamba mimi namalizia *CPA.* Atakuambia kwamba mimi bado nafanya kazi lakini pia najiendeleza kusoma. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba watendaji wameelimika na hili limewasaidia kuweza kutenda kazi yao vizuri.

Nasema hili kwa sababu sasa aina ya walipakodi na yenyewe imebadilika. Pia nasema hili kwa sababu ukitaka vijana waende kutunza kodi katika migodi katika

kampuni za madini lazima wawe vijana ambao wameelimika ndipo ataweza kutenda kazi vizuri na akasaidia nchi kupata mapato yanayofaa kutoa katika kampuni hizi za kisasa, kampuni za wawekezaji. Kwa hiyo, nazidi kuhimiza na kuielekeza *TRA* iendelee na mkakati huu wa kuelimisha vijana wetu ili waweze kutenda kazi kwa tija, waweze kuendelea kusaidia ili makusanyo ambayo tunahitaji kweli yazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri *TRA* wanakusanya mapato na makusanyo yanaongezeka. Lakini haitafaa lolote kama haya mapato hayatasimamiwa jinsi yanavyotumika. Kwa hiyo, muhimu kwamba Serikali yetu iweke mkakati wa kusimamia matumizi na mapato haya. Hasa katika mwaka huu katika mfuko wa barabara. Nachagua mfuko wa barabara kwa sababu katika mazungumzo mengi hapa kuhusiana na nyongeza ya bei ya mafuta, tumeeleza kwamba nyongeza hii itakwenda kusaidia mfuko wa barabara na barabara zitaboreka. Tunamaliza mkutano huu tunakwenda kwa wananchi na suala la nyongeza ya bei ya mafuta itabidi tulieleze. Maelezo mahususi ni kwamba barabara zitatengenezwa vizuri. Sasa kama matumizi ya Mfuko wa Barabara hayatasimamiwa barabara zikatengenezwa zikaboreka, barabara nyingi za vijijini zikatengenezwa hata ambazo hazikuwa katika orodha ya kutengenezwa basi wananchi wetu watatuona kwamba hii nyongeza ya bei ya mafuta hawakufaidika nayo. Kwa hiyo, nawaasa wasimamizi wote wa matumizi waweze kuhakikisha na sisi tukonao kwamba matumizi katika mfuko wa barabara yanakuwa manufaa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, sisi katika Kamati ya Fedha wakati ambapo ilikuwa hakuna Mkaguzi Mkuu, isipokuwa mkaguzi alikuwa ni mtu aliyekuwa anakaimu tuliongelea sana na kuitaka Serikali iteue mtu wa kuweza kushika wadhifa huo. Serikali ilisikiliza ikamteua bwana Utoah akashika nafasi hiyo. Ni muhimu kwamba sasa kuna mtu ambaye siyo kaimu isipokuwa anafanya kazi yake na ameteuliwa kamili na anakuwa na uwezo wa kuamua haraka haraka na kutenda kazi kwa kujiamini. Tuna imani na aliyeteuliwa na tunaona kama ameanza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi tuongeze mbinu za kuweza kufanya kazi hii ya ukaguzi. Sasa hivi kinachofanyika tunaita *traditional auditing* ambapo fedha zinatolewa, fedha zinatumika, baada ya mwaka, mwaka na robo, ukaguzi wanakuja kukagua hizo fedha na jinsi zilivyotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii katika fani ya uhasibu tunaita *traditional auditing* na katika lugha nyingine ya kiutani katika fani ya uhasibu tunaita *post-mortem auditing. Post-mortem* ni wakati jamaa anaugua, anapata homa, unamwangalia unanyamaza, anaugua kabisa unamwangalia unanyamaza, anakufa, hapo ndipo unamwita daktari aje akafanye utafiti amkate aangalie kwa nini amefariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napendekeza kwamba katika matumizi ya fedha zetu ndiyo *traditional audit* ingeendelea kuwepo lakini tuongezee mbinu nyingine za kusaidia kuzuia huyu mgonjwa kufariki au kufariki haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napendekeza kwamba mkaguzi mkuu awe na timu ndogo au vikosi vidogo ambavyo tunaweza tukaviita *rapid investigation teams*. Hivi vikosi vidogo ni kwamba huko katika Wilaya zetu, Wizara zetu, na Halmashauri zetu, tunapoona tuna hisia kwamba sasa hapa kuna neno, kuna jambo, tujinyamazie tu, tutoe taarifa tuombe kwa Mkaguzi Mkuu ili apeleke vikundi vidogo vije vikae wiki moja, mbili vitafiti, vihoji watu, vifanye shughuli na tutafaidika na jambo hili kwa sababu tutaweza kama kuna ubadhirifu. Kama kuna matumizi mabaya basi haya matumizi mabaya yatadhibitiwa.

Lakini pia si kwamba huu ukaguzi utakuwa hauna maana katika kuhusiana na ule ukaguzi tunaoita *traditional auditing*. Ni kwamba katika fani ya *auditing* tuna tabia ya kuweza kuamini *clears* ambayo imeshafanyika. Maana yake ile timu ikaja mwisho kufanya ukaguzi sasa inawezekana kabisa ile sehemu ambayo imeshakaguliwa na hii timu ya *rapid investigative auditing* basi wanaweza ile sehemu ya kazi hii wasifanye tena, wasiirudie wakaamini ripoti ya hii timu iliyokwishaandikwa kwa kufanyika na kuandikwa.

Kwa hiyo, naasa Idara ya Mkaguzi Mkuu iangalie suala hili ili iweze kuwa na timu hizi ambazo zinaweza zikawa zinafanya uzuizi wa matumizi mabaya ya fedha kabla fedha nyingi hazijatumiwa vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maongezi mengi miaka mingi katika Bunge hili Waheshimiwa Wabunge wameongelea suala la kufanyia kazi ripoti ya Mkaguzi Mkuu. Inafurahisha kwamba baada ya muda mrefu sasa Mheshimiwa Rais yeye mwenyewe amechukua hatua, akawaita viongozi wanaohusika, akawaelezea kwamba sasa huu ni mwisho. Kwamba sasa ripoti ya Mkaguzi Mkuu itakuwa inafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani kwamba hii ni kazi ya kumwachia Mheshimiwa Rais wetu. Hii ni kazi ya kufanywa na sisi katika Kamati zetu, katika vikundi vyetu, huko katika Halmashauri zetu kwa sababu ndiyo kazi hasa ya kuisimamia Serikali, kusimamia matumizi ya Serikali. Mheshimiwa Rais, inabidi ashughulikie yale matumizi mabaya sugu; inabidi ashughulikie wale ambao hawasikilizi, hawabadiliki. Lakini hii shughuli inabidi sisi kamati zetu tufanye kazi hizi tutumie ripoti ya Mkaguzi Mkuu na tupendekeze au tuchukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetoa ombi kwa Mkaguzi Mkuu kwamba ili tuweze kufanya kazi hii vizuri na kwa ufanisi ya kusoma ripoti yake katika kamati zetu na tukaweza kuchukua hatua, au kupendekeza hatua muhimu kwamba hii ripoti ikiandikwa ahakikishe kwamba inaandikwa katika lugha ambayo mtu ambaye hana taaluma ya kihasibu anaweza akaielewa vizuri. Akiandika katika lugha ya kitalaamu ikatuwia vigumu katika kamati zetu kuweza kuielewa. Ili uweze kujadili vizuri, uweze kuchukua hatua inabidi uelewe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napendekeza na namwomba Mkaguzi Mkuu ahakikishe kwamba hizi ripoti zake *(management audit reports)* ziandikwe katika lugha, katika ufafanuzi mpana ili ndani ya kamati zetu. Ndani ya Kamati katika Wilaya zetu na Halmashauri watu wote wazielewe kwa undani na kwa misingi hiyo wataweza kuzifanyia

kazi, wataweza kupendekeza mambo ya kufanya ili ziweze kuwa za manufaa katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo napenda kushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii kuwa mchangiaji wa kwanza lakini pia niseme kwamba naunga mkono hoja asilimia kwa mia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Katagira, yeye ni mtaalamu wa ukaguzi na ni Mwalimu wa kwangu, mimi na Mheshimiwa Utoah. Kwa hiyo, tunaendelea na msemaji mwingine Mheshimiwa Omar Sheha Mussa.

**MHE. OMAR SHEHA MUSSA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya upendeleo katika Mkutano huu wa Nane wa Bunge na kwa kawaida huwa sipendi kuongea, ni mtu mkimya kwa tabia yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo nimehisi nichangie hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa sababu kuna mambo yamenigusa sana katika hotuba hii, na nina mambo mawili tu. La kwanza, ni hili ambalo amezungumzia katika ukurasa wa 31 wa hotuba yake juu ya uhusiano kifedha baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na ile ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, historia inatueleza kwamba uhusiano wa Serikali hizi mbili umeanzia zamani sana. Hata wakati wa ukoloni, kama Wabunge wenzangu wanavyokumbuka ndani ya Bunge hili, kwamba iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika wakati huo kabla uhuru na zilizokuwa Jamhuri ya Ugunja na Pemba ambayo inaitwa Zanzibar sasa hivi, ziliungana mwaka 1964 na uhusiano huu wa kifedha baina ya nchi hizi mbili baada ya kuunga ulianzia toka ukoloni, na bahati nzuri zote mbili nchi hizi zimetaliwa na Waingereza, ingawa Zanzibar ilikuwa chini ya Waarabu wa Oman, lakini bado ilikuwa chini ya hifadhi ya Serikali ya Waingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uhusiano wetu ulianza na suala zima la sarafu, sote tulikuwa chini ya bodi ya sarafu ya Afrika Mashariki toka miaka hiyo. Kwa hiyo, nchi zetu mbili hizi, kabla ya kuungana hatukuwa na *central bank* au benki kuu ya pamoja na kwa maana hiyo kilichotuunganisha ni uhusiano ule wa kifedha uliokuwepo wakati huo na suala hili nalielezea kwa sababu.

Mheshimiaw Naibu Spika, nalikumbuka sana, mimi mwenyewe naongea haya na nina hakika nayo kwa sababu nimefanya kazi Serikalini kule Zanzibar miaka 30 kabla ya kujiunga na Bunge hili. Na katika umri huo wote karibu miaka 28 au 27 nilikuwa Hazina Zanzibar au Taasisi zake.

Sasa ninachoomba katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amezungumzia kwamba, Tume yake ya Fedha itafanya utafiti kuhusu uhusiano huo na vilevile itafanya *strategic plan.* Sina haja ya kunukuu kwa sababu yote yapo humu. Kwa hiyo, ninachoomba kusema ni kwamba, wanapofanya utafiti, Tume hii ya Fedha itilie

maanani Ripoti ya *IMF* ya mwaka 1994, ambayo imetayarishwa baada ya Ripoti ile ya Tume ya Shellukindo, kwa kufikia muafaka wakati ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa ni mmojawapo wa Wajumbe wa Tume ya Shellukindo na tulikuwa tunabishana kama Zanzibar ina haki au haina haki ndani ya Benki Kuu wakati ule. Serikali zote mbili zikakubaliana, tuwaajiri *IMF* watazame mambo yalivyokwenda na *IMF* bila kuchelewa, pamoja na muda mfupi waliopewa, wakatazama mambo haya, wakawasilisha Ripoti ya kwanza mnamo Machi, 1994 inayoeleza mambo matatu. Inaeleza fedha za Jamhuri iliyokuwa ya Tanganyika na inaeleza fedha za Zanzibar, ambazo zimewasilishwa Serikali ya Tanzania baada ya kuvunjwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1991. Kwa hivyo, naomba sana Tume hii inapotazama mahusiano haya baina ya pande mbili, iende sana kwenye Ripoti ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Ripoti ile iliondoa mabishano na pale Zanzibar ndiyo ikaamuliwa basi tuanzie na *formula* hii ya muda ya asilimia nne na nusu, kuwagawia chochote. Lakini *IFM* walisema wazi katika Ripoti ile kwamba, *formula* ile ni ya muda, bahati mbaya imechukua sasa hivi miaka 12, maana yake tumeanza kulipwa mwaka 1995 mpaka leo *formula* ile ya muda ni miaka 12 au 13. Sasa hii Tume ya Fedha ndiyo yenye *solution* au yenye ufumbuzi wa kuweza kuweka *formula* ya kudumu. *(Makofi)*

Tunaomba sana Tume hii Mheshimiwa Waziri, ikamilishe kazi yake. Mheshimiwa Waziri, kwa kweli nampongeza sana angalau yeye na Timu yake, wamekuwa na moyo mara hii kulivalia njuga suala hili. Kwa sababu suala hili la Tume ya Pamoja ya Fedha, limeanza kuzungumziwa toka ilipoandikwa Katiba ya Kudumu ya Tanzania mwaka 1977 na limeanza kugusiwa kwa mara ya kwanza mwaka 1984 katika Sheria za Jamhuri ya Muungano.

Bahati mbaya au nzuri, imechukua miaka 12 kuiandika Sheria ya Tume hii iliyotajwa humu namba mia mbili na ngapi sijui, imo katika kitabu hiki, kuandikwa Sheria ya Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ya Tume imeandikwa mwaka 1996, lakini imeanza kutekelezwa tena baada ya miaka 7 (2003) na leo hii tunazungumza 2007, baada ya miaka minne tena. Ninachosema, mtiririko wote huu wa kuchelewa si tatizo, tatizo ni nia ya kumaliza hii kazi. Ninachoomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atakapokuja ku-*wind* hotuba yake hapa, aliambie hili Bunge kuhusu hivyo vikao vya mashirikiano baina ya Jamhuri ya Muungano na Zanzibar. Suala hili tunaomba sana au naomba sana walimalize mwaka huu wa fedha angalau uletwe huu Muswada mwaka huu tumalize tena kwa sababu hii ndiyo kero kubwa ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano wetu haukai sawa, kama hatujaweka *formula* ya kudumu ya kugawana mapato na matumizi. Mapato na matumizi ni muhimu kueleweka yakajulikana, yakawekwa kwenye hesabu ya pamoja iliyotajwa kwenye Katiba na hili tusingojee tena, limekuwa la siku nyingi. Naomba sana na Waziri ananisikia hapa na mimi nampongeza, angalau yeye amekuwa na moyo wa kulileta hili.

Wenzake nyuma hapa kila mmoja anakaa pale Hazina miaka yake mitano analiacha, haligusi. Yeye ameligusa hili, tumpongeze jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa matumaini hayo, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, naamini hayuko sasa hivi Bungeni, lakini ataambiwa na Mheshimiwa Waziri Kiongozi naye ataambiwa, ninachosisitiza mwaka huu wa fedha 2007/2008, hii kazi waimalize, kwa sababu wenzetu Wapinzani nimewasikia hapa kila mara wanasema suala hili. Kwa nini waseme hilo wakati sisi wenyewe tunalijua, kwa nini tuwangojee wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nayasema haya kwa nia safi kabisa, mimi napenda Muungano uwepo na udumu kwa sababu una faida nyingi kuliko kasoro zake. Naomba sana kazi hii imalizike na kauli ya Mheshimiwa Waziri hapa akija basi atuambie iwe *timetable* tusiambiwe tu kwamba tuna *strategic* fulani, sijui tuna utafiti, hatutaki utafiti tena saa hizi, tumechoka utafiti jamani. Hii kazi wafanye tu, waweke fomu la kudumu ili tutulie. Hili la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nazungumzia kuhusu Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 25 kuhusu Miradi ya *Millenium Challenge Account.* Nimeona humu imeorodheshwa karibu miradi 11 ya *Millenium Challenge Account.* Ninachoomba vilevile kwa heshima tu kwamba, suala zima la miundombinu nalo kwa upande wa Unguja lifikiriwe. Kwa sababu bajeti hii ya mwakani ambayo tunaizungumza sasa hivi, miongoni mwa mambo ya kipaumbele, suala la miundombinu nalo limo. Sasa ingawa ninaelewa miundombinu si jambo la Muungano, lakini chini ya mashirikiano inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba ni kwamba, humu nimeona imezingatiwa miradi ya kutengeneza barabara sita za Pemba. Zanzibar imegawika majimbo 50 kimuundo. Majimbo 50 hayo 18 yako Pemba na 32 yako Unguja. Ningeomba sana sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atakapokuja kujumuisha hapa, atoe kauli kwamba na barabara za Unguja atazizingatia angalau kwa kima kidogo tu hata kama bilioni 15 tu, lakini ndani ya miaka hii mitano suala hili liwemo na kwamba naamini na nakuomba sana Bodi hii ya *MCC* ikikaa Septemba, basi na miradi hii ya upande wa majimbo za Unguja, majimbo 32 nayo yazingatiwe, kwa sababu nako kuna tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo sana na nayasema haya kwa dhati kabisa. Baada ya kusema hayo naomba kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kwa ufupi, naunga mkono hoja mia juu ya mia. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, niweze kuchangia kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwanza, ninampongeza yeye mwenyewe, Manaibu Waziri na Wasaidizi wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii, nawapa hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nilikuwa na jambo moja tu ambalo ningependa kuanza nalo. Nalo ni kuhusu na mapato yanayotokana na kodi. Juhudi inayofanyika sasa hivi ni kubwa sana na kila mtu anaona. Sitaki kurudia, watu wengi wameeleza namna *TRA* wanavyojitahidi kufanya kazi. Mimi nilikuwa na ushauri tu kwamba, kwa sababu nchi yetu ni tajiri sana kwa rasilimali, ingekuwa ni jambo zuri sana, tukaangalia tukatafuta wataalamu wakachunguza maeneo yote ambayo yangekuwa ni vyanzo vya kutupatia mapato. Kwa sababu utozaji wa kodi kwa vyovyote vile una mwisho. Kama hamwongezi njia za kuongeza mapato, utozaji wa kodi unaweza ukafika mahali ukakuta mmefikia mwisho. Maana yake kuna nchi ambazo unaweza ukakuta zinaongoza kwa kodi kubwa, nyingine kodi kiasi lakini wanakuwa na njia mbalimbali za kuongeza mapato yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii kwa kweli ni tajiri ukilinganisha na vinchi vidogo vidogo vinavyoshinda rasilimali ya nchi ni kubwa. Kwa hiyo, nilikuwa na ushauri huo kwamba, ingekuwa ni vizuri sana tuone namna ya kuongeza vyanzo vingine vya mapato, kuliko kuendelea kutumaini. Hata kodi yenyewe ukiona kwa kiasi kikubwa, kwa mfano, ukifika pale *Customs,* utakuta watu ni wengi sana kuliko hata Muhimbili. Kwa sababu ya kukomboa mizigo wanayoagiza kutoka nje. Maana yake ni kusema, sehemu kubwa ya mapato ya kodi ni kodi za ushuru wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi. Sasa mimi nashauri tutazame namna gani tunaweza tukaongeza uwezo ndani ya nchi yetu wenyewe kuliko kutegemea *imported goods*, ndiyo tukawa tunazitoza kodi peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya hilo, ningependa nisemee jambo lingine kuhusu uwezeshaji wa uzalishaji. Hili ni jambo la jimbo na mimi nataka niliseme lakini vilevile linahusu nchi. Nchi yetu ni nchi ya wakulima, tegemeo letu ni wakulima. Lakini jambo hili limesemwa sana hapa Bungeni na mimi nataka nirudie kwamba, wakulima wetu wengi bado ni wakulima wanaotegemea jembe la mkono. Tangu tumepata uhuru sasa yapata miaka 40, panga analotumia mkulima kufyeka, shoka analotumia mkulima kufyeka, hata wale wanaotumia maksai kwa kutumia plao, bado zana zote za mkulima zinatoka nje. Kwa hiyo, mimi nashauri tuanze kufikiria kama kweli tunaweza tukaendesha kilimo ambacho zana za mkulima ni tegemezi lazima tu-*import* kutoka nje jembo la mkono ili Mtanzania ili alime. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, utaratibu huu wa uwezeshaji ambao ni mzuri sana, kwa kule mikoani, sijui mikoa mingine, lakini kwa Mkoa wa Rukwa mimi nimeona kuna tatizo na Wabunge wengi walieleza hilo kwamba, wakulima wakitaka mikopo hii ya sasa wanaambiwa hapana, hii ni kwa ajili ya wajasiriamali. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nataka nikumbushie Wizara mambo ambayo tulifanya sisi na Wizara yenyewe na ambayo ningeomba niombe sana wakubali tuyatekeleze. Mkoa wa Rukwa tulileta mpango wa namna ya kutoa mikopo kwa wakulima na utaratibu huu ninaoueleza mimi, unatumika sana nchi ya Indonesia, unatumika Phillipenes na Bangladesh. Sisi tulileta mpango, ambao ulikubaliwa na *FAO*, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huo ulikuwa ni kutoa mikopo kwa wakulima. Benki tuliyoichagua wakati ule ilikuwa ni *NMB*. Tulichagua sisi wenyewe *NMB,* nao wakakubali, wakatuma wataalam wao, timu ya kwanza. Wakaja wakafanya utafiti, wakaona mapendekezo yetu yalivyo mazuri. Lakini kabla hawajaamua kwenye Bodi,

wakaamua kwamba, watafute *Private Consultant,* wa kuja kuchunguza juu ya mradi huu wa kukopesha mkulima. Walipokuja wakatoa mapendekezo ya hali ya juu sana kwamba, mpango huu ni mzuri na ungefaa utekelezwe na mpango huu ni nini? Tulikuwa tumependekeza, tulichagua kwanza vijiji, tukachagua wakulima kwa majina, tukawaandaa na nia ni kuondoa wakulima kutoka jembe la mkono kwenda jembe la kukokotwa kwa ng'ombe, ambalo ni *sustainable.* Ni kitu kinachoweza kuendelezwa, kwa sababu sasa hivi ukizungumza trekta kwa mkulima wa kawaida unamwumiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya tairi la trekta miaka ya 80 wakati mimi nikiwa Mkuu wa Mkoa pale tulipoanzisha mpango wa kilimo Morogoro, kwa wakati ule ilikuwa ni matrekta mawili, sasa ndiyo bei ya trekta moja leo. Kwa hiyo, sisi Rukwa tunafikiri kwamba, pamoja na kufikiria zana za kisasa, lakini sisi tunadhani mkombozi wa kweli kilimo cha kutumia maksai, yaani ng'ombe na plao. Kwa sababu plao kwa Rukwa unaweza ukatumia plao na maksai kulimia, ukapandia, ukapiga *harrow* na ukapalilia vilevile. Pia ukiwa na mkokoteni unaweza ukakusaidia kupeleka mbolea shambani, unakusaidia vilevile kubebea mazao shambani kurudisha nyumbani.

Sasa sisi tulivyokuwa tumependekeza wakati ule, tulichagua wakulima awamu ya kwanza, tulipendekeza watu 3,000 na tukawa tumependekeza kwa kiwango cha chini kabisa kila mkulima awe na hekta mbili. Tukawa tumependekeza kwamba, kwa kila mkulima apewe aina tatu, kwanza pembejeo halafu la pili anapewa mkopo kwa ajili ya zana, yaani *pair* moja au mbili za ng'ombe wa kulimia na jembe *pair* moja. Jembe moja unaweza ukalitumia hata kwa zaidi ya *pair* mbili za maksai wa kulimia.

Mpango wote tulipoutengeneza ulikuwa unafika shilingi bilioni tatu na uzalishaji wake umeonekana kama ni mkubwa sana. Kwa hiyo, sisi tulipopeleka maombi haya Benki, *NMB* walipopeleka mapendekezo haya Wizara ya Fedha, walituandikia barua rasmi ya kusema mpango huu umekubaliwa na wakaandika barua ya kuwadhamini wakulima wa Mkoa wa Rukwa. Tukianzia na jimbo la Kwela kama mfano wa kuanzia. Sasa basi mwaka juzi baada ya uchaguzi Serikali sisi tuliuwakili ule mpango na wakasema mpango huu ungefaa utumike kwa nchi nzima.

Sasa hii *approach* ya sasa ambayo ni mikopo ya sasa, sisi kule Rukwa tumeona kwamba kwa kweli ile tuliyoleta mwanzo ambayo Serikali muliikubali na Wizara ya Hazina mkatudhamini NMB mimi napendekeza sisi Rukwa ndiyo tuendelee kuitumia. Hii ya sasa haimsaidii mkulima na utaratibu tuliopendekeza sisi hatukuwa tunataka watu wapewe pesa. Tulikuwa tumependekeza watu watatu kwanza mkulima, pili Benki ya *NMB* na tatu mtu anayeweka pembejeo; majembe au zana. Kwa hiyo, mkulima akipewa mkopo yeye hapewi fedha. Yule *stockist* atampa mbolea na zana za kufanyia kazi. Akivuna atalipa kwenye benki yake wakate deni. Hii mimi nimeona nchi nyingi sana, imefanikiwa sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi napendekeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwa kwenye rekodi hizo mnajua jambo hili, *NMB* walikwisha kubali lakini baada ya kuingia huu mpango mpya, imeonekana kana kwamba ule haufai. Sisi ule tunaona unafaa kwa sababu umeandalia watu na watu wamejiandaa. Kwa hiyo, mimi napendekeza na naomba Wizara ya Fedha, mtukubalie turudi kwenye mpango ambao sisi

tulikuwa tumewasilisha na wananchi wanadhani hiyo ingekuwa sahihi kwa sababu hii ya sasa sisi tunaona kama ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kule Rukwa hakuna hata mkulima mmoja katika huu mpango mpya amepewa mkopo. Wanaopewa ni wachuuzi wanaonunua mahindi, wanaonunua alizeti, ndiyo wanaopewa wanaitwa wajasiriamali. Sasa tunakopesha wachuuzi, hatusaidii wazalishamali, unaona na utaona kama nilivyosema hata katika hotuba yangu iliyotangulia, nilisema hivi, mkombozi wa kweli ni kuongeza uzalishaji mali. Wanaofanya biashara Tanzania ni wengi kuliko wanaozalisha. Hii ndiyo unachelewesha nchi kupata maendeleo. Kwa hiyo, mimi naomba, nimeona siwezi kurudi jimboni bila kulisema jambo hili maana hii ndiyo *agenda* ambayo Wananchi wa Mkoa wa Rukwa wanasubiri. Nitafurahi sana kama Serikali itanipa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni la msingi nilishalizungumza jana na bahati nzuri nilikwishazungumza na wewe Mheshimiwa Waziri na nikakupa maandishi, sina haja ya kulisema, kwa sababu Serikali mnajiandaa mtatoa maelezo na mimi nitafarijika na maelezo yatakayotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo nasema nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kitu gani ambacho tutafaidi, sisi hatukijui? Asante kwa kunipa muda. Sasa nitampa nafasi Mheshimiwa John P. Lwanji na Mheshimiwa John M. Cheyo ajiandae.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika Wizara hii. Awali ya yote, ningependa kutoa salamu zangu za rambirambi kwa familia ya Mzee Fundikira. Sisi tuko jirani kabisa na Tabora, tumesikitishwa sana na hicho kifo. Pia ningependa kutoa pole zangu kwa Mheshimiwa John P. Magufuli, kwa kufiwa na mzazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kutoa pole kwa Wananchi wa Kitaraka kwa kufiwa na mwenzao Miraji Hassan. Juzi tarehe 7 tumezika kichwa kwa sababu huyu mtu ameliwa na simba. Ametoka Itigi na pikipiki katikati ya Itigi na Kitaraka alivamiwa na simba akaliwa kiwiliwili chote tukazika kichwa. Hali kadhalika, nitoe pole kwa Mbyaji, ambaye mapema mwaka huu naye alikuwa mhanga wa wanyama wakali. Simba walimla huyu mama ametoka alfariji kwa ajili ya shughuli zake za shamba akaliwa, tukazika kichwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingekuwa na sababu ya kutaja sababu ya vifo vya hawa watu, lakini nakumbuka tarehe 25 nilii-*caution* Serikali, japokuwa sikupata majibu kwamba sisi wenzetu ambao tupo mipakani tunachangia sana katika pato la taifa hili na juzi tuliipongeza Serikali, mimi mmojawapo niliyeunga mkono sana walipokuja na hoja ya kupandisha hizo *rates* za uwindaji. Napenda kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii, kwa jinsi walivyopanga na tunahitaji kuvuna kutoka huko. Nchi nyingi Shelisheli na nchi nyingine, zimetajirika kwa sababu ya utalii na uwindaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninachosisitiza ni kwamba, sambamba na hilo *what is parramount?* Kitu muhimu zaidi ni masuala ya maisha ya binadamu. Sisi sote hapa tunawawakilisha binadamu. Mwenyezi Mungu, alipoumba dunia hii alianza kwanza baada ya kuumba dunia akaumba binadamu, wanyama wakafuatia. Wanyama wakakabidhiwa kwa binadamu kwamba ni rasilimali yake. Sasa tusije tukawa na hisia kwetu kwamba, wanyama katika kutafuta hayo mapato ni bora zaidi kuliko binadamu. Mipaka ya *game reserves* mimi nina Muhesa, nina Rungwa na nina Kizigo. Mipaka imesogezwa mpaka vijijini, sasa tunaathirika sana, ningeliomba Serikali iliangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipotoa *concern* yangu hii nilizuiliwa Serikali isinijibu. Wakati tunakupongeza wewe kwa jinsi unavyotuelekeza hapa Bungeni na Mheshimiwa Spika, kwa umahiri wenu na kwa uzoefu wenu, mimi nilisikitika sana jioni hiyo ya tarehe 25 wakati natoa *concern* yangu ya watu wangu kuliwa na simba, mifugo yao kila siku wastani wa ng'ombe wawili, watatu, hupotea kila wiki ni wastani wa ng'ombe 52 kwa mwaka katika maeneo yote yale. Juzi tulikwenda pale tukaambiwa ng'ombe 144 walikufa mwaka jana tu katika vitongoji viwili kwa sababu ya kuliwa na simba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama watu na mali zao hatuwezi tukajali, ndiyo hapo. Nisikitika sana nilipozuiliwa tena na kufedheheshwa kwamba hili swali limeshaulizwa. Hata ukiangalia katika *Hansard,* hakuna mtu aliyezungumza habari za nyamaume hapa, simba mla watu wala habari za fidia ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nina *register concern* yangu kwamba, sikutendewa haki kabisa na Meza na ninaomba hili liangaliwe ili tusije tukawa waoga katika kutoa matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Katiba inaruhusu tupate Spika kutoka hata nje ya Bunge hili, lakini kwa kutambua umuhimu sisi tulichagua Spika na Wasaidizi wake kutoka miongoni mwa wenzetu. Kwa hiyo, tulitarajia kwamba wenzetu hawatakuwa kikwazo, Mawaziri wapewe nafasi ya kujibu maswali yetu na ninavyofahamu, Mawaziri wa sasa ni waadilifu kabisa. Wanapenda kabisa kujibu hoja za Wabunge. Sasa ningeliomba sana ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge - Kuhusu utaratibu. Hili suala unalolieleza siyo sehemu ya mjadala huu? Upo utaratibu mzuri kabisa wa ku-*register concern* yako na ikashughulikiwa. Hapa siyo mahali pake kabisa. Kwa hiyo, utakuta hawakusikii wala hawakuelewi. Kwa hiyo, tafuta muda mzuri kwa mujibu wa kanuni zetu, *register your concern.* Huo ndiyo utaratibu. Sasa zungumzia Wizara ya Fedha.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Asante Mheshimiwa Naibu Spika. Mchango wangu mwingine ningesema kwamba, sasa hivi ni miaka 30 toka Jumuiya ya Afrika Mashariki ivunjike. Kwa bahati mbaya mpaka leo tuna matatizo ya wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambao walipaswa kulipwa haki zao. Itigi tuna karakana kubwa iliyoachwa pale ya *East African Road Services* na hiyo karakana iliacha watu wengi waliokuwa *laid off* na kweli mpaka leo wanadai mafao yao.

Ninashukuru kila ninapokwenda mara nyingi Wizarani pale wawili, watatu, wanasaidiwa. Lakini mimi nadhani tunge-*close chapter* hii, watu hawa ni wazee wa miaka 70 - 80. Watu hawa wanatoka wanakwenda *Railway Station* wanalala pale, wanakwenda kufuatilia mafao yao wengi wanarudi mikono mitupu. Ningeliomba sana hili suala liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kitu kingine ambacho ningeliomba nizungumzie ni kuhusu Benki ya *NBC* Manyoni. Manyoni tuna matatizo ya mikopo. Nimekaa Iringa nimefananisha na sehemu nyingine, sijawahi kuona matatizo hayo. Kwa sababu wale watu wanaoomba mikopo hasa hii midogo midogo, masharti yao ni magumu. Lakini sehemu nyingine kama nilivyoona Iringa, vitu kama hati ya nyumba, *collaterals* hizi kwa biashara ndogo ndogo, hiyo siyo hoja. Watu *collaterals* zao ni *personal effects* na vitu vingine. Kwa sababu ni biashara ndogo ndogo na maduka yao na *groceries* zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ningeliomba tuangalie kuna nini *NBC* na hiyo *radius* ya huduma za benki inakuwaje? Unapoambiwa kwamba unakwenda pale bwana kilomita 20 au sijui 25 sisi hatuwezi kufika. Sasa wanapataje huduma hao watu? Ningeliomba sana hii mikopo iweze kuangalia hawa watu, hata kabla hii ya shilingi bilioni moja, mimi nazungumzia hii mikopo midogo midogo ya biashara, watu wajikwamue waweze kuendelea. Mimi ningeliomba benki pale waangalie kuna tatizo gani hasa huu urasimu. Tatizo labda la *radius* inawezekana wanasingizia usafiri. Sasa kwa nini Benki ya Manyoni haina gari? Wilaya hiyo ni kubwa ina kilomita za mraba 28,000, 29,000, unahudumiaje hii Wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanatoka Rungwa, wanakuja kuchukua wiki pale Manyon, kwa kitu ambacho wangeweza wakaenda wakamaliza tu. Kama ni fomu na mambo mengine kwenda kuangalia biashara zao, ningeliomba sana Wizara ione uwezekano wa kuwapatia gari pale Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine mimi ningeliomba kwamba, watazame eneo hilo. *CRDB* walikuja Itigi wakakagua. Walipokagua pale Itigi wakakuta kwamba, *it is a potential area* kufungua benki lakini imechukua muda. Hii Itigi pamoja na *corridor* ya kwenda Mgandu, asilimia kubwa karibu asilimia 50 ya mapato ya mkoa huo, yanatoka eneo hili. Mbao ziko nyingi na biashara nyingi, tumbaku. Sasa watu hawa huhatarisha maisha yao sana, kusafiri kila mara kwenda benki na kurudi. Sasa naomba nadhani wakati umefika, tuweze kupata msaada huo, tunawaomba kwa upendo tu na kwa heshima kwamba, muda wetu umefika na sisi kuweza kupata huduma hii. Watakaohudumiwa ni wengi tu mbali na wananchi, kuna mashule, kuna mahospitali. Wafanyakazi hawa wanapata tabu, muda mwingi wanapoteza badala ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani baada ya kusema hivyo, basi nashukuru kwa kunipa nafasi hii na nawatakia kila la heri. Wizara hii imekaa vizuri watu wenyewe ni waadilifu ni wataratibu, wanasikia, basi watusaidie ili tusonge mbele. Nashukuru sana kwa nafasi hii, asante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Asante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Awali ya yote, kwa niaba ya familia yangu na wapiga kura wangu, nataka kutoa salam za rambirambi kwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa kufiwa na baba yake. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Pia namkumbuka Mzee wetu, Chifu Abdallah Fundikira, namwomba Mungu amweke mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, kwanza nataka kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa kazi nzuri aliyoifanya leo asubuhi na baadhi ya mambo ambayo nitayarejea, ambayo kidogo itakuwa ni kujaribu kuweka msisitizo tu. Lakini natumaini Mheshimiwa Waziri, atayachukulia haya mambo ambayo yamezungumzwa leo kama njia ya kujenga Wizara hiyo na siyo mambo ya malumbano ya kisiasa. *(Makofi)*

Baada ya kusema utangulizi huo, nataka kusema kwamba, Wizara hii ya Fedha ndiyo pia Wizara ambayo inatuletea bajeti hapa Bungeni. Ukiangalia vitabu vyote vile ambavyo tunapewa hapa Bungeni, mimi nafikiri kuna haja sasa ya kujaribu kutafuta njia ya kuboresha hivi vitabu. Tangu nimeingia Bungeni 1996, Kitabu ni wa aina ile ile na mambo yale yale, kasma hizo hizo; hivi watu wabunifu ambao wanaweza wakatengeneza utaratibu ulio mzuri zaidi wameenda wapi katika Wizara hii ya Fedha? Ndani yake kuna mambo ambayo kusema kweli yanatia shaka sana juu ya bajeti nzima. Unapoangalia bajeti tulikuwa tunafanya juzi ukaguzi, unagundua kuwa mahali ambapo imeandikwa 26011, vitu ambavyo havijatambuliwa huko juu, inafika mpaka shilling bilioni 425, hii ni karibu asilimia 15 ya bajeti yote. Sasa kama huwezi ukapangalia shilingi bilioni 425, ambayo karibu Wizara ndogo ndogo kumi, hii ina maana gani juu ya ufanisi wa upangaji wa bajeti ya kwetu? Kwa hiyo, kuna haja ya Wizara hii kuliangalia upya ni jinsi gani wanaweza wakaboresha namna wanavyotuletea vitabu hivi vya bajeti ili sisi Wabunge tuweze tukatoa uamuzi ulio sahihi na tuweze kuona fedha kweli zinatumiwa kwa namna. *(Makofi)*

Jambo la pili ambalo pia hili linahusu Bunge, kwa muda wa karibu siku 35 leo tumezungumzia juu ya matumizi tu, lakini ni mara chache sana tunazungumzia juu ya mapato na kitabu hiki cha kwanza wala hatukiangalii. Sasa hii ni bajeti ya namna gani ambayo ni mapato na matumizi, hakuna hata siku moja tumefungua kasma namba ngapi inakubaliwa hapana wala hatusemi, hilo hatuiangalii kabisa kitabu *number one.* Kwa hiyo, inavyoonekana ni kwamba, tunakubali bajeti ambayo ni ya upande mmoja, hata ukiangalia *Appropriation Bill, of course* kama vile neno la Kiingereza linavyosema ni kuomba kutumia ni la matumizi tu, lakini haioneshi kwamba, hizi fedha zinazoombwa zitumiwe zinatoka wapi? Mimi nina hakika kuwa Wizara hii inaweza ikatusaidia sana kama ikianza kuweka ubunifu zaidi na pia Bunge ningeomba tuanze ku-*demand*, tuombe tujue hizi fedha zote tunazoambiwa tutapata ni kweli tutapata au vipi, yaani tuangalie na upande mwingine wa shilingi wa mapato kuliko kila siku ile kuzungumzia juu ya matumizi tu. *(Makofi)*

Lakini si hivyo tu, msemaji mkuu wa leo ametuonesha jinsi gani Serikali inapoteza fedha kwa kutotimiza ahadi zake na Wafadhili tumeambiwa katika hotuba ya

leo kuwa katika mradi ambao ulikuwa wa MKUKUTA, tuliahidiwa milioni 200 *dollars*, lakini ikabidi zipunguzwe mpaka zikafika bilioni 190. Kwa hiyo, tukapoteza kumi, kwa sababu tu Serikali nzima haikuweza kujikusanya ikahakikisha kwamba, yale yanayoahidiwa yanafikiwa kwa wakati. Kwanza, sisi ndiyo tunaowaahidi, sisi ndiyo tunaokwenda ku-*negotiate* na wafadhili, sasa kama kuna *time table* ambayo tunaiona sisi haifai, kwa nini tunaikubali mpaka baadaye tena tuje tuanze kupoteza bilioni kumi? Leo hii Msemaji Mkuu wa Serikali, amezungumzia juu ya *Audit A*ct, hiyo pia Mheshimiwa Waziri, ambaye kitengo chake cha *External Finance* ndiyo kinakubaliana na wafadhili juu ya *prior action* au masharti. Mojawapo ya masharti ambayo yatakuwa humo ambayo yanayohusu MKUKUTA, ambayo yanahusu *Public Finance Management,* yote yale pia yamekusanywa na kuwepo kwa *Public AuditAact.*

Sasa kama wanajua hivyo ni kwa nini mpaka hivi sasa tuko karibu mwezi wa Oktoba na *review* itakuja mwezi wa Oktoba mpaka leo hatujaletewa *Public Audit Act* au Sheria ya Ukaguzi, mambo haya wanayojua na wanajua *consequences* zake wanajua wasipofanya kitafanyika hiki. Sasa kama ni hivyo, mimi sioni kuna kitu gani katika Wizara hii, ambayo ndiyo Wizara mtambuka kwa mambo yote ya kifedha, inayoshindwa kuleta masharti yote ambayo yanahitajiwa na wafadhili kuhakikisha kwamba yanatimizwa. Sisi tunafikiri kwa upande wa *Public Audit Act,* jambo hili lifanyike mara moja ili tuhakikishe kuwa hatupotezi pesa, lakini zaidi ya hayo tunaimarisha uwajibikaji na hili jambo la uwajibikaji, mimi nafikiri kama kuna mwaka jambo hili limetamkwa kwa ufanisi kabisa na Mkuu wa Serikali ni mwaka huu. Rais ameweza kutumia fedha ya Serikali, kuwaita Maafisa Wahasibu Wakuu wote wa nchi nzima na somo lilikuwa uwajibikaji. Rais ameweza kufanya hata Mkutano wa Mawaziri, *special* kwa ajili ya *Report* ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali, somo pale ilikuwa uwajibikaji.

Tumefanya kongamano kubwa sana mwaka huu, somo ni uwajibikaji. Sasa kama Mkuu wa Nchi hii anazungumzia umuhimu wa uwajibikaji, sioni kwa nini tuwe na jambo ambalo linatusumbua katika kuhakikishia kwamba, tumeimarisha uwajibikaji kwa kuhakikisha kuwa, tuna sheria ya udhibiti na ukaguzi. Si hivyo tu, jambo hili litaleteleza sasa hivi katika *supreme audits* zote, yaani Wakaguzi wote wa Serikali wana utamaduni wa kuweza kupeana madaraja. Leo hii daraja la *National Audit*, ofisi yetu ni daraja la mwisho, yaani *rank one,* sasa ikiendelea na *rank one* ndiyo kusema kwamba, watu watakuwa wanaiona ofisi hii ni ya mashaka mashaka. Mwaka 2009 kumekuwa na mkutano, kutakuwa na ukaguzi mwingine na ni vizuri tukaweza kupanda tukafika hata daraja la tatu, lakini yote haya yanategemea kwamba pawepo na *National Audit Office*, ni kitu gani ambacho kinafanya Wizara hii ambayo ndiyo yenye jukumu la kutuletea Miswada hii, kuvuta miguu wasifike huko. Tungependa maelezo.

Lakini sio hivyo tu, sisi tungependa hii ofisi iimarishwe, *National Audit Office* kwa sababu sasa hivi hata ukiangalia ile bajeti kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani, waliomba shilingi bilioni 18 wamepewa shilingi bilioni kumi na nyingi ni za mishahara, lakini za kufanya shughuli zao za kawaida ni kama shilingi bilioni nane. Fedha za maendeleo, pamoja na Mheshimiwa Waziri, kusema ametoa shilingi bilioni 2.3, lakini ukweli ni kwamba, hizo shilingi bilioni 2.3 si za kujenga ofisi; shilingi bilioni 2.3 ni msaada kutoka Sweden, kwa ajili ya kuimarisha ofisi hiyo. Kwa hiyo, fedha za

kuweza kujenga ofisi hakuna. Kwa hiyo, mimi sioni kwa nini tunajua kuwa hii ndiyo roho, hii ndiyo kama vile *insurance company* ya kuhakikisha kuwa fedha zetu zinatumika vizuri, kwa nini hatuwekezi kule? Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri kuwa, Mheshimiwa Waziri, alichukulie hili jambo kwa uzito ambao tumeu-*present,* tulionesha ili kweli tuweze, Bunge la Novemba tupate *National Audit Office Act,* ambayo ndiyo itaweza kuhakikisha kuwa ofisi yetu inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiondoka hapo, nataka kuzungumzia jambo lingine dogo tu, kuhusu *reallocation.* Nimeangalia hapa, Bunge leo litaombwa ruhusa Waziri aweze ku-*reallocate* au kutoa fedha kupeleka fedha huku, ukiangalia takwimu ambazo zinazungumzwa hapa ni karibu shilingi bilioni 300 na zaidi. Mimi nashangaa na unaangalia mtu ameondoa fedha kwa mfano, za *TACAIDS*, za upande wa UKIMWI, shilingi bilioni 11, anaondoa fedha kwa ajili ya dawa shilingi bilioni nane anaziahamishia kwingine. Sasa sisi hapa tunakaa karibu miezi mitatu tunazungumza, tunatoa mate, tunashikana mkono, mwisho ni mtu mmoja tu anakaa kule peleka hii huku, hapa nitawaeleza Wabunge na baadaye tunaelezwa hapa hakuna lingine linalofanywa.

Mimi nafikiri lazima tuwe na bajeti ambayo iko *tight*, bajeti kweli ambayo kama tukikubaliana kwamba na haya yatafanyika, kweli tuone kwamba yatafanyika kuliko kuwa na bajeti ambayo inaonekana kama bajeti hewa na pia inaonekana sisi hapa tunafanya kazi ambayo sio stahili. Fedha shilingi bilioni 300 zinahamishwa na Wizara au na Waziri wa Fedha, kusema kweli ni fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nataka kusema kwamba, Wizara hii kusema kweli ni muhimu, Wizara hii ndiyo roho ya nchi hii na ni vizuri Mheshimiwa Waziri, akaiangalia hii Wizara. Mimi nafikiri kwamba, labda kuna sehemu nyingine watu wanakaa muda mrefu mno katika ofisi hii, kwa hiyo, inakuwa ubunifu wao unakuwa ni mchache, pia inafaa kuangalia ofisi hii katika vitengo mbalimbali viko imara kiasi gani; Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Idara ya *External Finance*, Idara ya Kudhibiti Fedha zinazokwenda katika sehemu mbalimbali kwa mfano, fedha zinazokwenda kwenye Halmashauri ikoje, ili kweli Wizara hii iweze kutupatia utaalamu na mfuatiliaji wa fedha ambazo zinaidhinishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo nilitaka kusema kwa leo asante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kuniruhusu niwe mzungumzaji wa mwisho, nadhani ni kwenye bajeti ya siku 35 kama kuna wengine basi mimi nitasema kama mzungumzaji wa mwisho.

Nianze na kumpa pole ndugu yangu, jirani yangu, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, amempoteza baba yake. Namwomba awe jasiri, mzee wetu ametangulia, ndiyo huwa tatizo nani atangulie, lakini na sisi tutafuata. Natoa pole kwa familia ya Chifu Abdallah Fundikira, alikuwa Mbunge mwenzetu kipindi kilichopita, alikuwa mzee

mashuhuri lakini ndiyo utaratibu wa Mwenyezi Mungu, tunamwombea Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amen.*

Kwa kuwa hii hotuba ya leo ni ya mwisho na ndiyo ya bajeti, napenda niseme kwamba, tumegawana fedha hapa na wapo ambao wamekabidhiwa majukumu, wenzetu Mawaziri, sasa wananchi wanatutegemea kuona zitafanyaje kazi na ningeomba Wizara hii iwe mfuatiliaji mkuu, kwa sababu ndiyo imekusanya imetupa.

Mimi nilikuwa nafuatilia sana, kila Wizara inapopata fedha wana-*react* namna gani, wana-*behave* vipi, sijui kama na ninyi wenzangu mlikuwa mnaangalia, Waziri na watu wake wana-*behave* vipi. Nilikuwa naangalia sana, nikafuatilia nikaona Wizara moja tu ndiyo ilinifurahisha, lakini wengine walikuwa wanamaliza, pata pole, tawanyika, wanaondoka. Wizara moja ilienda ikakaa *VETA*, wakawaambia viongozi wote ambao ni Watendaji Wakuu kaeni tumepewa fedha, sasa kinachofuata ni kutekeleza uharibifu, kitakachotokea kila mmoja atawajibika. Nitapenda niseme ni Wizara ya Elimu, walienda wakakaa wengine waliondoka, lakini wengine walichukua mizigo kwenda, sijui wameshagawa au vipi?

Sasa kwa tabia hiyo, mimi sikuipenda na nilikuwa nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, unafanya kazi nzuri pamoja na wenzako, lakini waambie wenzako kwamba, nawapa fedha, lakini kesho tutakuuliza wewe fedha tulizopewa zilikwenda wapi. Leo tumepewa fedha ndugu zangu tunaomba ziende kwa wananchi, kama ni Meneja wa *TANROAD* ikusudie kwenye barabara kule ilikokwenda, ndiyo tatizo tunalopata ni mabilioni mengi ya fedha, lakini utakuta hayafiki na ndiyo ugomvi tuliokuwa nao hapa. *(Makofi)*

Mimi nimekuwa nikisafiri Kenya, Uganda na Burundi, wanatupeleka Bunge lakini tatizo ambalo ninaliona, fedha yetu inashuka, sasa napenda kuelewa Wizara yetu ya Fedha ina mkakati gani, pamoja na watendaji wote, tatizo inashuka? Watanzania hatufanyi kazi, hatuzalishi mpaka Burundi inatuzidi, Uganda sasa hivi nafikiri tumebaki kidogo tu, *actually* ukienda na hela yako, hakuna anayeitaka hata *Bureau de Change* hawazitaki, kuna tatizo gani tunakunywa kahawa tu tatizo ni nini? Tujiulize hatuna viwanda sasa inabidi tufikirie, tutafute viwanda, tuanze kufikiria namna gani tuweze kuirekebisha fedha yetu, hatuwezi kuzungumza hapa tutakuja tutapitisha matrioni na matrioni lakini yakienda mtaani hayana thamani. Mimi naona ni hatari. *(Makofi)*

Juzi tu niliuliza swali la viwanda vya matunda, watu wakanijibu kirejareja, lakini kuna matunda hapo yanaweza yakazalisha *juice* zikatuletea fedha nyingi sana. Geita kuna mananasi ambayo nilisema ni *first class,* mtu akasema lakini hayalingani na machungwa ya wapi. Angalia ukiweka kwenye kiwanda kinaweza kikaingiza fedha, Kenya wanapata fedha kwa kutumia *juice,* Uganda wanatumia, Afrika ya Kusini, *juice apple* ya Afrika Kusini ina tofauti gani na *apple* ya Lushoto na mananasi ya Afrika ya Kusini yana tofauti gani na mananasi ya Geita, ambayo ni mazuri ukiweka lori ukitoa shilingi 5,000 lori linajaa kwa nini usiwawekee kiwanda?

Halafu vilevile hata umeme tunapopeleka, pelekeni mahali ambapo tunapata fedha, kuna maeneo ya machimbo kwa mfano, Wamgasa, Nyalugusu na Katoki, kuna wachimbaji wadogo, ukiwapa *assistance* hawa watu watatoa dhahabu jicho letu liwe pale. Tuna dhahabu lakini fedha yetu inashuka. Mimi nilikuwa kwenye Tume ya Madini na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anafahamu, tulienda Botswana, Rais wa kule jicho lake asubuhi na jioni liko kwenye dhahabu, anafanya *auditing* mara mbili kwa siku, kuliko kwenye almasi. Sasa na sisi Rais jicho lake linatakiwa liwe pale na ninaposema Rais, maana yake Waziri wa Fedha na Watendaji wake. Mnawadhibiti vipi hao watu kwa sababu tunaonekana maskini lakini vitu tunavyo. Sasa nilikuwa nasema jamani naomba sana, tunakokwenda ni kubaya, fedha yetu inakwisha. Nilikuwa naomba sana Wizara hii baada ya leo kufikia hatua ya mwisho, iweke mikakati ya kuhakikisha kwamba, hata fedha hizo wanaosema zimeibiwa zimepotea labda wanasema kuna matumizi mabaya ya Benki Kuu. Serikali iweke jicho kubwa zaidi pale ingawa wanasema *okay,* sijui Wabunge? Tume ya Bunge, tuna kazi nyingi sana, mimi nasema Serikali ndiyo ikalifuatilie hili, iliangalie hilo la Benki Kuu, kama kweli kuna kiwingu pale, ituletee ripoti iende ikaangalie kuna tatizo gani. *(Makofi)*

Taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu, tunaanza kuziona, kwa kweli zinaumiza sana, inatia aibu safari nyingine tena Rais au Waziri Mkuu, aanze kuita Wakuu wa Mikoa, aanze kuita Wakurugenzi awapeleke sijui Ubungo Plaza, kuanza kuwahutubia. Tunaomba hiyo hali isitokee tena, watendaji kule kule kama ni Mkuu wa Mkoa, waanze kuangaliana huku, Mkuu wa Wilaya amekuwa na huruma mno. Badala ya kuita afadhali aseme sasa nataka mwingine ndiyo aingie pale, kuita maana yake ninyi mpaka wale Watendaji Wakuu walikuwa hawaangali kule. Mkuu wa Mkoa angalia huku, kwa hiyo, nilikuwa naomba mgawanyo wetu wa fedha hebu tusimpe kazi, mpaka sasa tunataka awe mweusi, alikuwa mweupe Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, sasa atabadilika atakuwa mweusi kwa sababu ya kuanza mara afanye kazi za *auditing.*

Mimi nadhani kazi anaifanya vizuri, lakini tusimwongezee tumsaidie kule sisi kama watendaji hasa wale waliopewa dhamana, hakikisha unalinda dhamana yako kule uliko, tusingependa tena vikao vianze sijui Mkaguzi Mkuu amepitia mahesabu kabla, anza kuliangalia. Nilianza kwa kusema nilikuwa naangalia *behaviour* ya kila Wizara inapopata fedha, ina-*behave* namna gani na kuangalia ni vipi wana-*react* kwenye maagizo ya Serikali, maagizo ya Waziri Mkuu, maagizo ya Rais, maagizo ya Wakuu. Wote wanaoliona hili lakini ni wachache sana walikuwa na hiyo hali, kwa hiyo, nikaona bado haijaingia, ndiyo maana niliomba niseme ndugu zangu tumegawana na mimi nashukuru nimepewa hela yangu ya barabara, yule aliye kwenye eneo langu atapata tabu na nitaomba Waziri wa Fedha naye, atupe fedha atakazotupa za MMES atuambie ni ngapi wa TAMISEMI ameshatupa za barabara, za maji hatujapewa. Waziri wa Maji tunaomba atupe twende tunafahamu ni kiasi gani tumepewa na watu watazipokea hizo fedha. Lakini tunaomba utumiaji wa fedha tulizopewa, twende tukazitumie vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninawatakia kila la heri. Tumepewa mzigo kila mmoja aende na chake tulichokigawana hapa. Naomba Wizara hii ianze kuwashauri hizi Wizara nyingine, madini yalishaenda inaelekeza umeme wapi, kuna eneo kama Katoro, pale kuna *centre* kubwa sana ambayo

inahitaji umeme na wanaweza wakazalisaha saa 28, ishauri vilevile hata Wizara ya Mambo ya Ndani, unakuta sisi wakati magari yanasimama saa 12 au saa tatu, wenzetu Kenya mabasi yanatembea eti mnaogopa majambazi, Kenya hakuna majambazi?

Tunalala kuongeza *population*, wenzetu wanafanya biashara *centre* kama Katolo ukiwawekea umeme ni *24 hours* wanafanya kazi, watu wanafunga maduka kwenda kunywa pombe badala ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mimi nilikuwa naomba hebu tuangalie sana wapi tuna matatizo, basi utakuta mtu wanamfukuza tena wanawafukuza *actually* hawazui, *infact* tufanye kazi saa 24, unakuta watu wanakunywa kahawa. Nenda Kenya Ukisi, ukute kama kuna mtu saa nne anakunywa kahawa mpaka saa 12. Lakini sisi kuna mahali, tajiri mmoja amewawekea na TV watu wanaangali TV wanakunywa kahawa, watu wanazalisha utafikiri msiba, tufanye kazi bwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu yalikuwa katika masuala matatu, moja lilikuwa ni suala la usimamizi wa bajeti, lililozungumzwa kwenye hotuba ya Waziri, la pili lilikuwa kwenye suala *joint system strategy* na pesa za wahisani na la tatu lilikuwa kwenye huduma za kibenki. Nitajaribu kusema haraka haraka ili nisishindwe kumaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi leo tunajadili uwezo wa utekelezaji wa majukumu haya ambayo Wizara inayo, ambayo imepewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, masuala ya sera tulishayazungumza huko nyuma.

La kwanza kabisa, mimi ninaloomba kuzungumzia ni suala la usimamizi wa bajeti na vitengo viwili vinavyozungumziwa, *expenditure tracking unit* na *technical audit unit*. Tulipata nafasi ya kuyazungumza kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi na tatizo langu kimsingi ni kwa sababu tunawapa majukumu kulingana na hii nadharia nzima ya *decentralization by evoluation,* ambayo ni nadharia ya kutoa matumizi makubwa kwenye Serikali Kuu kwenda kwenye Serikali za Mitaa. Kimsingi ni nadharia nzuri, ni *foreign* lakini *its okay.* Nadharia ni nzuri, haina matatizo yoyote, lakini *applicability* yake kwenye uchumi wa Tanzania. Mimi nimewahi kuongea na Waziri na wataalamu wake, ninarudia kulisema hapa tena kwamba, jamani chonde chonde, hizi pesa tunazopeleka huko, sisi ni Wabunge wa majimbo tunawajua, ukitangaza pesa zinakwenda huko, watu wanaanza kusherehekea kabla hata hawajajua wanapewa kiasi gani. Ile hali tu ya wataalamu kule kujua wanaletewa pesa zaidi, inawapa nuru zaidi ya kutamani ile hela.

Sasa nakuomba sasa Mheshimiwa Waziri, suala la *Expenditure Tracking Unit* na *Technical Audit Unit,* ninalisema kila siku tusiogope ku-*spend in order to save*, kama ikibidi tutumie hela za ziada kwa ajili ya kupata wataalam, hili nalisema na Waziri

amelizungumzia, kuna jambo mle ndani linaitwa *data,* benki ambayo watakuwa wanashirikiana na ofisi ya TAMISEMI na Waziri Mkuu, ku-*monitor* utekelezaji wa miradi hiyo, ndiyo tatizo letu kubwa sana sana kwenye Halmashauri. *They are not ready* kupokea pesa hizi ambazo tunatumia, licha ya nia njema ya Serikali Kuu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, afanye *capacity building* ya hali ya juu kabisa, lazima tutapoteza hela wajanja watakuwepo lakini *percentage* ipungue.

Lingine ni hili suala *Joint Assistance Strategy*, Msemaji wa Upinzani amelizungumza akasema kwamba, mwaka jana tulipewa *Euro* nadhani milioni 200 na mwaka huu tunapewa *Euro* milioni 700, akamwonya Waziri asinunue ndege ambayo inatua kwenye viwanja viwili badala ya vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndege ya Rais imewakosea nini, maana yake imekuwa nongwa, ile ndege ni *Gau Stream,* imenunuliwa kwa dola milioni 45, *now in the market is wealth 65 million dollars*, sasa *if anything* basi tukubaliane iuzwe halafu inunuliwe ndege nyingine mnayoshauri ninyi. Lakini mnachozungumza hapa, mnasema hiyo ndege iondoke halafu iweje na kwamba, Rais atembelee na ndege gani, hiyo anayotembelea F 28 ina miaka 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo *let us go to issue,* badala yake nimeona kuna hoja imezungumzwa ya kwamba, hizo milioni 700 halafu mwaka kesho wahisani watatoa bilioni moja. Kwa hiyo, hizo pesa za wahisani zinatoka kwa sababu ya *transfer* waliyokuwa nayo na uongozi ule wa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Akienda Mheshimiwa Mama Zakia H. Meghji na wasaidizi wake wale wawili na Ndugu Mgonja, wakienda nje wanazungumza wanaonekana *these people are trust wealth,* ndiyo maana tunapewa hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima tuangalie hilo kwamba, hiyo misaada yenyewe tunayopata kwa wahisani ni kwa sababu ya imani waliyokuwa nayo kwa Serikali hii ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Kama wakiongeza *one billion* ni kwa sababu ya imani zaidi kwa Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, sasa tusiwe tunauma na kupuliza hapo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, niseme namtakia heri mama yangu, Mheshimiwa Zakia H. Meghji, mkienda huko tena mpate bilioni moja mwaka dola zaidi ya hizi na mnatapa ishara kwa uongozi wenu mzuri wa Wizara hii ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni huduma za kibenki, kwenye *page* namba kumi tumezungumzia usimamizi wa masuala haya. Naomba niliseme kwa Waziri wa Fedha, tumewakabidhi Benki Kuu, majukumu ambayo kusema kweli Benki Kuu *technically* wanaweza wakayafanya. Lakini hawana uwezo au *political responsibility* ya kuyafanya, tunawakabidhi majukumu mawili tu niseme katika hayo yalizungumzwa kwenye hotuba, *Credit Guarantee Schemes* na *whole sale bank* kwa *SACCOS* hizi ambazo baadaye tunataka ziwe *Community Banking*. Huko porini kama tusipopeleka

mabenki, watu wataendelea kuweka pesa mchagoni na ile *concept* ya ku-*save in a social quantification* haitofikiwa, maana yake ni kwamba, watu wa Mkuranga, Namtumbo, Ifakara na Kidatu huko hawatofikiwa na huduma za kibenki kama Wizara ya Fedha isipofanya mikakati ya makusudi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano hii ya mikakati ya makusudi ya kupeleka benki kwenye maeneo ipo. Kwa sababu *banking* ni *culture, the first thing you do about banking* kuwa na *culture* ya ku-*save*, tutabaki na watu ambao kazi yao pesa ikifika ni ulanzi, matokeo yake Mheshimiwa Naibu Spika, nimekukumbusha nyumbani, kwa wajomba zangu, lakini ndiyo ilivyo. Sasa lazima tuwe na *culture* ya ku-*save* na *culture* ya ku-*save* inatokana na sehemu ya kwenda kuwekeza ile akiba ndogo. Sasa Benki Kuu hawana *responsibility* hiyo kwa sababu *they are not politically responsible* na wala hawana ndoto hiyo na watatukubalia hapa kwa sababu miswada yao inapitia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi namwomba sana Mheshimiwa Waziri akae na watu wa Benki Kuu kwa makusudi, tuangalie namna tutakavyozipa nguvu zaidi benki hizi za asilia. *TIB,* Benki ya Posta, Twiga Benki ni rahisi, mimi kama Mswahili wa Mkuranga kwenda Twiga Benki, *NMB* hizi benki zetu za Kiswahili, ukienda *Standard Chartered,* hata kukutazama hawakutazami, labda upige *suite* nzito na kadhalika.

asa lazima tuangalie namna Wizara ya Fedha, itakavyofanya mikakati ya makusudi kabisa, *policy oriented* ya kuzisaidia benki hizi za Kiswahili ili nazo ziende huko kwa Waswahili ndani ziweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni suala *TIB* kama benki ya kusaidia maendeleo kwa kuwekeza, tayari kuna mkakati wa *PPF, NSSF, PSPF,* wawaongezee na Benki Kuu, hao watu wanahitaji shilingi bilioni 25, hizo fedha zipo katika mfumo wa benki hii na zikipatikana hizo, hawa watakopeshwa. Namna ya kumkopesha mkulima matrekta na kadhalika, *that is the way for us*. Malaysia wamefanya, hatuwezi kumtegemea *Standard Chartered*, *Stanbic* mimi mwenyewe ni Mjumbe wa Bodi ya *NBC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naomba wazingatie niliyoyasema nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru kwa kutumia vizuri muda mfupi uliopewa. Sasa Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tukiingia mchana watoa hoja wataanza kujibu, wakijibu tutaingia Kamati ya Matumizi halafu tukipitisha tutaingia kwenye *Appropriation Bill,* kama muda utaruhusu tungefurahi sana kama Waziri wa Fedha ataweza kusoma ile *Finance Bill* ili ijadiliwe siku ya Jumatatu. Baada ya kusema hivyo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Kwanza, natoa pongezi kwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji, Naibu Mawaziri wote, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mheshimiwa Mustapha Mkulo, Katibu Mkuu na watalaamu wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kwamba, kuna wakulima wa Vyama vya Ushirika wa Bukumbi, Kashishi, Kahama na Bukombe, ambao ni wakulima wa zao la pamba na ambao waliuza mazao yao mwaka 2004/2005 na hawajalipwa mpaka sasa na Serikali ilisema kwamba ingelipa ili kuwaondolea kero wakulima hao ambao walikopwa na Chama cha Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuongelea suala la sarafu ambapo hivi sasa *Casino* nyingi hutumia shilingi mia moja kwa ajili ya kuchezeshea na matokeo yake husababisha shilingi hiyo kuchunika na hatimaye hukataliwa katika soko. Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi kuzuia fedha/sarafu hiyo isitumike?

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Wizara kwa Bajeti na majumuisho ya hotuba. Mchango wangu ni juu ya usimamizi wa fedha hasa za barabara chini ya *TANROADS* na makandarasi wanaotafutwa na hao Ndugu wa *TANROADS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana *TANROADS* wawaweke makandarasi kwenye *site* za barabara walizopewa. Utakuta kwa mfano, katika Wilaya yangu barabara inayohudumiwa na makandarasi wa Ifakara Taweta, mkandarasi wake anakaa Morogoro. Barabara inaanza na shimo dogo mpaka linakuwa handaki lakini wanalipwa fedha za ukandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *TANROADS* isimamiwe kwa ukaribu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge kuchangia, tulishafunga mjadala sasa tunaanza kwa watoa hoja, wako Naibu Mawaziri wawili; ataanza Naibu Waziri mmojawapo na huyu tutampa dakika 15 za kuchangia, halafu nyingine Mheshimiwa Waziri atakuwa anajua saa moja atagawana na Naibu Waziri aliyebakia.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Waziri, awali ya yote, natanguliza kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge na hoja ya mwanzo ni kuhusu udhibiti wa manunuzi ya vifaa vya umma. Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004, imeanzisha utaratibu ambao unatoa fursa kwa kila taasisi ya umma, kufanya na kuwajibika. Manunuzi yake yatakayofanyika lakini ili kuhakikisha kwamba, taratibu zinafuatwa, ikaanzisha *PPRA* kwa lengo la kutoa mwongozo, kujenga uwezo na kusimamia na kudhibiti shughuli za manunuzi ya taasisi za umma. *PPRA* ilichukua nafasi iliyokuwa nayo *Central Tender*

*Board*, utaratibu huu unatumika katika nchi zote za Afrika Mashariki na siyo kweli kuwa unatumika hapa Tanzania pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa vile ni lengo la sheria kutoa nafasi kwa wazabuni wote, inasisitiza kuwa zabuni zitangazwe kwenye vyombo vya habari, hata sheria na kanuni zimewekwa wazi njia nyingine zinazoweza kutumika kuitisha zabuni bila matangazo kwenye magezeti kwa zabuni zenye thamani ndogo. Mamlaka yanayoelimishwa kama taasisi za umma kuhusu njia hizi mbalimbali kwa lengo la kuwawezesha kupunguza gharama za matangazo, vilevile mamlaka imeanzisha tovuti na iko katika hatua za mwisho, kuanzisha jarida litakalotumika kutangaza zabuni za taasisi za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, *PPRA* ikiwa ni moja ya kazi zake, inaendelea kufanya tathmini ya utaratibu utakaotumika kununua bidhaa na huduma zitakazotumiwa na taasisi nyingi za umma, yaani kama *new items* kama ni hii inafanywa kwa kushirikiana na Bohari Kuu ya Serikali, ambayo ndiyo hivi sasa yenye jukumu la kununua bidhaa hizo. Katika tathmini hiyo, matumizi ya mtandao kufanya manunuzi, yaani *e-procurement,* yataangaliwa kwa kina. Pamoja na tathmini hiyo ya utaratibu wa manunuzi ya *common use item*, vilevile *PPRA* inafanya tathmini nyingine ya kina, kuangalia uwezo wa taasisi ya Serikali na kufanya biashara kwa kutumia *computer* na teknolojia ya habari katika shughuli zao za kila siku. Mfano, sasa hivi pamoja na mamlaka kuweka matangazo ya zabuni kwenye tovuti yake ni wafanyabiashara wachache tu wanaoitembelea ili kuona matangazo hayo, hatua hii ni muhimu kufanyika kabla ya kufikiria kutumia utaratibu huu wa *e-procurement*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kwa ujumla ili kuboresha ufanisi wa manunuzi ya umma, pamoja na taratibu zilizoanzishwa na kusimamia na kudhibiti manunuzi, *PPRA* kufuatilia uzoefu unaoupata kila siku inapitia kwa undani, ufanisi unapatikana pamoja na matatizo yaliyopo katika kuitekeleza sheria ya ununuzi ili kuweza kuishauri Wizara kuhusu hatua za kuchukuliwa ili kuweza kuleta maboresho, ili niweze kutoa ushauri huo, *PPRA* itachukulia kwa umakini, maoni yote yanayotolewa na wadau mbalimbali ikiwa na hayo yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani ili kuwezesha manunuzi yanayofanywa na taasisi za umma yafanyike kwa ufanisi zaidi na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba, kuhusu gawio la faida Benki Kuu mwaka 2003/2004 na 2004/2005 na sababu ya Serikali kutotegemea faida kutoka Benki Kuu mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kulingana na ripoti ya mwaka 2004/2005 ya hesabu za Benki Kuu, ilionesha kiwango cha faida kilichopatikana mwaka wa fedha 2003/2004 cha Sh.127,487,200,000. Kiasi hiki kilijumuisha kiasi cha Sh.109,791,399,000, kinachotokana na mapato yanayotokana na tathmini inayofanywa kwa hazina ya fedha, yaani *file action* lililoko Benki Kuu, pamoja na kiasi ambacho kilikuwa hakijaiva yaani hakijawa *realized.* Kulingana na Kanuni za Fedha za Kimataifa, yaani *International Financial Report Systems* na Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 1995, mapato ambayo hayajaiva *(Unrealized Exchange Gains),* hayawezi kujumuishwa kama

sehemu ya faida ya mwaka ambayo inatakiwa kugawanywa, pamoja na sehemu yake kulipwa kama gawio.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kulingana na hesabu za benki za mwaka 2003/2004, faida halisi, yaani *distributable profit* iliyogawanywa ilikuwa kiasi cha Sh.17,749,233,000, gawio lilikuwa Sh.5,086,848,000, Serikali ya Muungano ya Tanzania ilipata gawio la Sh.4,857,939,440, ikiwa ni asilimia 95.5 ya gawio na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipata kiasi cha gawio la Sh.228,908,160, ambacho ni asilimia 4.5 ya gawio. Kiasi cha gawio kutokana na faida ya mwaka 2003/2004 cha Sh.5,086,848,000 kinaonekana ni kidogo kutokana na sababu zilizoelezwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa faida ya Benki Kuu kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004, ulifanywa kwa kuzingatia Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 1995, ambapo kiasi cha Sh.1,774,923,000 kilienda kutunisha mfuko wa kinga nyinginezo *(General Reserve Funds)* na faida yote unayoipata siyo lazima yote uigawe, nyingine lazima uweke kama kuongeza mtaji wa ile benki yenyewe. Kiasi cha shilingi bilioni kumi kilipelekwa Mfuko wa Mradi wa Benki ya Mali za Kudumu *(Reserve for Projects Fund)* na kiasi cha Sh.887,462,000 kilienda kwenye Mfuko wa Nyumba *(Staff Housing Fund)*. Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005, kiasi cha faida ya Benki Kuu iliyopata kwa mwaka ilikuwa Sh.9,177,822,000 na faida halisi ambayo inastahili kugawanywa kulingana na Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 1995 na Kanuni za Kimataifa za uhasibu *(International Financial Policy address),* ilikuwa ni kiasi cha Sh.5,202,775,000 baada ya kupunguza tengo la Sh.3,975,047,000, ambalo kulingana na Kanuni za Kimataifa za Uhasibu na Sheria za Benki Kuu ya 1995, hakiwezi kugawanywa bali kinapelekwa kwenye Mfuko Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa faida ya Sh.5,202,775,000 ulikuwa kama ifuatavyo: Mfuko wa Nyumba Sh.260,139,000, Mfuko wa Miradi ya Benki ya Mali za Kudumu shilingi bilioni tatu, Mfuko wa Kinga Nyinginezo Sh.520,277,000 na gawio *(dividend),* Sh.1,422,359,000. Ukitafuta jumla hii unapata hizo Sh.5,202,775,000. Serikali ya Muungano wa Tanzania ilipata Sh.1,354,352,845 na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipata Sh.64,006,155.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, tegemeo la faida lilikuwa halipo kutokana na mapato ya benki kuwa chini, pamoja na gharama kubwa ya riba inayolipiwa na benki kuhusiana na amana ili kupunguza ujazo wa fedha katika uchumi hivyo, kusababisha Serikali kutotegemea gawio la faida toka Benki Kuu mwaka huu wa fedha na ndio maana ikawekwa sifuri pale.

Hata hivyo, faida iliyopatikana kulingana na hesabu zilizokaguliwa kama ilivyoripotiwa kwenye taarifa ya Kambi ya Upinzani, inatokana na mapato ambayo hayatokani na shughuli za kawaida za uendeshaji Benki Kuu na siyo rahisi kukadiriwa kwa uhakika, kwani inategemea zaidi mwenendo wa thamani ya shilingi, yaani *exchange rate movements,* ikilinganishwa na fedha nyingine za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya matatizo yanayojitokeza katika magari yanayoingizwa Tanzania Bara kutoka Tanzania Zanzibar, licha ya *escudo plus*

*plus* kuwepo Zanzibar. Masuala yote ya uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi au bidhaa inayotolewa sehemu moja ya nchi hadi nchi nyingine, yanasimamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya 2004, kifungu cha 135. Sheria hiyo inafafanua kwamba, kodi ambayo haikukusanywa au ilikadiriwa pungufu kwa makosa ya aina yoyote, inapaswa kukusanywa pindi inapobainika kuwa haikulipwa kikamilifu. Aidha, Sheria inatoa madaraka kwa Kamishna wa Forodha, kuhakiki malipo ya ushuru kwa bidhaa ambazo tayari zimeingizwa nchini, ikiwa ni pamoja na magari yanayotokea Tanzania Zanzibar kuja Tanzania Bara ili kudhihirisha kama ushuru unaostahili ulilipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria na utaratibu huu si maalum kwa magari yanayotoka Zanzibar tu, bali pia kwa magari au bidhaa zinazokadiriwa kuwa ni pungufu sehemu yoyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bidhaa yoyote iliyoingizwa nchini iwe Tanzania Bara au Tanzania Visiwani, hutozwa kodi au tofauti ya kodi ambayo haikulipiwa pindi inapobainika kuwa bidhaa hiyo haikulipiwa kodi hiyo inayostahili, kwani nyote mnajua vituo vyote ambavyo bidhaa zetu kutoka nje zinapitia ni Horiri, Horohoro na vinginevyo ikiwemo Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kudhamini upya bidhaa hususan magari yanayoingizwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, limeendelea kuwepo licha ya kwamba, mtandao wa *escudo plus plus* umeshaanza kutumika Tanzania Zanzibar. Tatizo hili halitokei kwa magari mapya, bali kwa magari makuu kuu, ambayo mara nyingi bei zake hutofautiana. Tofauti hizo za bei mara nyingi hutoa mwanya kwa baadhi ya waingizaji wa magari kutueleza bei halisi waliyonunua magari hayo, kwa nia ya kukwepa kulipa ushuru unaostahili.

Tatizo hili husababisha Idara ya Forodha, kukadiria upya na kutoza ushuru unaostahili kulipwa pindi inapobainika kwa thamani iliyoelezwa na mwingizaji haiendani na thamani iliyopo katika kumbukumbu za bei, yaani *transaction price data base* za Idara ya Forodha. Hata hivyo, hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* kwa nia ya kuwaelimisha waagizaji bidhaa nchini na walipa kodi kwa ujumla ili waweze kueleza thamani halisi ya bidhaa walizoingiza nchini, kwa lengo la kuepusha usumbufu wa namna hiyo unapotokea pindi bidhaa zinazohamishwa kutoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano kwenda upande mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja juu ya malipo ya waliokuwa watumishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Kitengo cha *Income Tax*. Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amehoji kutolipwa mafao kwa watumishi waliokuwa wa Jumuiya ya Afrika Mashiriki iliyovunjika tarehe 30 Juni, 1977, Kitengo cha *Income Tax*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleweke kwamba, mafao yanalipwa kwa wale tu waliokuwa waajiriwa wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hadi tarehe 30 mwaka 1977, siku ambayo Jumuiya ilivunjika na kwamba kuvunjika kwa Jumuiya, kuliathiri ajira za waajiriwa wa Kitengo cha *Income Tax.* Ajira zao zilihamishiwa Serikali Kuu kabla ya kuvunjika kwa Jumuiya na walilipwa mafao yao kabla ya kuvunjika kwa

Jumuiya, hivyo mafao yanayolipwa kwa waliokuwa waajiriwa wa Jumuiya hadi tarehe 30 Juni, 1977, hayawahusu kwa vile ajira zao hazikuathiriwa na kuvunjika kwa Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nitoe mchango wangu kwa hotuba iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kujibu baadhi ya hoja zilizojitokeza hapa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza inahusu Miradi ya *Millennium Challenge Corporation.* Awali ya yote, ningependa kukumbushia ukweli usiopingika kwamba, mahitaji yetu kifedha ni makubwa sana kuliko mapato yetu ya ndani na yale ambayo tunayapata kutoka nje. Katika hali hii ni lazima kuchagua mambo machache kulingana na uwezo wetu kifedha, hiki ndicho kilichofanyika katika mchakato wa kupata miradi ya kunufaika na Mpango wa *MCC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa nitazungumzia utaratibu uliotumika kuainisha miradi ya kuwasilisha *MCC* kwa upande wa Tanzania Bara. Mapendekezo ya miradi yanatoka katika sekta husika, kwa upande wa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi, ilitumia utaratibu wake kupata miradi iliyohitajika kutokana na azma ya kuleta maendeleo kwa wananchi wote wa Zanzibar. Sehemu kubwa ya miradi iliyoainishwa ni kutoka Pemba na mradi mmoja wa *Sun Marine Transmission Cable* ulitoka Zanzibar. Barabara zilizochaguliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kama ifuatavyo; moja, Mzambarauni - Takao - Finya, kilometa 8.3; mbili, Mzambarauni - Karibu - Mapofu, kilometa 8.3; tatu, Bahanasa - Baya - Mtambwe, kilometa 13.1; nne, Chwale - Kojani, kilometa 2 na tano, Kipangagani - Kangagani, kilometa 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ilifikia uamuzi huo kwa kuzingatia mambo mawili; kwanza; kwa sababu Pemba ni sehemu ya Tanzania na hivyo ina haki sawa na sehemu nyingine ya Jamhuri yetu. Pili, tayari ipo miradi mingine kadhaa yenye wafadhili kutoka nje, inayotekelezwa Zanzibar kama vile *Zanzibar Port,* unaofadhiliwa na *European Union*, Mradi wa Barabara, yaani *Zanzibar Road Upgrading Project,* unaotekelezwa kwa ufadhili wa *ABD*, Mradi wa Elimu ya Sekondari wenye ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kuhusu kuboresha Vitabu vya Bajeti, iliyotolewa na Mheshimiwa John Momose Cheyo. Imetolewa hoja kuwa taarifa zinazotolewa katika Vitabu vya Bajeti hazieleweki kutokana na kutokuwa na mchanganuo wa kina. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa John M. Cheyo kuwa, Vitabu vya Bajeti huandaliwa katika mfumo wa Kimataifa wa takwimu za bajeti za Serikali, yaani *Government Finance Statistics* wa mwaka 1986. Ni kweli kuwa mfumo huo wa 1986, hautoi taarifa za kutosha na baadhi ya maelezo yanajumuisha aina nyingi za matumizi. Kwa hiyo, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Fedha la Kimataifa *IMF,* ambalo ndilo linalosimamia mfumo huo Kimataifa, imeanza kuteleza mpango

utakaotuwezesha kubadili mfumo wa vitabu vyetu na kuanza kutumia mfumo mpya wa mwaka 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo yameanza kutolewa kwa maafisa wanaohusika na uandaaji wa bajeti na takwimu zake kutoka Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango na Uwezeshaji, pamoja na Benki Kuu. Hata hivyo, ni vizuri kuzingatia kwamba, mifumo hii ni ya Kimataifa na inaendelezwa ili kuweza kulinganisha maendeleo ya kiuchumi baina ya Mataifa. Kwa hiyo, inawezekana kwamba, hata huo mfumo mpya unaweza ukaonekana kutokidhi baadhi ya mahitaji yetu, lakini ni bora kuliko ule wa mwaka 1986.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kazi zilizofanywa na Tume ya Pamoja ya Fedha, tangu kuanzishwa kwake. Kabla ya kujibu hoja hiyo, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo: Tume ya Pamoja ya Fedha, ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume, Sura Namba 140 ilizinduliwa rasmi Juni, 2003. Kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Tume ina majukumu yafuatayo:-

(a) Kuchambua mapato na matumizi yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgao wa kila mmojawapo wa Serikali hizo.

(b) Kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za kifedha za Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha ya Serikali mbili.

(c) Kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais ataipatia Tume au kama Rais atakavyoagiza na kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ambazo zimetekelezwa na Tume ni kama ifuatavyo:-

(a) Ripoti ya madeni baina ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzia mwaka 1993/1994 hadi 2003/2004.

(b) Ripoti ya asasi za Muungano na gharama zake kwa kipindi cha mwaka 1993/1994 hadi 2003/2004.

(c) Taarifa ya safari za mafunzo zilizofanywa na Tume kwenye nchi zenye muundo wa Serikali za Muungano au Shirikisho.

(d) Ripoti ya mapendekezo kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri alivyoelezea katika hotuba ya mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka

2007/2008, Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zipo katika mchakato wa kujadiliana mapendekezo yaliyowasilishwa na Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ilikuwa ni hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa kuhamisha huduma za pensheni kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Baada ya Serikali kuamua kuhamisha huduma za kuwalipa wastaafu mafao ya kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuanzia mwaka 2007/2008, yafuatayo yametekelezwa hadi sasa:-

- Mikutano na wadau mbalimbali zikiwemo Wizara mbalimbali na Mifuko husika, yaani *PSPF, PPF, GAPF* na *Controller and Auditor General,* pamoja *NSSF* imeshafanyika. Katika mikutano hiyo, kero mbalimbali zinazowahusu wastaafu zilijadiliwa na kutafutiwa ufumbuzi wa kuziondoa ikiwa ni pamoja na kufupisha taratibu zinazotumika hadi mstaafu anapolipwa mafao yake.

- Elimu kwa wastaafu kwa njia ya vipeperushi, magazeti na redio ili kuwafahamisha juu ya uamuzi wa Serikali wa kuhamisha huduma ya pensheni kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeanza kutolewa na itaendelea kutolewa.

- Maandalizi ya kuhamisha huduma ya pensheni kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii yanaendelea ili hatimaye ifikapo Janauri, 2008 huduma hii iweze kufanywa na mifuko husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni bajeti finyu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Pamoja na ongezeko la asilimia 23 katika bajeti ya fedha za ndani kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali, yaani *National Audit Office* kwa mwaka huu wa fedha. Ofisi hiyo bado inakabiliwa na upungufu wa fedha kwa kuzingatia kupanuka kwa haraka kwa majukumu yake. Kuongezeka kwa shughuli za ofisi hii kunatokana hasa na mambo makubwa yafuatayo: Ufinyu wa Bajeti ya Serikali, ambao unagusa Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali; Ongezeko la Wilaya na Halmashauri, pamoja na Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi; Mabadiliko ya kiteknolojia Duniani na utendaji Serikalini hivyo, kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali kuwa wa kitaalamu zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali; Nia ya kuondoa wakaguzi wa kazi, yaani *Resident Auditors* kutoka katika ofisi zinazokaguliwa ili kuhakikisha uhuru wao wanavyofanya kazi za ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa ofisi hii, Serikali imekuwa ikiongeza bajeti yake kama ifuatavyo katika miaka mitatu iliyopita mwaka 2005/2006, mishahara ilikuwa bilioni 145, matumizi ya kawaida yalikuwa Sh.6,566,000,000, mwaka huu wa 2007/2008, mishahara imeongezeka hadi kufikia bilioni 1,620,000,000, matumizi ya kawaida yameongezeka hadi kufikia bilioni 8,442,000,000 na jumla yote ni bilioni 12,363,000,000. Pamoja na ongezeko hili, Serikali inaendelea kuzungumza na wahisani walioyoonesha nia ya kusaidia ofisi hii ili wagharamie ujenzi wa majengo ya ofisi hii ili kuharakisha zoezi la kuwahamisha wakaguzi kutoka katika ofisi wanazokaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ilikuwa ni Sheria ya Ukaguzi wa Umma, yaani *Public Audit Act,* iletwe Bungeni mapema. Hoja ya kuwepo kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma, ilitolewa kwa mara ya kwanza Octoba, 2006 kwenye Kongamano la Uwajibikaji lililofanyika katka Hoteli ya Whitesands na kuhudhuriwa na Wabunge wa Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali Kuu na Hesabu za Serikali za Mitaa, Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu wa Hazina na Mhasibu Mkuu na Viongozi wengine mbalimbali kutoka Serikalini, pamoja na wadau wengine. Katika mkutano huo, sababu na madhumuni ya kuwepo kwa Sheria ya Ukaguzi wa umma zilielezwa bayana. Sababu hizo ni pamoja na kurekebisha mapungufu mengi yaliyobainika katika Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 na kuipa uwezo zaidi, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, kutekeleza majukumu yake. Aidha, kuwepo kwa sheria hiyo ni mojawapo ya matakwa ya Umoja wa Kimataifa kwa taasisi za Ofisi za Taifa za Ukaguzi, yaani *ANTOSAI* na hivyo, kukidhi utaratibu unaokubalika Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa, Wizara ya Fedha imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri, wenye mapendekezo ya kutungwa kwa sheria hiyo ili Muswada wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma, uwasilishwe Bungeni baada ya maandalizi yote kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ilijitokeza ni riba za mikopo bado kubwa sana, wakati riba za amana katika Mabenki ya Biashara ni za chini. Mambo yanayosababisha riba za mikopo kuwa juu sana ni pamoja na miundombinu hafifu, ambayo huongeza gharama za uendeshaji shughuli za kibenki, ardhi kutotumika kama dhamana ya mikopo, ucheleweshaji wa kesi za mabenki na wateja wake, utoaji wa *court injunctions* na benki za biashara kutoweza kuuza dhamana za mikopo kwa kipindi kifupi ili kurejesha fedha zilizokopeshwa, vilevile kuna udhaifu katika kurejesha mikopo kwa baadhi ya wakopaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kupitia usimamizi wa Benki Kuu, itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kibiashara ambayo yatapunguza gharama za uendeshaji, shughuli za kibenki ili kuziwezesha Benki zetu kutoza riba nafuu. Kukamilika kwa utekelezaji wa maboresho katika Sekta ya Fedha unaoendelea hivi sasa, yaani *Second Generation of Financial Sector Reform*, utaeleta ufanisi mkubwa ambapo moja ya matunda ya ufanisi huo, itakuwa ni kushusha riba za mikopo na kuongeza riba za amana katika mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ambayo ninapenda kuizungumzia ni Benki Kuu ya Tanzania, Wakurugenzi wote wanatoka Tanzania Bara, kwani hakuna yeyote kutoka Tanzania Visiwani ambaye ana uwezo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa Benki Kuu ni chombo cha Muungano, kikihudumia Serikali zote mbili ni haki kwa mfanyakazi anayeajiriwa kutoka upande wowote wa Muungano, kupandishwa cheo ili mradi awe na sifa zinazohitajika kulingana na nafasi ya ajira hii iliyopo. Vivyo hivyo, katika kujaza nafasi za uongozi katika Benki Kuu, Uongozi wa Benki Kuu huangalia sifa bila kujali mfanyakazi anatoka

upande upi wa Muungano. Kwa hulka yetu Watanzania si jambo jema wala si kawaida, kuulizana sehemu anayotoka mtu ili kuamua kama anafaa kuajiriwa au hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na swali hili kuulizwa mara kwa mara, inatulazimu kufanya uchambuzi wa asili za wafanyakazi walio katika Taaisi za Muungano zilizo chini ya Wizara ya Fedha. Kwa kweli, utaratibu huu unaweza kuathiri mshikamano wetu wa Kitaifa kama utaendelezwa lakini tumelazimika kufanya ili ukweli wa hoja ujulikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Benki Kuu ina wafanyakazi 1,330, kati ya hao wafanyakazi 70 wanatoka Tanzania Zanzibar, ambayo ni sawa na 5.3% ya wafanyakazi wote. Huu ni uwakilishi mkubwa kuliko uwakilishi wa kutumia kigezo cha idadi ya watu, ikizingatiwa kwamba, Wazanzibari wote ni takriban 2.9% ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana na sasa nitamwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi na Wenyeviti wa Bunge, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo mnaifanya, kwa kuongoza mkutano huu wa kujadili bajeti hii ya 2007/2008 tangu pale tulipoanza. Lakini kama tulivyosema awali ni kwamba, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, pamoja na Kamati nzima. *(Makofi)*

Pia napenda kumshukuru Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashi Mohamed, kwa maoni na ushuri wa Kambi yake, kuhusu bajeti hii ya Wizara ya Fedha na leo napenda kusema kwamba, imewasilishwa na Mwanamama Kijana, kwa hiyo tunasema ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, ambao walichangia kwa maandishi na pia wale waliochangia kwa kuandika, lakini pia wale ambao walichangia kwa kuzungumza hata nje ya Bunge, wamekuwa wakizungumza. Naamini kwamba, wale Waheshimiwa Wabunge ambao hawakupata nafasi kuchangia bajeti hii, basi wataendelea kuunga mkono Wizara hii ya fedha na Bajeti yetu ili tupate uwezo wa kutekeleza yale ambayo Wananchi wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge, walitaka tuyafanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kawaida, napenda niwataje Waheshimiwa Wabunge 11 waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni, pamoja na Manaibu Waziri wawili. Wabunge hao ni Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji , Mheshimiwa Eustace O. Katagira , Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Adam K. A. Malima, Mheshimiwa Dr. Chrisant M.

Mzindakaya, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib na Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge waliochangia kwa maandishi walikuwa 19 nao ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Mohammed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba na Mwanne I. Mchemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe maelezo kuhusu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, kuhusu bajeti ya Wizara ya Fedha. Naomba pia nichukue nafasi hii moja kwa moja, kuwashukuru Waheshimiwa Naibu Mawaziri, kwa kuelezea baadhi ya hoja hizi. Niseme kwamba, kwa mara nyingine tena, napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi, ambayo kwa kweli tumefanya kazi vizuri tu na mpaka hivi juzi tulikuwa tunazungumza juu ya suala hili la *NIC.*

Napenda labda tu niweke ufafanuzi kidogo, kwa kumbukumbu kuhusu maelewano yaliyofikiwa katika kikao cha pamoja cha Kamati ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwekezaji, *PSRC, NIC* na Jumuiya ya Wafanyakazi. Mazungumzo yalikuwa ya uelewano mkubwa sana na uelewa upande wa Serikali ni kwamba, tutakwenda kupendekeza kwa Baraza la Mawaziri, mkakati mbadala wa kurekebisha *NIC*, kwa sababu kama nilivyoeleza kwenye Baraza la Mawaziri ni kwamba, kumekuwa na mkakati huu wa ubinafsishaji, lakini kuna mawazo ambayo yalitolewa. Kwa hiyo, tutakwenda kwenye Baraza la Mawaziri ili kupendekeza mkakati mbadala na Kamati itafahamishwa uamuzi wa Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni juu ya tofauti ya takwimu kati ya Taarifa ya Benki na Vitabu vya Mapato. Ninapenda kusema kwamba, Kitabu cha Makadirio ya Mapato, yaani *Revenue Estimate Volume I,* huwa na takwimu za makisio ya Mapato ya Serikali kwa mwaka ambao unahusika. Taarifa za Benki Kuu, hutoa matokeo ya utendaji kwa kipindi ambacho kinahusika na kwa kweli tunaweza kusema ni takwimu za historia kwa sababu ni takwimu za nyuma. Kwa sababu hiyo, kuwepo kwa tofauti kati ya Makisio na Matokeo halisi, baada ya programu kutekelezwa kwa mwaka mzima, kwa kweli siyo jambo la ajabu kwamba unaweza kubajeti hivi lakini matumizi yakawa ni tofauti, siyo jambo la ajabu. Ndiyo maana hata mara nyingine tunasema kwamba, hapa tunakuja kwa ajili ya *reallocation*, kwa sababu unaweza kubajeti lakini ikabidi utumie zaidi kuliko kile ambacho umekibajeti kwa sababu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimtoe wasiwasi Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba, mapato yanayozidi kiwango kilichokadiriwa awali, hutumika kwa kuzingatia sheria za nchi. Mapato yoyote ya ziada yanapopokelewa na Serikali, huingizwa katika akaunti zake na kutumika katika vipindi vinavyofuata kwa msingi wa bajeti inayoidhinishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa ni kuhusu udhibiti wa manunuzi ya vifaa vya umma. Jibu ni kwamba, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004, imeanzisha utaratibu ambao unatoa fursa kwa kila taasisi ya umma, kufanya na kuwajibika na manunuzi yake itakayofanya. Lakini ili kuhakikisha kuwa taratibu zinafuatwa, ikaanzishwa *PPRA* kwa lengo la kutoa miongozo, kujenga uwezo na kusimamia na kudhibiti shughuli za manunuzi ya Taasisi za Umma. Kwa hiyo, *PPRA* ilichukua nafasi iliyokuwa nayo *Central Tender Board.* Utaratibu huu unatumika katika nchi zote za Afrika Mashariki na kwa kweli siyo kweli kwamba, unatumika hapa Tanzania peke yake. Kwa vile ni lengo la Sheria kutoa nafasi kwa wazabuni wote, inasisitiza kuwa zabuni zitangazwe kwenye vyombo vya habari, hata hivyo, Sheria na Kanuni zimeweka wazi njia nyingine zinazoweza kutumika kuitisha zabuni bila matangazo kwenye magazeti kwa zabuni zenye thamani ndogo. Mamlaka inawaelimisha wahusika kwenye Taasisi za Umma kuhusu njia hizi mbalimbali, kwa lengo la kuwawezesha kupunguza gharama za matangazo. Vilevile Mamlaka imeanzisha tovuti na iko katika hatua ya mwisho kuanzisha jarida litakalotumika kutangaza zabuni za Taaisi za Umma.

*PPRA* ikiwa ni moja ya kazi zake, inaendelea kufanya tathmini hivi sasa ya utaratibu utakaotumika kununua bidhaa na huduma zinazotumiwa na Taasisi nyingi za umma, yaani *common use items,* kuna zile ambazo zinatumika. Kwa hiyo, utaratibu unataka kuangaliwa ni jinsi gani ambapo tutaweka utaratibu huu. Tathmini hii inafanywa kwa kushirikiana na Bohari Kuu ya Serikali, ambayo ndiyo sasa hivi yenye jukumu la kununua bidhaa hizo. Katika tathmini hiyo, matumizi ya mtandao kufanya manunuzi ya *e-procurement,* ambayo imezungumzwa, yataangaliwa kwa kina pamoja na tathmini hiyo ya utaratibu wa manunuzi ya *common use items.*

Vilevile *PPRA* itafanya tathmini nyingine ya kina kuangalia uwezo wa Taasisi za Serikali na Wafanyabiashara kutumia kompyuta na teknolojia ya habari katika shughuli zao za kila siku. Mfano sasa hivi pamoja na Mamlaka kuweka matangazo ya zabuni kwenye tovuti yake ni wafanyabiashara wachache tu wanaoitembelea ili kuona matangazo hayo, hatua hii ni muhimu kufanyika kabla ya kufikiria kutumia utaratibu huu wa *e- procurement.*

Kwa ujumla, ili kuboresha ufanisi wa manunuzi ya umma, pamoja na taratibu zilizokwisha kuanzishwa za kusimamia na kudhibiti manunuzi, *PPRA* kufuatilia uzoefu inaoupata kila siku, inapitia kwa undani ufanisi unaopatikana pamoja na matatizo yaliyopo katika kuitekeleza Sheria ya Ununuzi ili kuweza kuishauri Wizara kuhusu hatua za kuchukua ili kuweza kuleta maboresho. Ili iweze kutoa ushauri huo, *PPRA* itayachukulia kwa umakini maoni yote ambayo yanatolewa na wadau mbalimbali, ikiwemo haya ambayo yametolewa kwa upande wa Kambi ya Upinzani ili kuwezesha

manunuzi yanayofanywa na taasisi za umma, yafanyike kwa ufanisi na kwa gharama nafuu. Lakini labda nieleze kwamba, suala zima pia limezungumziwa hapa, matangazo ya kwenye magazeti na kwamba fedha nyingi zinatumika na kadhalika. Mimi nafikiri kwamba, suala lolote lile ambalo linataka *transparency* au uwazi lina gharama zake, kwa sababu pia hatujawa transparency nayo, pia tunaweza kushuku kuwepo na rushwa. Kwa hiyo, jambo hili kwa kweli kabla hatujafikia suala hilo la *Procurement*, nafikiri kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gawio la faida hili lilishazungumzwa kwa hiyo, sitalizungumza kwa sababu hakuna haja ya kulirudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miradi ya MCC, Naibu Waziri ameshalieleza hili na suala lilikuwa kwamba ni kwa nini miradi isiende Unguja na suala zima la Miradi ya Pemba. Napenda kusema kwamba, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndiyo ambayo ilileta mapendekezo haya ya kupeleka miradi hii kwenda Pemba na mimi ninafikiri hili ni jambo zuri sana ili Wananchi wa Pemba wajue kwamba, Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi inawajali vilivyo. *(Makofi)*

Kwa upande wa Unguja kuna miradi mingi ambayo imefanyika kwa mfano, miradi ambayo imefadhiliwa, ukichukua mradi ambao umefadhiliwa na *EU, Zanzibar Port,* Mradi wa Barabara, yaani *Zanzibar Road Up-grading Project,* ambao unatekekelezwa na ufadhili wa *ADB,* Mradi wa Elimu ya Sekondari ambao unafadhiliwa na *World Bank* na kadhalika. Kwa hiyo, hata juzi hivi tulikwenda Zanzibar kutia saini kwa ajili ya Barabara mbalimbali kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni juu ya Benki ya Raslimali *(TIB),* napenda kusema kwamba, Serikali imeendelea kutekeleza azma yake ya kuimarisha Benki ya Raslimali Tanzania, kwa kuiongezea mtaji kwa awamu hadi kufikia shilingi bilioni 50. Hadi sasa Serikali imekwisha ongezea mtaji wa shilingi bilioni 12.7 na hivyo kufikia shilingi bilioni 20. Aidha, *TIB* pia imeweza kupata mkopo wa dola za Kimarekani milioni tano kutoka *NORDIC, Southern African Development Community*, kuiwezesha kutoa mkopo kwa shughuli za kiuchumi na pia mazungumzo yanaendelea kati yake na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *NPPF, NSSF* na *PSPF* ili kwa kweli nao waweze kutoa mkopo wa muda mrefu kwa ajili hii.

*TIB* itaimarisha usimamizi wa Mifuko Maalumu, ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Fedha wa Kuhuisha Mikopo, yaani *Re-financing* na ule utaratibu maalum, wa ukopeshaji kwa ajili ya uzalishaji wa maua au tunaweza kusema ni *Structured Financing,* yenye thamani ya shilingi bilioni 155 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la *TIB* katika mwaka wa fedha 2007/2008 ni kuongeza rasilimali zake kwa kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha vya ndani na pia vyombo vya fedha vya nje na kuweza kurekebisha mfumo wa uongozi, kuimarisha mfumo wa teknolojia na kuweza kuimarisha ushirikiano wa vyombo vya fedha vya Kimataifa kwa lengo la kupata mikopo zaidi na kukopesha zaidi miradi ya maendeleo ili

kuweza kukuza uchumi. Lengo kwa kweli ni kuhakikisha mtaji unafikia shilingi bilioni 73.7 mwaka 2010 na kuongeza mikopo hadi shilingi bilioni 155 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la taarifa kuhusu upatikanaji wa mtaalamu wa kufanya Ukaguzi Maalumu, yaani *Special Audit* ni ya *EPA Account,* Benki Kuu. Serikali ilifanya uamuzi wa kuwepo na Ukaguzi Mkuu Maalumu wa Akaunti ya *EPA*, Benki Kuu mwezi Oktoba, 2006 na Waziri wa Fedha alimwandikia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuhusu uamuzi huu wa Serikali mwezi Novemba, 2007. *CAG* alianza mchakato wa utayarishaji wa Hadidu za Rejea, yaani *Terms of Reference* za kazi hiyo na Hadidu za Rejea hizi zilikubaliwa mwezi Aprili, 2007.

Mwezi Mei 2007, *CAG* alikaribisha zabuni za kazi hii kutoka kwa makampuni ya ukaguzi binafsi ya kimaitaifa yaliyo na ofisi hapa nchini. Makampuni hayo ni saba kulingana na taaarifa zilizopatikana kutoka Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi, yaani *NBAA*, ambayo ndiyo iliyoratibu taasisi hizi. Nazo ni *Price Water, Annes and Anne PKF Tanzania Deloit and Tush, DCMD grand thorn tone PKMG.*

Tarehe 14 Juni, 2007 kulikuwa na kikao cha awali cha wazabuni wa Bodi ya *tender* ya Ofisi ya Ukaguzi kuzungumzia *tender* hii, ambapo taasisi tatu za ukaguzi ndizo zilizoshiriki. Nazo zilikuwa ni *Price Water, Annes and Anne* na *PKMG.* Tarehe 28 Juni, 2007 ilikuwa ni siku ya mwisho kupokea maombi ya *tender* hii, ambapo Bodi ya *Tender* ya Ofisi ya Ukaguzi ilifungua *tender* zilizokuwa zimewasilishwa mbele ya wasimamizi wa taasisi husika. Ilibainika kuwa, Taasisi zilizokuwa zimewasilisha *tender* zao kwa kazi hii zilikuwa mbili; nazo ni *Annes and Anne* na *KPMG.* *CAG* aliteua Kamati ya kutathmini mapendekezo ya kitaalamu, yaani *technical and proposal,* ambapo taasisi zote mbili zilifaulu.

Matokeo hayo yalinadiwa na kupitishwa na Bodi ya *Tender* ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi tarehe 18 Juni, 2007. Bodi ya *Tender* ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilifungua bahasha za mapendekezo ya gharama za uchunguzi huu, yaani *financial proposals* mbele ya wawakilishi wa zabuni tarehe 25 Julai, 2007 na Kamati ya kutathmini mapendekezo hayo bado inaendelea na kazi hiyo. Matarajio ni kuwa kazi hii itakamilika ijumaa ya tarehe 17, yaani ijumaa ijayo. Taasisi itakayofanikiwa kupata kazi hii, itatakiwa kukamilisha kazi hii katika muda wa siku 60. Hayo ndiyo maelezo kuhusu *EPA.*

Suala la kuboresha vitabu vya bajeti, Mheshimiwa John M. Cheyo, nafikiri limeshazungumzwa kwa hiyo, sina haja ya kulirudia. Suala la Wakurugenzi pia kutoka Zanzibar, kama alivyoeleza Mheshinimiwa Naibu Waziri na hivi sasa labda niseme kwamba, kuna *Deputy Govenovers* kama watatu na kati yao mmoja ni kutoka Zanzibar, lakini tunasema kwamba tunafuatilia pale ambapo kweli kuna Wazanzibari wenye sifa za kuweza kufikiriwa, basi itaweza kufanyika hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la *JFC,* yaani Tume ya Pamoja ya Fedha na kulikuwa na wasiwasi kwamba, mbona imechukua muda mrefu. Lakini tuseme kwamba, imechukua muda mrefu kwa sababu suala hili ni lazima lifanywe kwa umakini, baada ya taarifa hizi kuja, ilibidi *ownership* iwe upande wa Zanzibar na upande wa

*United Republic, otherwise* kwa mfano, ingekuwa kwa Baraza la Mawaziri la Serikali ya Jamhuri, kungekuwa hakuna *ownership* upande wa Zanzibar, kwa hiyo, mapendekezo hayo yalipelekwa Zanzibar. Upande wa Zanzibar wamefanya vikao na baada ya hapo Wizara ya Fedha ya Zanzibar na Wizara ya Fedha kwa upande wa Jamuhuri ilifanya vikao na baada ya hapo mapendekezo haya kama tulivyosema, yatakwenda kwenye Kikao cha Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. Nina hakika kwamba, suala hili litaweza kukamilishwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni juu ya *ZRB* ipewe Wakala wa kukusanya mapato ya Muungano Zanzibar. Ninapenda kusema kwamba, kwa mujibu wa Katiba na Sheria, jukumu la kukusanya mapato yote ya Muungano ni la Serikali ya Muungano, pamoja na Taasisi zake. Kwa eneo la kodi, jukumu hilo limekabidhiwa kwa *TRA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* hutumia mawakala mbalimbali, kukusanya kodi panapobidi kwa kutegemea utaalamu unaotakiwa. Kwa hivi sasa *TRA* na *ZRB*, wanashirikiana sana hasa katika kubadilishana taarifa za walipa kodi. Kwa hiyo, kuna ushirikiano mkubwa kati ya *TRA* na *ZRB.*

Kuhusu *ZRB* kuwa Wakala wa kukusanya mapato ya Muungano Zanzibar kwa niaba ya *TRA*, Serikali inaona kwamba, hatua hiyo itakuwa na gharama zaidi kuliko ilivyo hivi sasa, kwa kuwa italilazimu *ZRB* kuweza kujenga uwezo wa kusimamia kodi za forodha na kodi za mapato, ambazo haizisimamii kwa sasa.

Aidha, *TRA* tayari imejenga uwezo huo na inatekeleza majukumu yake hayo kwa nchi nzima. Sidhani kama ni busara kufanya hivyo, kwa sababu kwa kusema kwamba itaongeza *actually cost* na kama nilivyosema kwamba, ushirikiano unafanyika kati ya *TRA* na *ZRB* na hata katika *Finance Bill*, ambayo tutaipitisha tutaona kwamba ni jinsi gani ambapo uboreshaji huu unakwenda zaidi ambapo tunasema kwamba, vitu vyote vile ambavyo vinatumika kwa mfano, Zanzibar basi mapato yaende Zanzibar moja kwa moja yasipitie Wizara ya Fedha. Yatoke *TRA* moja kwa moja na kwenda Zanzibar. Utaratibu wa sasa ilikuwa ni mpaka ipitie kwenye Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, hilo nafikiri ni jambo zuri, ambalo linaonekana kwamba linaweza kuleta manufaa zaidi.

Suala lingine lilikuwa ni juu ya suala la Benki kuwafikia wananchi Tanzania. Naweza kusema kwamba, ilipitishwa Sheria ya Mabenki na Taasisi za fedha mwaka 1991, ambayo imerekebishwa na kubadilishwa na Sheria ya mwaka 2006. Sheria ya mwaka 1991, iliruhusu kuanzishwa kwa mabenki binafsi na Watanzania na pia wageni na kufanya kazi kwa mfumo wa soko huria.

Mpaka sasa mabenki 24 na taasisi za fedha 10, zinatoa huduma za kibenki nchini. Hapo awali mabenki mengi yalikuwa na matawi Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na Mwanza, isipokuwa Benki za *NBC, NMB* na *CRDB* ambazo zilikuwa na matawi katika kila mkoa na baadhi ya Wilaya.

Kadri miaka inavyokwenda na idadi ya mabenki kuongezeka na hii inaonesha *confidence* kwa kweli katika uchumi, ushindani umekuwa mkubwa sana hivyo mabenki sasa yanashindwa kufungua matawi mikoani na wilayani. Hivi karibuni, Benki Kuu imetoa vibali vingi sana vya kufungua matawi mikoani na wilayani, hasa kwa yale mabenki makubwa na ya kigeni kama Barclays, wana kibali cha kufungua matawi 20, Stanbic na mengineyo ya Kitanzania kama Azania, Exim na kadhalika. Benki kongwe nchini nayo hayakuachwa nyuma katika mchakato huu wa kufungua matawi, mathalani kwa mwaka 2007, *NBC* imefungua matawi mapya sita, *NMB* imefungua matawi mapya matano na kuomba kufungua matawi mengine 15 kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Vuguvugu hili linatupa imani kwamba, si muda mrefu tutaanza kuona huduma za benki zikiwafikia Watanzania wengi zaidi, hasa ukizingatia pia kwa kurahisisha na kuenea kwa *Microfinance Institutions*, pamoja na *SACCOS* ambazo zitaanzishwa kwa kasi ili kutekeleza azma ya Serikali ya uwezeshaji. Kwa hiyo, suala zima nafikiri la *SACCOS* na *Community Banks,* linakwenda moja kwa moja kwa wananchi.

Suala lingine lilikuwa hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa kuhamishia huduma za pensheni kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Napenda kusema baada ya Serikali kuamua kuhamishia huduma ya kuwalipa wastaafu mafao yao kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuanzia mwaka 2007/2008, yafuatayo yameweza kutekelezwa hadi sasa:-

Kwanza, mkutano wa wadau mbalimbali, zikiwepo Wizara mbalimbali na Mifuko husika, yaani *PSPF, PPF, GEPF* na *CAG* imekwisha fanyika.

Mbili, katika mikutano hiyo kero mbalimbali zinazowahusu wastaafu zimejadiliwa na kutafutiwa ufumbuzi wa kuziondoa, ikiwa ni pamoja na kufupisha taratibu zinazotumika hadi wastaafu wanapolipwa mafao yao.

Tatu, elimu kwa wastaafu kwa njia ya vipeperushi, magazeti na redio ili kuweza kuwafahamisha juu ya uamuzi wa Serikali wa kuhamishia huduma ya pensheni kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii, imeanza kutolewa na itaendelea kutolewa.

Nne, maandalizi ya kuhamisha huduma ya pensheni kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii yanaendelea ili hatimaye Januari, 2008, *Inshallah,* huduma hii ifanywe na mifuko husika.

Suala lingine lilikuwa juu ya hili la *dollarisation* kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Bungeni ni kwamba, Serikali itatoa tamko katika kipindi cha wiki inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena nichukue nafasi hii, kushukuru kwa kutupa nafasi lakini nakushukuru zaidi pia kwamba, *winding-up* hii haijafanyika mchana, bali imefanyika jioni kwa hiyo, angalau imefanya kidogo tuwe na ahueni. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hii imetolewa na kuungwa mkono, sasa ili tuweze kuendelea tunaingia katika hatua nyingine.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 22 - Wizara ya Fedha**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwaarifu kwamba, tunapoingia kwenye vifungu, Fungu 22 ni Deni la Taifa, hakuna shilingi ya mtu yeyote pale. Fungu 23 ni Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Waziri bado hayupo hapo. Fungu 45 ni Ofisi ya Mkaguzi Mkuu, hakuna Mshahara wa Waziri hapo.

Kwa hiyo, tutakapofikia Fungu 50, ndiyo mambo yenu, yaani Mshahara wa Waziri upo hapo. Kwa hiyo, Fungu 22, 23 na 45 wala msisumbuke hapo, hampewi kitu, Mshahara wa Waziri ni Fungu 50.

Kif. 1001 - *Administration and General* ……………Sh. 609,147,867,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kif. 3001 - *Public Debt Management* ..............................Sh. 1,457,186,400
Kif. 3002 - *Expenditure Management* ..............................Sh. 554,286,000
Kif. 3003 - *Financial Management*............................Sh. 83,955,094,600
Kif. 3004 - *Systems and Internal Audit*.............................Sh. 4,843,503,500
Kif. 3005 - *Sub Treasury Arusha*……..………………...Sh. 252,446,000
Kif. 3006 - *Sub Treasury Coast*……..…………………Sh. 201,140,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3007 - *Sub Treasury Dodoma*… … … … … ... ... Sh. 238,049,000/=
Kifungu 3008 - *Sub Treasury Iringa*… … … … … ... ... ...Sh. 215,322,000/=
Kifungu 3009 - *Sub Treasury Kagera*… … … … … ... ... ..Sh. 205,905,000/=
Kifungu 3010 - *Sub Treasury Kigoma*… … … … … ... ....Sh. 211,343,000/=
Kifungu 3011 – *Sub Treasury Kilimanjaro*… … … … ...Sh. 207,620,000/=
Kifungu 3012 - *Sub Treasury Lindi*… … … … … … ... ... Sh. 227,622,000/=
Kifungu 3013 - *Sub Treasury Mara*… … … … … ... ... ....Sh. 215,560,000/=

Kifungu 3014 - *Sub Treasury Mbeya*… … … … … ... ... .Sh. 222,530,000/=
Kifungu 3015 - *Sub Treasury Morogoro*… … … … … ..Sh. 240,230,000/=
Kifungu 3016 - *Sub Treasury Mtwara*… … … … … ... ...Sh. 215,620,000/=
Kifungu 3017 - *Sub Treasury Mwanza*… … … … … ... ..Sh. 208,740,000/=
Kifungu 3018 - *Sub Treasury Rukwa*… … … … … ... ... Sh. 236,400,000/=
Kifungu 3019 - *Sub Treasury Ruvuma*… … … … … ... ..Sh. 206,140,000/=
Kifungu 3020 - *Sub Treasury Shinyanga*… … … … … Sh. 213,331,700/=
Kifungu 3021 - *Sub Treasury Singida*… … … … … ... ...Sh. 217,520,000/=
Kifungu 3022 - *Sub Treasury Tabora*… … … … … ... ...Sh. 226,460,000/=
Kifungu 3023 - *Sub Treasury Tanga* … … … … … ... ... Sh. 203,688,000/=
Kifungu 3024 - *Sub Treasury Manyara*… … … … … ... Sh. 423,800,000/=
Kifungu 7001 – *Pension and Gratuity*… … … … … ... ..Sh. 835,040,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and General*… … … Sh. 10,062,932,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 50 – Wizara ya Fedha**

Kifungu 1001- *Administration and General*… … … … Sh. 7,750,301,900/=

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nilikuwa naomba ufafanuzi tu kwa Mheshimiwa Waziri. Kama ninavyofahamu kwamba maduhuli yote yanayokusanywa na mafungu yote yanapaswa kuingia kwenye Mfuko wa Serikali. Sasa kwenye Idara ya Uhamiaji nimekuja kuona kwamba kutokana na hoja za Mkaguzi kwa muda wa miaka mitatu mawasilisho ya makusanyo ya kutoka Zanzibar yamekuwa hayawasilishwi kwenye Mfuko wa Serikali na hii imekuwa ikileta hoja sana za ukaguzi. Sasa nilichotaka kupata ufafanuzi kwa Waziri ni kujua kama huo utaratibu umebadilishwa na kama kuna *changes* zozote je, Mkaguzi hana taarifa na kuendelea kuweka hizi hoja?

Swali la pili, ni kwa upande wa fedha zinazopelekwa kwa Wakimbizi kutoka kwa wafadhili mbalimbali zimekuwa zikipelekwa moja kwa moja kwa Wakimbizi na haziingizwi kwenye vitabu vya Serikali. Nilitaka nijue tu je, hizi pesa zilizopelekwa moja kwa moja kwa Wakimbizi zinaingizwa kama *grant* kwa Serikali na kama sivyo kwa nini zimekuwa zikihojiwa na Mkaguzi au kuna utaratibu gani ambao umewekwa na Serikali kuzi-*book* fedha zote za wafadhili kwa ajili ya Wakimbizi? Ahsante.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, suala hili la fedha za Idara ya Uhamiaji ni suala ambalo na sisi pia tumelifuatilia kwa upande wa

Zanzibar na tumezungumza tayari na *CAG* ili kuangalia aidha, kufuta au kuanza na utaratibu tofauti. Kwa hiyo, hivi sasa tunalifuatilia na tayari tumewasiliana na *CAG* ili kulimaliza suala hilo.

Suala hili lingine la fedha ambazo zinakwenda kwa Wakimbizi labda ningefananisha pia kama fedha ambazo kuna wakati Mheshimiwa John Cheyo anasema kwamba kuna fedha mara nyingine hazionekani huku. Kwa hivyo, zinakuwa *queried.* Lakini inawezekana kwamba fedha zimekwenda moja kwa moja Mikoani, lakini taarifa zile nyaraka kutoka kule Mikoani zinakuwa hazikufikishwa katika Wizara mbalimbali. Kwa hivyo, pale ambapo nyaraka hizi hazikufikishwa basi *CAG* anakuwa anaweza ku-*query.*

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niko kwenye *Vote 50.*

**MWENYEKITI:** Kuhusu mshahara wa Waziri.

**MHE. FATMA ABDULHABIBI FEREJI:** Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri pamoja na Waziri kwa kujibu hoja vizuri ambazo zimetolewa na Kambi ya Upinzani. Vile vile kwa kukubali baadhi ya ushauri ambao tumewapa, tunashukuru sana kwa hilo.

Lakini nina suala moja ambalo sikupatiwa majibu kisawa sawa wakati nilipowasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani na linahusiana na kero ya magari ya Zanzibar yanayoingizwa kwa ajili ya matumizi hapa Tanzania Bara. Nilieleza kwamba magari yenye namba za ZNZ yanatakiwa kulipa kwa mwezi dola 25 za Kimarekani ili iweze kutumia namba hiyo kwa ajili ya matumizi hapa Tanzania Bara wakati kitu hicho hakipo Tanzania Visiwani. Gari yenye namba za usajili za Tanzania Bara zinapoingia Visiwani hazitakiwi kulipa na katika risiti hiyo kinachoshangazwa ina maelezo kabisa kwamba ukiingiza gari la kigeni ndani ya *Tanganyika Territory* na nilisema risiti hiyo tunayo na tunaweza tukai-*present*. Kwa hiyo, naomba majibu au maelezo juu ya suala hili. Hii ni kero ambalo niliizungumza na sio tofauti ya mapato. Ahsante.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa suala hili la Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, linahusiana naona na hili ni leseni na sio magari yale ambayo yanaingizwa bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Leseni ni kwamba leseni ni tofauti kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na upande wa Zanzibar. Kwa hivyo, fedha hizi ambazo zinazotolewa kwa mfano dola 25, shilingi 25,000/= ambazo matokeo ni kwamba ukileta gari na ikakaa zaidi ya siku saba basi lazima ulipie leseni ile au uiandikishe huko Tanzania Bara. Hiyo ndiyo ambayo inayotolewa na bahati mbaya labda hili tulikuwa tulijibu juu ya usajili wa magari. Ni kwamba usajili wa magari kama nilivyosema sio suala la Muungano kwa kuwa linasimamiwa na sheria mbili tofauti na kila mmoja likifanya kazi katika upande mmoja wa Muungano na kwa upande wa Tanzania Bara sheria hiyo hutumika ni Sheria ya Uandikishaji wa Uhamishaji wa Magari wa mwaka

1972. Kwa upande wa Zanzibar, Sheria inayotumika ni ya vyombo vya usafiri barabarani ya mwaka 2003. Hata hivyo kama tulivyosema usajili wa magari kutoka Zanzibar hautofautiani na utaratibu unaotumika kwenye usajili wa magari yanayotoka sehemu nyingine yoyote ile. Kwa hivyo, ikitoka Zanzibar inahesabiwa kama vile imetoka katika sehemu nyingine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda jambo la kuweza kufikiria ni kuangalia uwezekano wa kuwa na sheria moja katika Jamhuri nzima ya Muungano a kutokutofautisha kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nataka kuungana na Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kujibu maswali vizuri sana leo, sijui amelalaje, lakini nashukuru sana hili ndilo tulikuwa tunategemea. Mimi nataka kuuliza tu jambo dogo kwamba Naibu Waziri ameeleza juu ya sheria kwamba itakuja kwenye Bunge hili wakati maandalizi yatakapokuwa tayari, yeye Mheshimiwa Waziri anajua madhara?

**MWENYEKITI:** Ni sheria gani baba?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Sheria ya Ukaguzi, yeye Mheshimiwa Waziri anajua madhara ya kuchelewa na nimetumia muda mrefu sana, tumezungumza kwa muda mrefu juu ya jambo hilo, je, anaweza kutupa sasa kama ni muda gani au ni lini hiyo sheria itakuja hapa Bungeni ili tuweze tukaimarisha taasisi hii ambayo ni ya maana sana katika Taifa letu yaani Ukaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama unavyofahamu kuwa kazi ya ukaguzi haiwezi ikamalizika mpaka Wizara imejibu *in a form of Treasury Memorandum,* ni kwa muda mrefu mimi sijaona kwamba jambo kama hili linaletwa au linajibiwa na nafikiri ni utamaduni ambao labda umeachwa katika Wizara yake je, kwa sababu sasa *Public Accounts Committee* inaleta ripoti hapa ndani ya Bunge na kujadiliwa, ni lini basi utaratibu huu wa *Treasury Memorandum* ambao ni majibu ya Serikali utaanza kutekelezwa na hii ni jukumu la Wizara hii ya Fedha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nasikia umelala vizuri leo. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, basi wapunguze maswali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Cheyo, kwanza kuhusu hili la *audit,* napenda kumhakikishia Mheshimiwa John Cheyo kwamba suala hili lipo katika ngazi ya kupelekwa kwenye Baraza la Mawaziri na tutalifuatilia na kuhakikisha kwamba angalau mwezi Novemba, 2007 tutakapokutana hapa basi tuweze kulileta.

Suala la *Treasury Memorandum* ni kwamba utakumbuka kwamba huko nyuma baada ya Sheria ya *Finance* kupitishwa na kurekebishwa mwaka 2004, kulikuwa kunatakiwa kutengenezwe *regulations* na Waziri. Lakini hizi *regulations* zilikuwa hazikutengenezwa mpaka mwaka 2005, hizi *regulations* ndizo ambazo zinafanya *Public Accounts Committee (PAC)* watoe mapendekezo *(recommendation)* ambayo yatakwenda kwa Waziri ili kutoa adhabu kwa yule anayehusika. Kwa hivyo, hili ni suala ambalo kwa kweli kwa upande wa Wizara ya Fedha kwa sababu *regulations* ziko tayari na tutaona kwamba kutakuwa na mabadiliko katika suala hilo.

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia mchana nilimsihi Mheshimiwa Waziri sana sana kuhusu mambo matatu, mawili naomba niyarejee nipate maelezo kidogo ya ziada. Moja ni lile suala la Vitengo vya Kudhibiti Matumizi na msimamo wangu huu Waziri anaujua tangu tukiwa kwenye Kamati mwezi Juni, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba vitengo hivyo vya *Expenditure Tracking Unit* na *Technical Auditing* na vitengo vyote ambavyo sababu yake ni kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali, kama vikiwa *under funded,* matatizo yake ni kwamba tutakuwa na vitengo kwa ajili ya kuwa navyo. Sasa ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri namwomba akubaliane na mimi kwamba ana mamlaka ya kufanya *reallocation* kutoka Wizara nyingine kwenda nyingine na kadhalika anaweza akafanya *reallocation within* ili kuvijaza nguvu vitengo hivi, kuvipa ma-*accountant,* ma-*financial analysis, projects specialist* hasa kwa sababu vinafanya kazi kwa pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Kuvipa nguvu kwa sababu tukijenga *culture* ya kuogopa fedha ya Serikali basi nadhani kwamba tutakuwa tunaelekea katika njia nzuri katika *public spending* na naomba Waziri aniambie kama anakubaliana na mimi katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili hivi juzi juzi Kamati ya Fedha na Uchumi ilipata ugeni wa ujumbe kutoka Ethiopia na tuliwauliza *specifically* kazi za Benki Kuu ya kwao. Wakasema kazi ya Benki Kuu ya kwao moja kwa makusudi kabisa ku-*support* Benki za Kienyeji *(Local Banks).* Sasa na mimi nilikuwa naomba kwa sababu najua kwamba mimi nina uhakika Benki Kuu yenyewe haina uwezo wa ku-*support banking activity* kwenye *level* ile ambayo tunataka iwafikie watu wa Mkuranga na Mchinga na kadhalika.

Sasa maana yangu ni kwamba lengo langu nilikuwa nataka maelezo kama Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba hivi viprogramu vyote ambavyo tunataka vikuzwe ili pesa na *financial services* zinaweza kwenda vijijini pamoja na ile ambayo iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya *Rural Financing Development Scheme* kama vinaweza vikasimamiwa na Wizara yake kwa mtazamo wa kisera halafu kwa Benki Kuu ikawa ni utekelezaji tu. Lakini sera na usimamizi jicho haswa liwe chini yake kwa sababu sisi kama Wabunge tunaweza kumwuliza yeye hatuwezi kumwuliza Gavana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri najua wewe huna tatizo katika kujibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kumjibu Mheshimiwa Adam Malima kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba napenda kumhakikishia kwamba vitengo hivi vya kudhibiti ambavyo wamezungumzia Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na Waheshimiwa Wabunge ni kitengo ambacho ni muhimu sana na kimeongezewa kwa kweli uwezo kwa sababu ukiangalia hata katika kitabu hiki utaona kwamba ina-*cover* katika upande wa *expenditure management, financial management* pamoja na *system and internal audit.* Kama nilivyoeleza kwenye Bajeti yangu kwamba tayari kazi hii imeanza kufanywa tokea tarehe 27 Julai, 2007 ili kuweza kutembelea maeneo mbalimbali. Tunajua kwamba fedha nyingi na tumegawana kusema kwamba kuna baadhi ya Wizara ambazo zitaanza kwa mfano Wizara ya Miundombinu, Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Fedha pamoja na mikoa kadhaa ambayo hii *tracking* itaweza kufanyika.

Suala hili la *BOT* na *guarantee schemes* napenda kusema kwamba tutachukua mawazo yake na tunaangalia pia kama uwezekano wa suala zima la *guarantee schemes* labda pia kwenda kwenye Benki yetu ya Maendeleo *(TIB)* tuangalie ni jinsi gani ambapo tunaweza kufanya hivyo.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda nipate ufafanuzi kuhusu maelezo niliyotoa leo kuhusu mikopo ya wakulima wa Mkoa wa Rukwa. Kwa kuwa nilisema na Waziri alisikia, sitaki kurudia kwa kirefu lakini nataka niseme kwamba maendeleo ya nchi hii yanategemea kilimo na Benki hizi zina utaratibu bado wa kuendelea kutoa mikopo na mimi ninayo barua ambayo Wizara ilishaiandikia *NMB* kuidhinisha au kudhamini wananchi wapewe mikopo ya kilimo kwa utaratibu maalumu na nilisema pia *consultancy* ilishafanyika. *NBM* walichagua *consultant* akawashauri kwamba mradi huu ni mzuri na Bodi ilishapitisha lakini baada ya uamuzi huu wa Serikali wa uwezeshaji wa mikopo hii ni kama imevuruga fikra ile ya mwanzo ambayo ni kitu maalumu, mimi nataka nipate ufafanuzi.

La mwisho au la pili, ni kuwa katika Taarifa ya Mkaguzi Mkuu kulikuwa na hoja ambayo inaonyesha kwamba nchi marafiki zinazoahidi kuisaidia Tanzania na kwa utaratibu wa sasa fedha zote zinaingia katika Mfuko Mkuu kwa ajili ya Bajeti na ku-*support* Bajeti kwa ujumla. Lakini imeonekana katika Taarifa ya Mkaguzi kwamba baadhi ya ahadi hazikuwa zinatekelezwa kwa wakati, kwa hiyo, miradi mingine haikutekelezwa kwa sababu fedha hazikutolewa na wahusika kama ilivyoahidiwa na kuweka katika Bajeti. Sasa jambo hili nataka ufafanuzi Serikali haioni kama linaleta mushkeli katika utekelezaji wa Bajeti nzima kwa jumla?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze na suala la *General Budget Support (GBS)* ambayo inaungwa mkono na *donors* kama 14 hivi sasa

wakiongozwa na Waingereza. Nilisema kwamba kwa kweli asilimia ya fedha tulizozipata kutoka wahisani zilifika karibu asilimia 93. Kwa hivyo, labda pengine si sahihi kusema hivi ndiyo maana pale mwanzo nilisema kwamba mara nyingine kunakuwa na miradi inakwenda Mikoani lakini nyaraka zinachelewa kufika. Kwa hivyo, *CAG* anapokwenda kukagua anaona hakuna nyaraka hili ndilo ambalo linatokea. Tunazungumza na wenzetu ili kuhakikisha kwamba mara *project* zinapokwenda pamoja na wahisani na tumezungumza tayari na Sweden pamoja na Norway ambao wamekubali kwamba mara watakapopeleka *projects then* lazima wawasilishe nyaraka hizi.

Suala la *guarantee* la *NMB* baada ya kulizungumza nimezungumza mchana huu na wataalamu wangu walikuwa hawalielewi vizuri na labda niseme tu kwamba tutaweza kuzungumza na Mheshimiwa Mbunge lakini niweze kuweka wazi kwamba utaratibu ule wa bilioni 21 haukuvuruga utaratibu huu wa *guarantee*. Kwa sababu *guarantee* zipo bado na kuna *SMEs, export guarantee schemes* na kadhalika na hizi shilingi bilioni 21 ni tofauti, kwa hivyo tusije tukasema kwamba hizi labda zimeharibu utaratibu huu. Utaratibu huu unaendelea na utaratibu wa *guarantee* unaendelea na ningependa Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya labda baadaye pengine angeweza kuzungumza na wataalamu wangu na mimi mwenyewe. Ahsante

**MWENYEKITI:** Na ile barua akuletee.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kupata ufafanuzi wa masuala yafuatayo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, baada ya kumpongeza kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi wa kwanza unahusu maelezo tuliyopewa kuhusu faida za Benki Kuu na jinsi zinavyogawanywa. Eneo moja ambalo faida ya Benki Kuu inakwenda ni katika kujenga akiba ya kuendeleza taasisi. Sasa kama tunavyofahamu sasa hivi pale Benki Kuu kuna mradi mkubwa sana. Ule mradi nikilinganisha thamani ya mradi bila kwenda kwenye malumbano kama ni kiasi gani au kiasi gani ni ile thamani tu ambayo inakubalika. Ukiangalia *build up* inayotokana na *profit* za Benki yenyewe hailingani na thamani ya ule mradi. Sasa naomba ufafanuzi Benki Kuu inajenga jengo hili kutokana na pesa zinazotoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, huko nyuma nilipata kuhoji kwa nini Serikali imeweka *duty* kwenye dawa za binadamu ukiondolea mbali dawa za UKIMWI na Malaria, nikaambiwa mahali pake ni hapa pa leo. Sasa *duty* juu ya dawa za binadamu, binadamu hawa Watanzania wagonjwa halafu maskini kisha tunawawekea *duty* kwenye dawa wanazotaka kuzitumia, mimi hilo haliingii akilini na hasa nikizingatia kwamba katika *regime* ya nchi kwenye upande wa *tariffs, tariff* zinawekwa kwa mambo mawili ama ni *protection* ama ni *revenue raising measure*. Sasa sisi kama Watanzania tuna *protect* nini katika eneo la dawa ukizingatia kwamba asilimia takribani 90 ya dawa za nchi hii yanatoka nje, viwanda vyetu vina-*produce hardly 10%.* Nataka ufafanuzi huo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie hili la dawa za binadamu ambayo tumeweka asilimia 10. Hapa siku zote tunazungumzia juu ya kulinda viwanda vyetu na tunasema kwamba lazima tuendeleze uzalishaji katika viwanda

ndipo ambapo tutajiondoa katika utegemezi. Lakini hata suala zima la mfumuko wa bei hapa lilikuwa linazungumziwa ni kwamba hata shilingi yetu kuwa imara nafikiri itakuwa imara tu pale ambapo tutakuwa na viwanda zaidi na uzalishaji zaidi. Kwa hivyo hasa limefanywa kwa sababu ya kutetea viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliondoa hii asilimia 10 huko nyuma na ikafikiriwa kwamba bei za dawa zitakuwa chini. Lakini utafiti ambao uliofanywa ukaonyeshwa hapana bei zilikuwa juu zingine juu zaidi ya asilimia 40, ikaonekana kwa kweli haikusaidia kitu lakini badala yake inaumiza viwanda vyetu. Kwa hivyo, ikaamuliwa kwamba tukiweka asilimia 10 lakini asilimia 10 hii ni kwamba haihusishi kama alivyosema dawa kwa mfano ya malaria lakini haihusishi pia dawa yanayoagizwa na Serikali *through MSD* na kadhalika. Ni asilimia 10 kwa dawa mengine. Kwa hivyo, zaidi umuhimu hasa hasa ni kulinda viwanda vyetu na utafiti umefanywa kwamba hata pale ambapo imeondolewa haikusaidia kitu lakini wafanyabiashara waliongeza bei za madawa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *BOT* ni kwamba nafikiri anazungumzia juu ya *Twin Towers?*

**MWENYEKITI:** Nadhani ndiyo hizo kwamba hela nyingine zinatoka wapi ukilinganisha na fedha walizojengea na faida zao?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kutokana na mtaji wa *BOT* na labda nieleze pia kwamba kwa sababu suala hili la *Twin Towers* lilikuwa linazungumzwa sana ni kwamba ukaguzi wa *Twin Towers* pia umefanyika na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu na kuna barua yake pia hapa ambayo tayari imesema *Twin Towers* walikagua malipo yote yaliyofanywa na Benki Kuu kuhusu majengo hayo na tuliweza kuhakiki uhalali wa malipo yote kwa kipindi cha mwaka 2005/2006. Tuliridhika na maelezo ya ongezeko la bei ya ujenzi kwa jambo hili, sasa labda sijui Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Kuna nini tena, kuhusu hiyo ya *Twin Towers*?

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu amejibu suala ambalo mimi sikuuliza hilo. Suala langu ni kwamba kama alivyosema sasa hivi imejengwa kutokana na mtaji wa Benki Kuu. Mtaji wa Benki Kuu ni shilingi bilioni 20 na kama zimeongezeka watuambie zimeongezeka zimefika kiasi gani. Lakini thamani ya majengo hayo ni mabilioni ya shilingi. Sasa suala ni kwamba hizi zimetoka wapi? Ndiyo suala hilo wala mimi sikuuliza uhalali. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Anauliza kwamba ukiangalia hailingani na mapato yake sasa umetoa wapi fedha nyingine? Kama huna kesho unaweza kujibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba *CAG* ndiye ambaye anakwenda kukagua na kutoa taarifa hizi. Kwa hivyo, katika ukaguzi kama

nilivyosema wa *CAG* ameangalia na ameridhika kwa fedha ambazo zilizotolewa na kutumika na Benki Kuu na kwamba zimetoka kwenye mfuko wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wanachosema mapato ya *BOT according* kwa Mheshimiwa Mbunge pale wanashangaa hivi hela zingine zimetoka wapi, maana ukilinganisha na walionayo haiwezi kujenga kiasi hicho. Mtapata jibu baadaye, tunaendelea. Nyie wataalamu mtafutieni Waziri majibu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba ufafanuzi tu kuna hili suala la riba kuwa kubwa. Leo asubuhi wakati Waziri anajibu swali hapa Bungeni ….

**MWENYEKITI:** Riba ya nini?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Riba katika Mabenki

**MWENYEKITI:** Kwa ajili ya mikopo?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Yaah, katika mikopo. Nilitaka kupata ufafanuzi wa *strategy* kwa sababu Waziri anasema sababu zinazofanya riba ziwe kubwa na nitaomba nimnukuu hapa anasema: "Miundombinu hafifu ambayo huongeza gharama za uendeshaji, shughuli za Kibenki, ardhi kutotumika kama dhamana ya mikopo, ucheleweshwaji wa kesi za Mabenki na wateja wake, utoaji wa *court injuctions,* wateja kuchelewa kupata hati miliki ya ardhi yaani *Title deed* na Benki ya Biashara kutoweza kuuza dhamana ya mikopo kwa kipindi kifupi kurejesha fedha zao. Jana wakati Mheshimiwa Rais anafungua Benki ya *Stanbic* kule Moshi, moja ya jambo kubwa na *message* aliyowapa wale kwenye Benki ni kwamba bado *interest rate* ni kubwa sana na Waziri leo bahati nzuri ametuambia sababu zinazofanya *interest rate* zetu kuwa kubwa. Mimi nanachotaka kupata ufafanuzi kuna mkakati gani sasa wa kuweza ku-*combat* hizi *reasons* ili ziweze kutusaidia kushusha hizo *interest rate?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, *CUF* wamewakilishwa na Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri swali hili limejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri asubuhi hii vizuri sana na ndiyo yale ambayo ameeleza Mheshimiwa Peter Serukamba. Tunathibitisha kwamba hayo lakini tuangalie kwa mfano kuna Sheria za Ardhi, mara nyingine unaweza kutoa mkopo halafu watu wakaweka *Court injunction* kwa hiyo, suala hilo lazima tuangalie, kuna Sheria ya *Mortgage Financing* ambayo tunazungumza kwamba tunatarajia kuileta labda mwezi wa Oktoba.

Kwa hivyo, ni mambo yote hayo ambayo yatafanya ili *interest rate* ziwe chini lakini pia tumeeleza katika Bajeti hii kwamba Serikali haitakopa kutoka kwenye *Commercial Banks* na kwa maana hiyo kama haitakopa basi wananchi wataweza kukopa zaidi na kwa maana hiyo fedha zitakuwa nyingi kwa upande wa Mabenki na kwa maana

hiyo lazima kwa vyovyote vile kutakuwa na ushindani; na kama kutakuwa na ushindani ili wazitoe zile fedha zao lazima *interest rate* tunategema kwamba itakuwa chini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, lakini suala la *BOT* ni muhimu muandae majibu.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante wakati anaandaa majibu ya *BOT* labda na mimi nihoji kidogo. Wakati nilichangia kwa mdomo na kwa maandishi, kwa maandishi nilichangia mambo mawili. Kuna suala la *hotel levy* ambalo ni sheria inawataka wenye hoteli waweze kuchangia asilimia 20 kwenye mapato yao. Sasa sisi imetuletea matatizo sana na niliuliza kwamba asilimia 20 ni kubwa mno, kama mtu anavyumba kumi kwenye hoteli yake na anachangisha shilingi 10,000 kwa kila chumba ni laki moja na inatakiwa shilingi 20,000 ipelekwe kule; na hiyo inaonekana ni *very unfair*. Sisi watu mpaka watu wa hoteli wamefikia hatua ya kuiambia Halmashauri au wakusanya kodi kwamba hizo fedha afadhali wawape wao waendeshe. Sasa kisichoeleweka je, hiyo kodi inakatwa baadhi ya faida au ni pamoja na matumizi yote inakatwa pale? Kwa sababu niliomba waiangalie upya hiyo kodi kwamba inaumiza wananchi, kwa sababu sehemu nyingine zote ni asilimia tatu au mbili na imekuwa migogoro kwenye Wilaya zote.

La pili, nilipenda kuomba msaada kwa sababu katika Bajeti ya Wizara ya Fedha iliyopita tuliipokea vizuri sana walikuwa na mawazo mazuri sana, tulikuwa na suala la mafuta. Walituletea tukakubaliana nao kwamba itaongezeka shilingi mia moja. Lakini sasa hivi mafuta yamepanda, kwa Mwanza ni 1,600/= kwenye Wilaya yangu ni 1,700/= petroli ambayo ni ongezeko kama la shilingi 400/=. Nilipenda kufahamu je, Serikali inapata nini katika hilo ongezeko kubwa na itatusaidia vipi ku-*control* vipi kwa sababu ilikuwa ni kwamba tulipouliza swali ilikuwa ni kwamba tuta-*control* watu waweze kuangalia na matokeo yake ni kwamba sasa sehemu zingine bei ni kubwa mno ya usafiri. Ninaomba kusaidiwa hilo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze na hili la mafuta, ni kwamba kama tulivyoeleza kwamba kwa kupandisha shilingi 100/= tusingetegema mafuta yangepanda vile; na hata Mheshimiwa Rais amelizungumza suala hili lakini naomba kusema kwamba kwenye *Finance Bill* hii ambayo inakuja suala hili litakuwa *addressed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *hotel levy* ningeomba kumwambia Mheshimiwa Faustine Rwilomba, kwamba suala hili tunalichukua na kuangalia na Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Anasema swali la pili la hoteli wataliangalia kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii. Suala la mafuta litashughulikiwa kwenye *Finance Bill* kati ya leo au Jumatatu. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Natoa tu angalizo kidogo, akizungumzia Maliasili na Utalii maana yake anazungumzia hoteli kubwa kubwa, sasa zimekuwa

*affected* hata wale wauza migahawa wanadaiwa kule kwetu kama hawamo ieleweke kwamba inagusa hoteli kubwa na wale kwa sababu mimi kwangu hakuna hata hoteli moja ya kitalii. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faustine Rwilomba, sikiliza basi kwanza hiyo ni Halmashauri kwanza, ndiyo maana wenzako wakasema wataangalia huko. Mheshimiwa kuhusu lile la Benki Kuu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Kuhusu suala la Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, jibu ni kwamba fedha zilizolipwa zinatokana na faida ya Benki Kuu zilizowekezwa kwa miaka ya nyuma yaani kwa maana nyingine ni *accumulated reserve* na pia *allocation* ya *reserve* kwa ajili ya *projects* za kila mwaka kwa sababu kila mwaka kunakuwa na *projects*. Kwa hiyo, hizi ni fedha ambazo zimekuwa *allocated* kwenye *projects* hizi za kila mwaka. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichatajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 *Finance and Accounts* ... ... … … … … Sh. 7,817,660,000/=

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, *sub vote 1002, sub item 260300 hospitality*. Wakati tulipokuwa tunaangalia Wizara nyingi na hasa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa tuliona kwamba kifungu cha *hospitality* kilikuwa kidogo sana na sehemu nyingine haikuwepo. Lakini ukiangalia hapa *hospitality* imepanda kwa kwa shilingi milioni 80.

Sasa ni kwa nini kifungu hiki kimepanda kiasi hiki hasa kwenye kitengo cha *Finance* ikizingatiwa hata kile cha *Administration* ambacho Mheshimiwa Waziri yumo, *hospitality* pale ni ndogo. Lakini namba mbili ni kifungu namba 260800 *Training Expenses*. Nikiangalia pale ni kwamba pia napo kuna ongezeko la zaidi ya shilingi milioni 95 kwa mwaka huu nilikuwa naomba Waziri atuambie ni kwa nini imekuwa hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba *sub vote 1002, item 260300* imeongezeka kutoka milioni 3.0 hadi milioni 83.6 hii imetokana na shughuli ambazo zimeongezeka hasa katika *Auditing System* ya sehemu mbalimbali katika Wizara ya Fedha kwa hiyo, ile *hospitality* kwa wale wote ambao wanafanyakazi zimekusanywa hapa. Ukiangalia *sub vote 1001*, ukiangalia *hospitality* utaona kwamba hapo zimepunguzwa kutoka milioni 67 mpaka imekuja kwenye milioni 47. Ukiangalia hivyo hivyo katika *sub-vote* nyingine utakuta vile vile zingine zimepunguzwa zingine zimezidishwa. Kwa hiyo, tumerekebisha kulingana na hali ya matakwa hasa ya *Financial Management* katika Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *training,* tunazungumza siku zote kwamba lazima wafanyakazi wahasibu na ma-*auditors* lazima wawe *trained* na kila tunavyoendelea lazima tuwe tuna-*train* watu wengi zaidi. Kwa hivyo, *apparently* fedha za *training* zitazidi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1004 *Legal Services* … … … … …. …. … ... ...Sh. 234, 672,500/=
Kifungu 1005 *Information, Education and Comm*… ...Sh. 1,658,561,000/=
Kifungu 1006 *Internal Auditor* … … … …. … …. ... ... ...Sh. 164,900,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 *Government Budget* … … … … ..Sh.128, 327,890,400/=

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri alivyojibu maswali vizuri, naomba ufafanuzi kuhusiana na *programme 20, sub vote 2001, item 261100 other goods and services note classified above.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana zilikuwa bilioni 37 na mwaka huu ni shilingi bilioni 126 ongezeko la shilingi bilioni 90 ambalo ni ongezeko la asilimia 240. Kuna tatizo la wakulima wa pamba ambao hawajalipwa muda mrefu sana deni lao kwa taarifa zilizopo.

**MWENYEKITI:** Hebu subiri kwamba swali hapa si wakulima wa pamba? Swali ni sababu gani kifungu hiki kimeongezeka, si kwa sababu ya wakulima wa pamba?

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Nauliza kwamba fedha za wakulima wa pamba ndiyo ongezeko hili, kuna hela za wakulima wa pamba hapa? Ndiyo swali langu, ili hawa wakulima wa pamba walipwe na tatizo hili liishe kabisa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza hii ya *other goods and services not classified* ni juu ya nyongeza ya mishahara upande wa Serikali na upande wa Mashirika ya Umma. Kwa hiyo, si wakulima wa pamba

**MWENYEKITI:** Hakuna wakulima wa pamba hapa.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa pamba hawajalipwa fedha hizo na hawajatengewa fedha. Je, Mheshimiwa Waziri atanieleza kwamba kwa niaba ya wakulima hawa Kahama, Bukombe, Uyui, Urambo, Magu na kwingineko kwamba fedha hizi za wakulima wa pamba kwa nini zisichukuliwe hapa shilingi milioni 130, wakalipwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Limbu, Kanuni inakukataza kusema hivyo. Ungetaka kusema maneno yako ambayo hayapo popote pale ni kwenye Mshahara wa Waziri hapa ni *very specific,* hawawezi kuchukua mishahara ya watu wakalipa wakulima wa pamba, unaona tofauti?

Noamba ukae wala sitakuruhusu, hapa ukiuliza ni *specific* kwa maeneo fulani ingekuwa pale kwenye sera ya mshahara wa Waziri unaweza kuuliza kitu chochote ambacho unatamani ujibiwe tu pale. Sasa hapa umemaliza hoja.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 *Policy and Research* … … … … .. ... ...Sh. 90, 118,951,500/=
Kifungu 2003 *Treasury Registrar* … … … … … …... ...Sh. 6, 246,575,500/=
Kifungu 4001 *External Finance* … … … … … … ... ...Sh. 3,372,778,900/=
Kifungu 5001 *Stock Verification* … … … … … …... ...Sh. 3,953,529,100/=
Kifungu 6001 *Computer Services* … … … … … ... .... ..Sh. 1,627,895,600/=
Kifungu 6002 *Tax Revenue Appeals Board* … … ... ... ... Sh. 781,648,400/=
Kif.ungu 6003 *Technical Audit Unit* … … … … … ... ... Sh. 412,806,900/=
Kifungu 6004 *Tax Revenue Appeals Tribunal* … ... Sh. 464,084,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kifungu 3003 *Financial Management* ... ... ... .... ... ... ...Sh.6, 162,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kifungu 1001 *Administration and General* ... .... .... .....Sh. 2, 300,000,000/=

*(Kifungu kilichatajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 50 - Wizara ya Fedha**

Kifungu 1001 *Administration and General* ... .... .... ... ..Sh. 2,705,400,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 *Finance and Accounts* … … … … … ... ..Sh. 3,210,900,000/=

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote 1002, sub item 6321,* ninaomba Mheshimiwa Waziri anieleze hii *Construction of IAA* ni kitu gani na hii *library* ipo wapi?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *Arusha Institute of Accounts* ambayo ipo Arusha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1004 *Legal Services* … … … … …. …. … ... ... Sh. 165,200,000/=

Kifungu 2001 *Government Budget* … … … … … ... ...Sh. 2,032,700,000/=

Kifungu 2002 *Policy and Research* … … … … .. ... ... Sh.17,091,200,000/=

Kifungu 2003 *Treasury Registrar* … … … … … … ... ...Sh. 4,834,400,000/=

Kifungu 4001 *External Finance* … … … … … …. ... ...Sh. 1,606,500,000/=

Kifungu 5001 *Stock Verification* … … … … … … ... ... Sh. 246,800,000/=

Kifungu 6001 *Computer Services* … … … … … ... ... ... Sh. 1,173,000,000/=

Kifungu 6002 *Tax Revenue Appeals Board* … … .. ... ...Sh. 247,700,000/=

Kifungu 6003 *Technical Audit Unit* … … … … … ... ... Sh. 196,000,000/=
Kifungu 6004*Tax Revenue Appeals Tribunal* … ... ... ... Sh. 198,200,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Bunge lilirudia*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka 200/2007 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza asubuhi kwamba sasa tunaingia kufunga siku 35 kwa Muswada mdogo huu unaitwa *Appropriation Bill.* Utaratibu wa sasa ni *Bill* si tena hotuba ya Waziri, tukifika kwenye vifungu hatutakuwa tena na Kamati ya Matumizi itakuwa Kamati ya Bunge Zima. Kwa hiyo, hapo hakuna kutoa shilingi tunapitia Muswada. Katibu.

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2007 *(The Appropriation Bill, 2007)***

*(Kusomwa mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2007 *(The Appropriation Bill, 2007)***

*(Kusomwa mara ya Pili)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa kutumia shilingi 6,066,832,108,300/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya miradi ya maendeleo itakayotekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na kutumia fedha zitakazotolewa na Serikali kwa ajili hiyo sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2007/2008 ilieleza shabaha na malengo ya Serikali ya kutumia shilingi 6,066,832,108,300/= kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kama ifuatavyo:-

Kwanza matumizi ya kawaida shilingi 3,865,736,179,000/=, pia matumizi ya miradi ya maendeleo shilingi 2,201,095,929,300/= na jumla ni shilingi 6,066,832,108,300/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu limeshajadili na kupitisha hoja mbalimbali za Waheshimiwa Mawaziri wakati walipowasilisha makadirio za Wizara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kuliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 ya jumla ya shilingi 6,066,832,108,300/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo iliyokubaliwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, kama nilivyosema Muswada huu hatujadili kwa sababu wenye Muswada huu wakiangalia kiambatanisho utakuta Wizara zote mlizojadili na kiwango cha pesa mlizopitisha kwa kila Wizara kipo huku. Kwa hiyo, tunaingia hatua ya pili Kamati ya Bunge Zima, sasa hiyo ndiyo tunaendelea kuhojiwa kifungu kwa kifungu ili kusudi tuweze kuhitimisha.

Kwa hiyo, mtakuta kwamba Muswada huu tumesoma hatua zote kwa wakati mmoja, *first reading* tumesoma sasa hivi na *second reading* tunaingia sasa *second reading* kwa maana Kamati ya Bunge Zima halafu tutaingia *third reading* tutakuwa tumemaliza. *(Makofi)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2007 *(The Appropriation Bill, 2007)*

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4(2) ambacho kinazungumzia juu ya kumpa Mheshimiwa Waziri mamlaka ya kuweza kukopa, sasa nataka kuelewa tu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa Fedha, tumepitisha sasa hivi ukiangalia katika deni la Taifa inaonekana kuna ongezeko kubwa sana katika *payment* ya *interest* hizi kwa *short term* mikopo ya ndani na pia kwa *long term* imefika mpaka karibu bilioni 100 na ushee. Sasa mimi nauliza hii *power* kweli inatumiwa vizuri na Mheshimiwa Waziri kama tunaona ongezeko kubwa kama hilo la deni la ndani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema kwanza kabisa kwamba Serikali haitakopa ndani safari hii. Lakini pia utaratibu wa mikopo hivi sasa ni kwamba Waziri wa Fedha hawezi tu akaamua hivyo, kuna Kamati ambayo inaitwa *National Debts Strategy* ambayo inapitia mikopo yote na mikopo yote ni lazima iwe ni mikopo yenye *interest* ndogo kama vile ambavyo tulikubaliana na *HIPC* na *IDA*. Kwa hivyo, utaratibu uko *compact* yaani siyo kwamba unaweza tu ukaamua tu leo ukakopa na kadhalika. *(Makofi)*

**MHE. JOHN. M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

**MWENYEKITI:** Kwanza nimekuona nikupe tu upate elimu lakini sio kwamba sikukuingiza kwenye kubishana. Nilitaka upate elimu, tunaanza na *Finance Bill* unaweza kuzungumza tena.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ukiamua hivyo ahsante.

**MWENYEKITI:** *Finance Bill* unaweza kuzungumza.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibala ya 5

**MHE KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha tano kinampa Mamlaka Waziri wa Fedha kufanya *reallocation* ya fedha ambazo Bunge limepitisha; na uzoefu wa mwaka jana unaonyesha kwamba Waziri wa Fedha alifanya *reallocation* ya jumla ya shilingi bilioni 318, takribani asilimia kumi ya Bajeti ya Serikali ambayo Bunge hili lilikaa na kupitisha na baadhi ya *reallocation* ambazo zilifanyika kwa sababu kifungu hiki kinazungumza kwenye *public interest* yaani baadhi ya *reallocation* ambazo zilifanyika kwa uzoefu wa Bajeti ya mwaka jana zilikuwa ni *reallocation* ambazo inatia shaka ku-*define* hiyo *public interest* hasa ukiangalia ile *statement of reallocation* namba moja na *statement of reallocation* namba mbili ambalo linaeleza hizo fedha zinakwenda wapi. Kuna takribani shilingi milioni 300 ambazo zilienda kwa uhamisho tu wa Wakuu wa Wilaya. Sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri aweze kunifafanulia, ana *limitation* gani za kisheria kwa mujibu wa *percent* za kufanya *reallocation* ya fedha ambazo Bunge limepitisha?

Pili, katika *reallocation* ambayo ilifanyika mwaka jana, Wizara ya Fedha ilichukua takribani shilingi bilioni tano kutoka katika Bajeti ya Bunge, je, Waziri wa Fedha atalihakikishia Bunge hili Tukufu kwamba katika *reallocation* ambayo kama ikitokea itakayofanyika mwaka huu atahakikisha kwamba hadhi na heshima ya Bunge inalindwa na fedha ya Bunge haitachukuliwa bila ruhusa ya Bunge? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** La pili hatajibu! La kwanza atajibu kwa sababu ni swali la *principle*; ni utaratibu gani *reallocation* inaweza kufanywa. Hilo utajibiwa ! Lile la kwanza, hapana. Hii tunazungumzia fedha za mwaka huu, si zile!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *reallocation* ambayo hutoa taarifa hapa Bungeni, hayo inaweza kutokea kwa mfano, kwa mwaka jana tukikumbuka kwamba Taifa liliingia katika matatizo kadhaa ambayo halikutegemea. Kwa mfano, kulikuwa na njaa ambapo ilibidi Serikali iwahudumie wananchi kama shilingi milioni 3.6. Bila Serikali kufanya hivyo, wananchi wale wangeweza kufa kwa njaa. Kumetokea na tatizo la umeme pia hapa na kwa sababu kumekuwa na matatizo ya mvua na kama Serikali isingehamisha fedha hizo, basi ingemaanisha kwamba tungeendelea pengine kuwa gizani kwa saa zaidi ya 18 na kwa maana hiyo viwanda visingefanya kazi na kodi hii ambayo tunasema tunaipata tusingeweza kupata.

Kwa hiyo, *reallocation* inatokea tu pale ambapo kitu ambacho kinatokea kile ambacho hukutegemea. Hivi ndivyo ambavyo *reallocation* inatokea na taarifa zinatolewa Bungeni. Lakini, labda niseme kwamba suala hili la kwamba Serikali imetumia pesa nje ya Bajeti kwa kweli hili si sahihi.

**MWENYEKITI:** Hapana, pointi hapa ni kwamba unaweza kufanya *reallocation* kama kunatokea dharura yoyote, ndio *principle* tunayoizungumzia hapa. Kwa hiyo, hatuingii ku-*discuss* yale mambo mengine kwa sababu tuna-*finalize* ile tuliyoanza nayo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*Bunge lilirudia*

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kutoa hoja kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Kutoa taarifa, siyo hoja!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani! Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedh, naomba kutoa taarifa kwamba Muswada wa Sheria ya Kutumia Fedha Shilingi 6,066,832,108,300/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa jili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo itakayotekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, sasa ukubaliwe. Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, siku 35 sasa zimekwisha, sasa tunaanza *business* nyingine.

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2007**
***(The Finance Bill, 2007)***

*(Ulisomwa mara ya Pili)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2007 pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kwa kiwango kikubwa, Muswada huu umezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati na pia tutaendelea kufanyia kazi mapendekezo mengine ipasavyo. Aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa tena shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichangia katika hotuba ya Bajeti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa Muswada huu, wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti wametoa ushauri wao ambao pia tumeuzingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi lengo la Muswada huu ni utekelezaji kisheria wa hatua kadhaa za mfumo wa kodi na ada mbalimbali kama nilivyowasilisha Bungeni katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2007/2008 mnamo tarehe 14 Juni, 2007 na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Aidha, Muswada huu unakusudia pia kuzifanyia marekebisho Sheria 12 zinazohusu fedha, kodi na ushuru kwa lengo la kuweka, kurekebisha au kufuta viwango vya kodi, ushuru na ada mbalimbali. Sheria hizo ni Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura Namba 147, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura Namba 41, Sheria ya Kodi ya Mapato Sura Namba 332, Sheria ya Madini, Sura Namba 123, Sheria ya Fedha za Umma, Sura Namba 348, Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura Namba 220, Sheria ya Bodi ya Rufaa za Kodi, Sura Namba 408, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura Namba 148, Sheria ya Kodi ya Mauzo Nje ya Nchi, Sura Namba196 , Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Utoaji wa Huduma za Maji, Nishati na Bidhaa za Petroli Sura Namba 414, Sheria ya Hifadhi ya Petroli Sura Namba 392 na Sheria ya Kusambaza Nishati Vijijini, Sura Namba 321. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kumi na tatu. Sehemu ya kwanza, inahusu masuala ya utangulizi, kama vile jina na tarehe ya

kuanza kutumika kwa Muswada wenyewe. Sehemu ya pili, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura Namba ya 147 katika vifungu namba 124, 141 na Jedwali la Nne kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha Kifungu cha 124 ili kwanza, kufuta kifungu kidogo cha (1A) kinachoweka sharti la kuweka alama ya *for export only* katika bidhaa zinazouzwa nje ya nchi, sharti hili limeonekana kukwamisha juhudi za kuongeza mauzo nje badala ya kuhamasisha. Pili, kuweka kifungu kipya cha 124 (1A) kinachotambua kisheria utaratibu uliopo hivi sasa wa kuirejeshea Serikali ya Mapinduzi Zanzibar makusanyo ya Ushuru wa Bidhaa *(excise duty)* kwa bidhaa zinazozalishwa Tanzania Bara na kuuzwa au kutumika Zanzibar. Aidha, utaratibu huu ndio unaotumika hivi sasa ambapo Hazina huirejeshea Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kodi husika. Marekebisho haya yana lengo la kuhalalisha kisheria utaratibu huu na vile vile kutoa mamlaka kwa *TRA* kuwasilisha kodi husika moja kwa moja Hazina - SMZ bila kupitishia Hazina - SMT kama ilivyokuwa hivi sasa. Pia kufuta neno *date* katika kifungu kidogo cha (5A) na badala yake kuweka neno *year* ili kuiwezesha *TRA* kutambua umri wa magari kutokana na mwaka ambao gari lilitengenezwa badala ya utaratibu wa sasa wa kutambua gari kwa tarehe ya gari iliyotengenezwa ambapo hutoa mwanya wa ukwepaji kodi.

(b) Kurekebisha kifungu cha 141 (2)(c) kwa kuongeza maneno *and the Value Added Tax Act* ili kurasimisha katika Sheria hii kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwenye thamani ya bidhaa wakati wa kukokotoa ushuru wa bidhaa. Utaratibu huu ndio unaotumika hivi sasa lakini ulikuwa bado haujawekwa kisheria.

(c ) Kurekebisha, kwa asilimia saba viwango vya Ushuru wa Bidhaa kwa bidhaa zinazotozwa ushuru huo. Kiwango hiki cha asilimia saba kinakaribia kiwango cha mfumuko wa bei. Aidha, marekebisho haya ni kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ambapo ushuru huu utaongezwa kila mwaka kwa kiwango cha mfumuko wa bei ili kulinda thamani halisi ya mapato ya Serikali kutoka kwenye vyanzo hivi. Viwango vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Vinywaji baridi kutoka shilingi 45 kwa lita hadi shilingi 48.00 kwa lita;

(ii) Bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa kutoka shilingi 161 kwa lita hadi shilingi 173 kwa lita;

(iii) Bia nyingine zote kutoka shilingi 274 kwa lita hadi shilingi 294 kwa lita;

(iv) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25 kutoka shilingi 878 kwa lita hadi shilingi 940 kwa lita; na

(v) Vinywaji vikali kutoka shilingi 1,302 kwa lita hadi shilingi 1,394 kwa lita.

(d) Kurekebisha viwango vya Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa za mafuta ya petroli kama ifuatavyo:-

(i) Petroli (*MSP* na *MSR*) kutoka shilingi 315 kwa lita hadi shilingi 339 kwa lita;

(ii) Dizeli *(GO)* kutoka shilingi 292 kwa lita hadi shilingi 314 kwa lita;

(iii) Mafuta ya taa *(IK)* yatabakia shilingi 52 kwa lita baada ya Serikali kuzingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2007/2008;

(iv) Mafuta mazito ya mitambo *(HFO)* kutoka shilingi 109 kwa lita hadi shilingi 117 kwa lita; na

(v) Dizeli nzito ya kuendeshea mitambo viwandani *(IDO)* kutoka shilingi 366 kwa lita hadi shilingi 392 kwa lita.

(e) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo:-

(i) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 4,462 hadi shilingi 4,775 kwa sigara elfu moja;

(ii) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 10,529 hadi shilingi 11,266 kwa sigara elfu moja;

(iii) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (i) na (ii) kutoka shilingi 19,195 hadi shilingi 20,460 kwa sigara elfu moja;

(iv) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara *(cut filler)* kutoka shilingi 9,657 hadi shilingi 10,333 kwa kilo; na

(v) Ushuru wa Bidhaa kwa *Cigar* unabaki kuwa asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha Kifungu cha 20(1) na (2) ili kurefusha muda wa uhai wa leseni za ajira kwa makundi ya wafanyakazi wa *casino (key and support employees)* kutoka mwaka mmoja hadi miaka miwili ili kuondoa usumbufu kwa makampuni yanayoajiri wafanyakazi hao.

(b) Kurekebisha kifungu cha 24(1) kwa kufanya marekebisho ya marejeo *(cross reference)* kwa kufuta kifungu cha 15 na badala yake kuweka kifungu cha 16.

(c) Kufuta kifungu cha 32 kwa kuweka utaratibu mpya ili kuwezesha Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kukusanya kodi ya *(gaming tax)* kutoka katika *casino* kila wiki badala ya utaratibu wa sasa wa kukusanya kodi hiyo kwa mwezi. Hatua hii ina lengo la kudhibiti ukusanyaji wa kodi hii ambayo ni chanzo kimojawapo kikuu cha mapato ya

Serikali, kama nilivyobainisha katika hotuba ya Bajeti kwamba Bodi ya Michezo ya Kubahatisha iliweza kukusanya mapato ya shilingi bilioni 2.2 katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2006/2007 chini ya utaratibu mpya wa Bodi hii kukusanya kodi husika kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(d) Kurekebisha kifungu cha 41 kwa kuongeza kifungu kidogo cha sita ili kutoruhusu utoaji wa leseni ya kuendesha Bahati Nasibu ya Taifa kwa *product* ya aina moja kwa zaidi ya Kampuni au mtu mmoja. Utaratibu huu ndio unaotumika duniani kote kwenye michezo ya aina hii.

(e) Kurekebisha kifungu cha 70 ili kuwaruhusu watoto wa umri wa chini ya miaka 18 kushiriki katika michezo ya kubahatisha yenye lengo la kutangaza *(promote)* bidhaa zinazoruhusiwa kutumiwa na watoto kisheria kama vile vinywaji baridi.

(f) Kurekebisha kifungu cha 85 kwa kuongeza kifungu kidogo cha 2(f) ili kumwezesha Waziri anayesimamia Sheria hii kutunga Kanuni zitakazotoa mamlaka kwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kutoa adhabu za kiutawala *(administrative measures)* kwa watu au Kampuni zinazokiuka kanuni na taratibu za Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 kama ifuatavyo:-

(a) Kufuta maneno *section 3(1)(a) and (b)* yaliyoainishwa katika kifungu cha 98(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato kama rejea *(cross reference)* na kuweka maneno *section 4(1) (a) and (b).*

(b) Kurekebisha jedwali la kwanza ili kupunguza kiwango cha chini cha kukokotoa kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 18.5 inayotozwa hivi sasa hadi asilimia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano, inapendekeza kufanyia marekebisho kifungu cha 86(1) cha Sheria ya Madini ili kuondoa sharti la kuthibitisha kulipa kodi ya mazingira kwa wazalishaji wa chumvi wanaopata msamaha wa mrabaha. Hivi sasa utaratibu wa kutoza kodi ya mazingira bado haujakamilika na hivyo kusababisha wazalishaji wa chumvi kushindwa kutoa uthibitisho huu na kuwasababishia usumbufu usio wa lazima.

Sehemu ya sita, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 12 cha Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha saba ili kumpa Waziri wa Fedha mamlaka ya kufanya marekebisho kwenye jedwali la Sheria hii linaloainisha orodha ya mifuko maalumu iliyoanzishwa chini ya Sheria ya zamani ya *Exchequer and Audit Ordinance* sura namba 21 ya mwaka 1961 na kutambuliwa na Sheria ya Fedha za Umma. Aidha, marekebisho haya yatafanyika kwa utaratibu wa kuandaa amri itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba, inapendekeza kufanya marekebisho katika jedwali la pili la Sheria ya Ushuru wa Mafuta na Barabara sura ya 220 ili kuongeza

ushuru wa mafuta ya petroli na dizeli kutoka shilingi 100 hadi shilingi 200 kwa lengo la kuongezea uwezo wa kifedha Mfuko wa barabara kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane, inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Bodi ya Rufaa za Kodi Sura 408 kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha Kifungu cha 3 ili kutoa ufafanuzi kuhusu tafsiri halisi ya maneno mbalimbali yaliyotumika chini ya Sheria hii.

(b) Kurekebisha Kifungu cha 6 (2) ili kuweka bayana majukumu ya Katibu wa Bodi ya Rufaa za Kodi yanayohusu masuala ya Kimahakama kama yalivyoainishwa katika Sheria hii.

(c) Kurekebisha Kifungu cha saba kwa kuongeza kifungu kipya cha 7A ili kuweka bayana mamlaka ya Bodi ya Rufani za Kodi kushughulikia malalamiko ya walipa kodi yatokanayo na maamuzi ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato na kusisitiza kwamba malalamiko yanayohusu kifungu cha 12 cha Sheria hii ni budi kwanza yawasilishwe kwa Kamishna Mkuu wa *TRA* badala ya kuwasilishwa moja kwa moja kwa Bodi.

(d) Kurekebisha kifungu cha 10(2) ili kuweka bayana majukumu ya Msajili wa Baraza la Rufani za kodi yanayohusu masuala ya Kimahakama kama yalivyoainishwa katika Sheria hii.

(e) Kurekebisha Kifungu cha 13 (3) ili kuweka neno sahihi makadirio badala ya neno pingamizi liliko hivi sasa.

(f) Kurekebisha Kifungu cha 14 ili kuweka bayana maamuzi mengine ya Kamishna Mkuu wa *TRA* ambayo yanaweza kuombewa rufaa moja kwa moja kwenye Bodi.

(g) Kurekebisha Kifungu cha 15(1) ili kuainisha kwa usahihi marejeo ya vifungu husika *(cross referencing)*.

(h) Kurekebisha Kifungu cha 16(1) na (3), marekebisho haya yanalenga kuainisha maamuzi ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato ambayo yanaweza kuombewa rufaa kwenye Bodi. Aidha, katika sehemu hii inapendekezwa kurekebisha Kifungu cha 16(4) ili kuweka utaratibu wa kuomba rufaa kutoka kwenye Bodi kwenda kwenye Baraza la Rufani za Kodi ambapo inapendekezwa kuwa muda wa siku thelathini za kuwasilisha rufaa kwenye Baraza uanze kuhesabiwa kuanzia tarehe ambayo muomba rufaa atapokea kumbukumbu zote za mwenendo wa shauri na hukumu ya Bodi. *(Makofi)*

(i) Kurekebisha Kifungu cha 26 (1), (2) na (3) ili kuainisha mamlaka ya Katibu ya kutoza gharama za kuendeshea shauri linalowasilishwa mbele ya Bodi kama ilivyo kwa Msajili kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tisa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kama ifuatavyo:-

(a) Kifungu cha 11 kwa kuongeza kifungu kidogo cha 2 ili kuweka sharti kwamba, msamaha utakaotolewa kwa mtu au kampuni chini ya Sheria hii utaondolewa endapo bidhaa zilizosamehewa kodi zitauzwa kwa mtu au kampuni ambayo haistahili msamaha husika; Sheria ilivyo hivi sasa sharti hili linahusu Asasi Zisizo za Serikali *(NGO's)* pekee.

(b) Kufuta kifungu cha 35 cha Muswada kinachopendekeza marekebisho ya kifungu cha 17 cha Sheria hii, na kuendelea na utaratibu uliopo hivi sasa.

(c ) Jedwali la Pili (linalohusu bidhaa na huduma zilizosamehewa kodi *(exempt supplies and imports)*:-

Kwanza, kurekebisha aya ya kwanza kwa kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa vyakula, mazao ya kilimo na mifugo zinapouzwa na kutumika katika kantini maalumu zinazotoa huduma kwa Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania badala ya utaratibu wa sasa ambapo vyakula na bidhaa hizi hutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani vikitumika katika kantini na migahawa inayotoa huduma kwa wanajeshi.

Pili, kurekebisha aya ya 3(6) ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye *diapers* na mifuko ya usafi kwa matumizi ya tiba.

Tatu, kufuta aya ya 20 ili kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyuzi ghafi zinazotengenezwa nchini *(yarn)* ili kuwawezesha wazalishaji kurejeshewa *VAT* wanayolipa kwenye huduma kama umeme, usafirishaji na kadhalika na hivyo kuwaongezea uwezo wa ushindani.

Nne, kuongeza aya ya 24 kwa kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mitungi ya kuzimia moto ili kupunguza gharama na kuhamasisha matumizi ya vifaa hivyo katika kupambana na majanga ya moto.

(d) Jedwali la Tatu, kurekebisha aya ya nane kwa kuongeza aya mpya ya 8A ili unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani unaotolewa kwa shughuli za utafutaji na uchimbaji madini uhuishe pia shughuli za utafutaji gesi na mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi, inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Mauzo Nje ya Nchi, sura namba 196 kwenye Jedwali kwa kubadili mfumo wa kutoza ushuru wa kuuza ngozi ghafi kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 20 na kuwa asilimia 40 au shilingi 400 kwa kilo kutegemea kiwango kipi ni kikubwa. Hatua hii inatarajia kuiongezea mapato Serikali kutoka shilingi bilioni 1.3 kwa mwaka hadi shilingi bilioni 2.6 kwa mwaka ambapo fedha zitakazopatikana zitahifadhiwa katika Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo *(Livestock Development Fund)* ambao Serikali iliwasilisha Bungeni hati ya kuanzisha mfuko huu mnamo tarehe 19 Julai, 2007 na Bunge kuridhia. *(Makofi)*

Aidha, fedha zitakazopatikana zitatumika katika kuendeleza sekta ya ngozi ikiwemo kuimarisha viwanda vya kusindika ngozi, uboreshaji wa shughuli za ugani, machinjio, kuendeleza wafugaji na kadhalika.

Mapendekezo yanayopendekezwa yamezingatia uwiano katika mifumo ya utozaji ushuru ngozi ghafi inayouzwa nje ya nchi na majirani zetu wa Kenya na Uganda ili kupunguza biashara ya magendo ambayo itaipotezea Serikali mapato. Aidha, hatua hii itasaidia upatikanaji wa malighafi ya ngozi hivyo kulinda viwanda vya kusindika ngozi nchini, kuongeza ajira kwa wananchi na kuipatia nchi yetu mapato ya fedha za kigeni kwa kuuza ngozi zilizosindikwa na bidhaa za ngozi nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi na moja inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Utoaji wa Huduma za Maji, Nishati na Bidhaa za Petroli sura namba 414 kama ifuatavyo:-

(i) Katika kifungu cha 7 kwa kufuta kifungu kidogo cha 1(d) ili kuipa uwezo *EWURA* kusimamia na kuratibu bei ya bidhaa za petroli na gesi asilia. Sheria hii kama ilivyo hivi sasa inatoa ukomo kwa *EWURA* katika kusimamia na kuratibu bei ya bidhaa za petroli na gesi asilia. Kifungu cha 7(1)(d) kinachopendekezwa kufutwa kina mapungufu ambapo kinatoa utaratibu wa kipekee kwa *EWURA* kusimamia na kuratibu taratibu za usambazaji wa bidhaa hizi pekee, hata hivyo kifungu hakitoi mamlaka kwa *EWURA* kusimamia bei. *(Makofi)*

(ii) Kurekebisha kifungu cha 40(3) ili kuongeza kiwango cha faini kutoka shilingi laki tano ya sasa hadi kiasi cha shilingi milioni tatu kwa mtu au kampuni itakayokiuka masharti ya kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(iii) Kurekebisha kifungu cha 42(1) kwa kuongeza faini ya mtu au kampuni itakayokiuka masharti ya sheria hii kutoka kiasi kisichozidi shilingi milioni tatu hadi kiasi kisichopungua shilingi milioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho haya yanalenga; Kwanza, kushughulikia mapungufu yaliyoko katika Sheria hii kwa kuipa Mamlaka ya Kusimamia Utoaji wa Huduma za Maji, Nishati na Bidhaa za Petroli *(EWURA)* nguvu za kisheria ili iweze kusimamia na kuratibu ipasavyo bei ya bidhaa za petroli kwa lengo la kuwalinda watumiaji wa bidhaa za petroli nchini dhidi ya upandishaji holela wa bei ya bidhaa hizi unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara hususan baada ya Serikali kuongeza ushuru wa barabara kwa petroli na dizeli katika Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2007/2008. Aidha, hatua hii ni utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alilolitoa wakati akihutubia Taifa hapa Mjini Dodoma mnamo tarehe 1 Agosti, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kumi na mbili inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Petroli sura namba 392 kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza, kurekebisha kifungu cha tatu, kinachohusu tafsiri kwa kuingiza tafsiri mpya ya maneno *economic regulation* na *regulated supplier* na kifungu cha 4A kinachohusu mamlaka na kazi za *EWURA* kwa kuongeza neno *economic* kati ya maneno *technical service.* Lengo la marekebisho haya ni kuipa nguvu za kisheria *EWURA* kuweza kusimamia ipasavyo sekta ya bidhaa za petroli kwenye masuala yanayogusa uchumi wa nchi na yenye uhusiano wa moja kwa moja na sekta ya petroli ikiwemo bei za bidhaa za petroli na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria kama ilivyo hivi sasa inaipa mamlaka ya *EWURA* kusimamia shughuli zinazohusu masuala ya kiufundi na kiusalama pekee katika sekta ya bidhaa za petroli. Aidha, marekebisho yanayopendekezwa itawezesha mamlaka ya *EWURA* kwa kushirikiana na wadau wa sekta husika kubainisha vigezo *(formula)* vitakavyotumika katika kufikia bei ya bidhaa za petroli kwa kuzingatia pamoja na mambo mengine gharama za usafirishaji.

(b) Kurekebisha kifungu cha 6 ili kwanza, kufuta kigezo cha kutoza faini kwa siku, pili, kuongeza kiwango cha faini kutoka shilingi 5,000/= ya sasa hadi kiasi kisichopungua shilingi milioni moja.

(c ) Kufuta kifungu cha 7 kinachobainisha faini ya shilingi elfu tano kwa kila siku ambayo taratibu za kisheria zimekiukwa na mtu au Kampuni inayomiliki leseni au kibali kinachotolewa kwa mujibu wa sheria hii na kuweka kifungu kipya cha 7 ili kuainisha adhabu mpya kwa makosa haya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu SPika, kwanza, faini ya shilingi milioni moja itatozwa kwa kosa linapotendeka kwa mara ya kwanza; pili, adhabu ya faini ya shilingi milioni tano na kusitishwa leseni au kibali kwa kipindi cha miezi kumi na mbili endapo kosa litatendeka kwa mara ya pili; tatu, kufutwa kwa leseni au kibali cha biashara kosa litakapotendeka kwa mara ya tatu.

(d) Kurekebisha kifungu cha 8, kwanza kwa kuondoa sharti la kutoza faini kwa kila siku ambayo kosa limetendeka; pili kwa kuongeza kiwango cha faini kutoka shilingi 8,000/= ya sasa hadi kiasi kisichopungua shilingi milioni mbili kwa kosa.

(e) Kurekebisha kifungu cha 9, kwanza kwa kuondoa sharti la kutoza faini kwa kila siku ambayo kosa limetendeka; Pili kuongeza kiwango cha faini kutoka shilingi elfu moja ya sasa hadi kiasi kisichopungua shilingi milioni mbili kwa kosa.

(f) Kurekebisha kifungu cha 10 kwa kuongeza kifungu kipya cha 10A ili kuainisha adhabu kwa mtu au kampuni zitakazokiuka maagizo yatakayotolewa na *EWURA* katika utekelezaji wa shughuli zake. Inapendekezwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi milioni tatu au kifungo cha miaka mitano au faini na kifungo kwa pamoja.

(g) Kurekebisha kifungu cha 11 kwa kuongeza kiwango cha faini kutoka ya shilingi elfu ishirini ya sasa hadi faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni tano kwa wamiliki wa meli zinazotumika kubeba bidhaa za petroli endapo hawatatoa taarifa kwa Mamlaka za Bandari kila wanapoingia katika Bandari husika.

(h) Kurekebisha kifungu cha 12 kwa kuongeza kiwango cha faini kwa mtu au kampuni yoyote itakayokiuka kanuni zozote zilizotungwa kwa mujibu wa sheria hii kutoka faini ya shilingi 20,000/= ya sasa hadi kiasi kisichopungua shilingi milioni tano. Faini hii ni kwa makosa ambayo adhabu zake hazijaainishwa ndani ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya marekebisho katika Sheria hii yameongeza viwango vya faini kwa makosa mbalimbali. Hatua hii ni katazo *(deterent measure)* kwa baadhi ya wafanyabiashara wa bidhaa hii wasiofuata kanuni na taratibu za sheria hii na kuwasababishia watumiaji wa bidhaa hii usumbufu usio wa lazima.

Sehemu ya kumi na tatu na ya mwisho inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 19 Sheria ya Usambazaji wa Nishati Vijijini, sura namba 321; kwanza kwa kurekebisha kifungu kidogo cha 3(c) na (d) na kuingiza maneno *of all the value of electricity generated* ili kubainisha kwamba msingi *(base)* wa kutoza ushuru wa kiwango kisichozidi asilimia tano kwa wazalishaji umeme utakuwa ni thamani ya umeme wote uliozalishwa kwa kipindi husika, pili, kwa kuongeza kifungu kidogo cha 5 ili kumpa mamlaka Waziri wa Nishati na Madini kupitia Tangazo la Serikali kutoza ushuru wa kiwango kisichozidi asilimia 5 kwa watumiaji wa umeme kwa ajili ya kugharamia mfuko wa kusambaza Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa sheria hii iliyopitishwa na Bunge mwaka 2005 inampa mamlaka Waziri wa Nishati na Madini, kutoza ushuru usiozidi asilimia 5 baada ya mashauriano na Waziri wa Fedha. Hata hivyo sheria haijabainisha utaratibu wa kisheria utakaotumika katika kutangaza kiwango kilichokubalika kutozwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba baadhi ya hatua za kodi ambazo zilibainishwa katika hotuba ya Bajeti kwa mwaka 2007/2008 zimetekelezwa kisheria chini ya utaratibu maalumu wa Mawaziri wa sekta husika kutoa tangazo la Serikali *(GN)* kwa mujibu wa sheria husika. Hatua hizo ni pamoja na tozo mbalimbali zinazokusanywa na Wizara ya Maliasilia na Utalii, zilichapishwa kupitia *Government Notice* namba 159 ya tarehe 29 Juni, 2007 na *GN notice 161* iliyochapishwa tarehe 29 Juni, 2007 na ada ya mwaka leseni za magari kulingana na ujazo wa Injini zilizochapishwa kupitia *GN Notice* 162 ya tarehe 29 Juni, 2007.

Mwisho, kama nilivyoeleza hapo awali mengi ya marekebisho yanayopendekezwa Muswada huu ni utekelezaji kisheria wa pendekezo la Serikali ambao tayari yameridhiwa na Bunge lako Tukufu wakati wa kuhitimisha hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi baada ya kuchambua na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2007 *(The Finance Bill, 2007)* unaokusudia kuboresha mfumo wa kodi na ada mbalimbali kama zilizovyoainishwa katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Kamati imekubaliana na mapendekezo na marekebisho yote ya Muswada huu ambayo ni utekelezaji kisheria wa hatua kadhaa za mfumo wa kodi na ada mbalimbali kama zilivyoridhiwa na Bunge lako tukufu tarehe 22 Juni, 2007 wakati wa kuhitimisha hotuba ya Bajeti ya Serikali.

Aidha, Muswada huu unakusudia pia kufanyia marekebisho sheria 10 zinazohusu fedha, kodi na ushuru kwa lengo la kurekebisha au kufuta viwango vya kodi, ushuru na ada mbalimbali kama ilivyoelezewa vizuri na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wakati wa kuwasilisha Muswada wenyewe. Kamati yangu inatambua kuwa njia mojawapo muhimu inayotegemewe na Serikali katika kupata mapato yake ni kupitia kodi na ada mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka ya mapato Tanzania imefanyakazi nzuri kufanikisha jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha mwaka 2006/2007. Mamlaka ya mapato imeweza kukusanya zaidi ya malengo yaliyowekwa.

Pamoja na juhudi za Serikali katika ukusanyaji wa mapato, Kamati bado ina wasiwasi wa kuwepo na mianya ya kukwepa kulipa kodi kunakofanywa na baadhi ya wawekezaji, wazalishaji mali na wafanyabiashara wasiyo waaminifu. Hili linajidhihirisha na takwimu za ukusanyaji wa mapato ambapo katika kipindi cha miaka kumi iliyopita kumekuwa na ongezeko la mapato kutokana na hatua zinazochukuliwa na *TRA* kuziba mianya ya wakwepaji kodi.

Mheshimiwa Naibu Spka, ni matumaini ya Kamati kuwa mikakati ya kuwabana wakwepa kodi itaongezewa nguvu. Aidha, Serikali iweke mikakati ya kutoa elimu kwa wananchi na wadau mbalimbali kujua umuhimu na uwajibikaji wa kulipa wa kulipa kodi hasa baada ya urekebishaji wa sheria hizi mbalimbali zinazohusu mfumo wa kodi na ada mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa Serikali imekuwa ikipoteza mapato katika maeneo ya uvunaji wa magogo na vitalu vya kuwinda.

(a) Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua katika kuongeza udhibiti katika eneo la uvunaji wa bidhaa za misitu eneo la uvuvi hasa wa baharini, ule wa *Economic Exclusive Zone* pamoja na maeneo mengine ya ukwepaji kodi hasa madini.

(b) Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanyia marekebisho sheria za kodi za mauzo ya nje ya nchi kubadili mfumo wa kutoza kodi, ushuru wa kuuza ngozi ghafi kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 20 na kuwa asilimia 40 au shilingi 400 kwa kilo kutegemea kipi ni kikubwa. Hii itasaidia kukuza na kulinda viwanda vyetu, kuongeza thamani *(value addition)* na kuendeleza mfumo wa sekta ya ngozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa kumejitokeza mtindo wa upandishaji holela wa bei ya bidhaa za mafuta unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara hususan baada ya Serikali kuongeza ushuru wa barabara kwa petroli na dizeli katika Bajeti ya mwaka 2007/2008. Pamoja na kwamba *EWURA* wanafanyakazi nzuri ya kusimamia bei za mafuta ili ziendane na bei halisi ya nyongeza ya bei iliyoongezwa na Waziri wa Fedha, Kamati inaipongeza Serikali kuleta marekebisho katika sheria ya mamlaka ya kusimamia utoaji wa huduma za maji na bidhaa za petroli zinazolenga kuipa nguvu kisheria *EWURA* katika kusimamia taratibu za usambazaji matumizi na biashara hii ya bidhaa za mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kuongeza viwango vya adhabu ya faini kwa wamiliki wa vyombo vinavyotumika kusafirishia bidhaa za petroli na sehemu zinazotumika kuhifadhi bidhaa za petroli pia kampuni au mtu anayemiliki leseni au kibali cha kuendesha biashara ya bidhaa za petroli endapo watakiuka taratibu hizi ni wa kuungwa mkono. Eneo hili likidhibitiwa vyema litapunguza uharibifu mkubwa wa mitambo ya mashine au magari unaotokana na uharibifu wa uchanganyaji wa mafuta. Aidha, itasaidia kuziba mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali kwa ajili ya ukwepaji kodi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo mengi duniani wameanzisha mfumo wa kulipa kodi kwa kutumia vitambulisho vya uraia. Kamati inapendekeza Wizara ya Fedha, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani, wahakikishe kuwa katika mradi wa kutengeneza vitambulisho vya uraia wanaingiza utaratibu wa kutumia vitambulisho hivyo katika kurahisisha mfumo wa ukusanyaji kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake marekebisho yaliyofanyika leo yamelenga kwenye maeneo ya kwanza kuhamasisha ukuaji wa mauzo nje, pamoja na kuimarisha vyanzo vya upatikanaji wa mapato kwa *Zanzibar Revenue Authority*, pili kuongeza ufanisi katika taratibu za kibiashara zikihusiana na ushuru na kodi mbalimbali. Mikakati ya kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka bidhaa za mafuta, vinywaji baridi pamoja na sigara pamoja na michezo ya kubadilisha. Kamati inashauri mapato yatakayotokana na marekebisho ya sheria hizi yatumiwe vizuri kwa kufikia malengo tuliyojiwekea hususan katika ujenzi na ukarabati wa barabara nchini pamoja na yale maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Bajeti na mipango ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji, Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Ndugu Gray Mgonja, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ndugu Kitilya kwa kusaidia Kamati kufanikisha kujadili na kupitisha Muswada huu. *(Makofi)*

Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao makini ambayo kwa kiwango kikubwa imesaidia kuboresha Muswada huu. Kama ilivyo ada naomba nitumie fursa hii kuwatambua wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo,

Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mwenyekiti, Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir. *(Makofi)*

Naomba nikushukuru wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Spika, kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambao wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na Makatibu wa Kamati, Ndugu Anselm Mrema na Helen Mbeba, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kutumia muda vizuri, sasa nina matangazo. Kambi ya Upinzani, watasoma Jumatatu baada ya kipindi cha Maswali na Majibu, wao watatoa pia maoni yao, halafu tutaendelea na mjadala mpaka kipindi cha asubuhi halafu tutaendelea na hoja nyingine. Sasa wakati tuko kwenye Kamati ya Matumizi ya Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, alikuwa ametaka kwamba zile fedha zilizoongezeka shilingi bilioni 90 labda wangetoa kidogo wakalipa wakulima wa pamba. Baada ya kuamua mimi kuwa hiyo haiwezekani ameniandikia akifikiri kwamba hatukumwelewa kwa hiyo, akaona kama vile hakuridhika.

Sasa nimemwandikia kwamba kwa mujibu wa Kanuni zetu kifungu cha 81(4) hakiruhusu katika kipindi kile kubadili madhumuni ya fungu linalohusika. Nikamwambia kama ungekuwa umependa ungezungumza wakati wa mshahara wa Waziri, wewe ungeongelea pale, Waziri sijui angeahidi nini, sijui angesema nini. Lakini wakati alipokuwa anaulizia kifungu cha 81(4) kinakatazwa. Kwa hiyo, naomba hili lieleweke, isionekane sisi tunawaburuza wenzetu. Kwa hiyo, nadhani hiyo tumeelewana. *(Makofi)*

Lakini la pili, kesho Kamati ya Uongozi saa tano asubuhi kutakuwa na mkutano *(Steering Committee)* Wenyeviti wote. Halafu pia tulitangaza mchana kwamba tutakuwa na uchaguzi wa wenzetu wanaotaka kutuwakilisha kwenye Vyuo mbalimbali. Nadhani labda tulipotangaza hamkuwa wengi hawajachukua fomu. Jumatatu saa saba mchana ndiyo mwisho wa kurudisha fomu. Kwa hiyo, wale wanaotaka kushiriki basi wakachukue fomu kesho na siku ya Jumapili. Baada ya kusema hayo naahirisha Kikao mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu,*

*Tarehe 13 Agosti, 2007 saa tatu asubuhi)*